# KISWAHILI

## Mwongozo wa Mwalimu

## Kidato cha 5

## Mchepuo wa Lugha (LFK)

© 2022 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi

Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi.

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# Dibaji

Mwalimu mpendwa,

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima kwa kutoa mwongozo wa mwalimu kwa kidato cha tano katika ngazi ya juu ya elimu ya sekondari. Mwongozo huu ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unamwezesha mwanafunzi kuendeleza mawazo yake na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi. Wanafunzi, kwa msaada wa wakufunzi, watapata stadi za lugha zinazofaa zitakazowawezesha kutumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wataonyesha tofauti siyo tu katika maisha yao binafsi bali pia hata kwa taifa.

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira

yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu jukumu lako litakuwa:

- Kuandaa masomo yako na vifaa vya ufundishaji vinavyofaa;
- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikiano ya wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwa ufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu;
- Kushirikisha wanafunzi kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya mijadala, utafiti, mazoezi ya utafiti na kazi za kibinafsi;
- Kutoa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao, kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatazo, ubunifu na uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano;
- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani;
- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti;
- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu za tathmini zinazoegemea katika uwezo wa wanafunzi;
- Kuutumia mwongozo kutakusaidia katika kazi yako ya kufundisha kwani yaliyomo katika mwongozo huu wa mwalimu yanaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi;
- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani;
- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti;
- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu za tathmini zinazoegemea katika uwezo wa wanafunzi;
- Kuutumia mwongozo kutakusaidia katika kazi yako ya kufundisha kwani yaliyomo katika mwongozo huu wa mwalimu yanaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi.

Ingawa mwongozo huu wa mwalimu una majibu kwa kila kazi zote zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi, unaombwa kupitia kila swali na kazi kabla ya kutathmini.

Ninapenda, kwa moyo wote, kutoa shukrani zangu kwa watu wote walioshiriki kutoa mchango wao wa kuboresha mwongozo huu wa mwalimu, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi ( REB/CTLR) walioandaa mchakato wa kazi hii tangu ilipoanzishwa.

Pongezi maalumu ziwaendee walimu wa ngazi tofauti kwa msaada wao wa kuendeleza na kukamilisha zoezi hili.

Maoni au mchango wowote wa mawazo unakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo mengine yatakayofuata baadaye.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, REB.**

# Shukrani

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki cha mwongozo wa Mwalimu. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu za kwanza ni kwa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki. Pia ninapenda kutoa shukrani kwa walimu wa ngazi zote kwa juhudi zao katika ufanikishaji wa kazi hii ya thamani.

Aidha, natoa shukrani kwa uongozi wa shule mbalimbali nchini Rwanda kwa kuwaruhusu walimu kushiriki katika kukiandaa na hata kukikamilisha kitabu hiki.

**Joan Murungi**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (REB- CTLR)**

## YALIYOMO


Dibaji ..... iii

Shukrani ..... vi

YALIYOMO ..... vii

SEHEMU I. UTANGULIZI WA JUMLA ..... 10

1.1. MUUNDO WA MWONGOZO WA MWALIMU ..... 10

1.2. MWELEKEO WA UFUNDISHAJI ..... 11

1.2. 1. Mwelekeo wa Kuendeleza Uwezo ..... 11

1.2.2 Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka ..... 12

1.2.3. Mwongozo wa Tathmini ..... 14

1.2.4. Mbinu na Mikakati ya Kuendeleza Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 15

1.2.5. Mbinu za Ufundishaji Zinazokuza Shughuli ya Ujifunzaji Shirikishi ..... 15

SEHEMU II: SAMPULI ZA MAANDALIO YA MASOMO ..... 17

SEHEMU YA III: UUNDAJI WA MADA ..... 30

MADA KUU YA 1: UWANJA WA FASIHI KAMA SANAA ..... 30

MADA NDOGO: NADHARIA YA FASIHI SIMULIZI KATIKA KISWAHILI ..... 30

1.1 Uwezo upatikanao katika mada ..... 30

1.2 Ujuzi wa awali ..... 30

1.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake ..... 30

1.3.1.Kidokezo cha mada ..... 30

1.3.2.Maelekezo kuhusu kidokezo cha mada ..... 31

1.4. Orodha ya masomo ..... 31

SOMO LA 1: TANZU ZA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI NA VIPERA VYAKE ..... 34

SOMO LA 2: DHANA YA HADITHI SIMULIZI ..... 43

SOMO LA 3: DHANA YA METHALI ZA KISWAHILI ..... 44

SOMO LA 4 : DHANA YA NAHAU NA MISEMO YA KISWAHILI ..... 51

SOMO LA 5: DHANA YA VITENDAWILI VYA KISWAHILI ..... 58

SOMO LA 6: DHANA YA USHAIRI SIMULIZI WA KISWAHILI ..... 65

1.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ..... 69

1.5.1.Maelezo ya ziada kwa mwanafunzi ..... 69

1.5.2.Maelekezo ya ziada kwa mwalimu ..... 73

1.6. TATHMINI YA MADA YA KWANZA ..... 77

1.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI ..... 78

1.7.1. Kazi za urekebishaji ........ 78
1.7.2.Kazi za uimarishaji ........ 79
1.7.3. Kazi za wanafunzi wenye uelewa wa haraka ........ 80
MADA KUU YA 2: UHAKIKI NA UWASILISHAJI KATIKA FASIHI SIMULIZI ........ 82
MADA NDOGO: UHAKIKI WA FANI NA MAUDHUI KATIKA FASIHI SIMULIZI ........ 82
2.1. Uwezo upatikanao katika mada ........ 82
2.2. Ujuzi wa awali ........ 82
2.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake ........ 82
2.3.1. Kidokezo cha mada ........ 82
2.3.3.Maelekezo kuhusu kidokezo cha mada ........ 82
2.4. Orodha ya masomo ........ 83
SOMO LA 1: DHANA YA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI KATIKA KISWAHILI ........ 86
SOMO LA 2 : UHAKIKI WA HADITHI KATIKA KISWAHILI ........ 93
SOMO LA 3: UHAKIKI WA METHALI KATIKA KISWAHILI ........ 99
SOMO LA 4: UHAKIKI WA VITENDAWILI KATIKA KISWAHILI ........ 107
SOMO LA 5: UHAKIKI WA NAHAU NA MISEMO KATIKA KISWAHILI ........ 113
SOMO LA 6: UHAKIKI WA MASHAIRI SIMULIZI KATIKA KISWAHILI ........ 118
2.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ........ 124
2.5.1. Maelekezo ya ziada kwa mwalimu ........ 124
2.6. TATHMINI YA MADA YA PILI ........ 124
2.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI ........ 126
2.7.1. Kazi za urekebishaji ........ 126
2.7.2. Kazi za uimarishaji ........ 126
2.7.3. Kazi za wanafunzi wenye uelewa wa haraka ........ 127
MADA KUU YA 3: MAWASILIANO RASMI ........ 130
MADA NDOGO: UTUNGAJI WA BARUA RASMI, SIMU NA MATANGAZO ........ 130
3.1. Uwezo upatikanao katika mada ........ 130
3.2. Ujuzi wa awali ........ 130
3.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake ........ 130
3.3.1. Kidokezo cha mada ........ 130
3.3.3. Maelekezo kuhusu kidokezo cha mada ........ 130
3.4. Orodha ya masomo ........ 131
SOMO LA 1: DHANA YA BARUA RASMI NA UTUNGAJI WAKE ........ 133

SOMO LA 2: DHANA YA SIMU ........ 141
SOMO LA 3: UANDISHI WA MATANGAZO ........ 147
3.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ........ 153
3.5.1. Maelekezo ya ziada kwa mwalimu ........ 153
3.5. TATHMINI YA MADA YA TATU ........ 154
3.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI ........ 157
3.7.1. Kazi za urekebishaji ........ 157
3.7.2.Kazi za uimarishaji ........ 158
3.7.3. Kazi kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka ........ 159
MADA KUU YA 4: KUSOMA NA KUFASILI ........ 162
MADA NDOGO: UFAHAMU NA UFUPISHO ........ 162
4.1. Uwezo upatikanao katika mada ........ 162
4.2. Ujuzi wa awali ........ 162
4.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake ........ 162
4.3.1. Kidokezo cha mada ........ 162
4.3.3. Maelekezo kuhusu kidokezo cha mada ........ 163
4.4. Orodha ya Masomo ........ 163
SOMO LA 1: DHANA YA UFAHAMU WA HABARI NA TARATIBU ZAKE ........ 166
SOMO LA 3: DHANA YA UFUPISHO WA HABARI NA MBINU ZAKE ........ 173
4.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ........ 178
4.5.1. Maelekezo ya ziada kwa mwalimu ........ 178
4.6. TATHMINI YA MADA YA NNE ........ 181
4.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI ........ 181
4.7.1.Kazi za urekebishaji ........ 181
4.7.2.Kazi za uimarishaji ........ 182
4.7.3.Kazi za wanafunzi wenye uelewa wa haraka ........ 183
MAREJEO ........ 186

## SEHEMU I. UTANGULIZI WA JUMLA

### 1.1. MUUNDO WA MWONGOZO WA MWALIMU

Kitabu hiki ni mwongozo wa mwalimu katika mchakato wa ufundishaji wa somo la Kiswahili, kidato cha tano, mchepuo wa lugha katika shule za sekondari nchini Rwanda. Kimetayarishwa kwa mwelekeo wa mtaala uegemeao katika uwezo. Mwongozo huu wa mkufunzi unaundwa na sehemu tatu.

Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla ambao unajishughulisha na namna ya kufundisha na kujifunza Kiswahili, kukuza uwezo wa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji, jinsi ya kushughulikia masuala mtambuka na inatoa mwongozo kuhusu tathmini. Sehemu ya pili ni sampuli ya andalio la somo ambayo inaonyesha vipengele vya somo na jinsi ya kuandaa somo hilo. Sehemu ya tatu inahusu uundaji wa mada tofauti. Sehemu hii inatoa taarifa kuhusu uwezo upatikanao katika mada, ujuzi wa awali wa wanafunzi kuhusu mada inayofundishwa, mwongozo kuhusu vidokezo, orodha ya masomo, mwongozo kuhusu namna ya kufanikisha masomo mbalimbali, maelezo ya ziada, kazi ya utafiti, tathmini ya mada, kazi za ziada ambazo zinajumuisha: kazi za urekebishaji, kaziza uimarishaji na kazi kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka. Majibu ya kazi zote, tathmini ya mada na kazi za ziada yanapatikana katika kitabu hiki.

Aidha, mwongozo huu wa mwalimu umezingatia mada kuu nne kama ifuatavyo:

1. Nadharia ya fasihi simulizi katika Kiswahili
2. Fani na maudhui katika fasihi simulizi ya Kiswahili
3. Utungaji wa barua rasmi, simu na matangazo
4. Ufahamu na ufupisho.

Kila mada hujigawa katika mada ndogo na kila mada ndogo katika masomo mbalimbali.

Mwongozo wa mwalimu hutia mkazo kwenye majibu ya kazi zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi pamoja na mbinu za kufundishia kwa kila kazi

### 1.2. Mwelekeo wa ufundishaji

Kinyume na Mtaala Uegemeao katika Ujuzi, Mtaala Uegameao katika Uwezo huwa na lengo kuu la kumfanya mwanafunzi mlengwa wa somo ashiriki kimatendo katika mchakato wa ujifunzaji wake. Hapa mwalimu hatawali somo bali wajibu wake ni kumuelekeza au kumwongoza mwanafunzi katika somo lote. Kwa ufupi, mwanafunzi hachukuliwi kama mgeni katika somo lake bali huchukuliwa kama mshiriki-mlengwa.

#### 1.2. 1. Mwelekeo wa Kuendeleza Uwezo

Katika mchakato wa ujifunzaji wa Kiswahili, uendelezaji wa uwezo wa jumla kwa mwanafunzi unapewa kipaumbele sana. Uwezo huo wa jumla wa kuendelezwa ni kama vile tafakuri tunduizi, ubunifu, utafiti, utatuzi wa matatizo na ushirikiano. Haya yote yanafanikishwa katika ufundishaji kwa lengo la kuhakikisha kuwa mahitaji ya mwanafunzi yametoshelezwa. Hivyo basi, wanafunzi watapewa kazi mbalimbali zinazohitaji ushirikiano kati yao ili kukamilisha kufanya tafiti zao au kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika maisha. Kila ujifunzaji na ufundishaji wa kila somo lililoandaliwa unazingatia nafasi ya kumjengea mwanafunzi stadi sahihi za mawasiliano katika miktadha mbalimbali ya kimaisha kama mtu aliye na uwezo wa kushirikiana na watu mbalimbali katika miradi tofauti ya kijamii na kimaendeleo. Uwezo unaotakiwa katika kumjenga mwanfunzi utajikita katika mazeozi ya kusoma, kusikiliza, kuzungumza na kuandika kama njia muhimu za kudumisha mawasiliano katika lugha ya Kiswahili.

Ili kumwezesha kuwasiliana kwa usahihi na katika hali inayoweza kuyatatua matatizo yanayowakabili wanafunzi, mwalimu akumbuke kumwezesha katika kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Pia ufundishaji unaotarajiwa katika masomo husika ni kumwezesha mwanafunzi kupata menejimenti yake kama mtu binafsi aliye na malengo mahususi na pia katika mahusiano yake na watu wengine. Haya ni kusema kwamba mada mbalimbali zilizojadiliwa zinajenga muktadha wa kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kukuza na kuendeleza uwezo wa kila mwanafunzi.

Katika uendelezaji wa uwezo huu, mwanafunzi hushirikishwa katika kuyaelewa vyema maisha ya nchi na matatizo yake ya kila siku. Ndiyo sababu jambo la masuala mtambuka hutiliwa mkazo ndani ya kila somo. Ukweli ni kwamba uwezo peke yake wa mwanafunzi hauwezi kuendelezwa wakati ambapo masuala mtambuka yamewekwa pembeni. Masuala mtambuka yote manane

yanayojitokeza katika mtaala wa taifa kama vile: Mafunzo dhidi ya mauaji ya kimbari, mazingira na maendeleo endelevu, usawa wa kijinsia, mafunzo kuhusu ujinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili mema, mafunzo kuhusu uzalishaji mali, desturi ya usawa, mafunzo kuhusu elimu isiyo na ubaguzi. Uingizaji wa masuala mtambuka katika somo hufaulu zaidi kutokana na jinsi mazoezi ya kimajadiliano yalivyotayarishwa na mwalimu.

### 1.2.2 Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka

Katika kitabu hiki, imetolewa mifano ya jinsi ya kushughulikia masuala mtambuka katika somo la Kiswahili, na mwalimu awaongoze wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia masuala mtambuka yafuatayo:

- **Elimu jumuishi:** Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu analazimika kubainisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kuwaandalia mazoezi kufuatana na mahitaji yao. Shirikisha wanafunzi wote katika kazi walizoandaliwa bila upendeleo.

**Mfano:** Mpatie mwanafunzi aliye na ulemavu wa mwili (asiyeona) jukumu la kuongoza mjadala. Mtafutie mahali pa kukaa na vifaa vya kutumia kufuatana na mahitaji yake.

- **Usawa wa kijinsia:** Katika mchakato wa ufundishaji, mkufunzi analazimika kuandaa mazoezi ambayo yanashirikisha wavulana na wasichana na kuwasaidia kutumia uwezo wao ipasavyo.

  Hakuna kazi ambayo inatarajiwa kuwa ya msichana au mvulana.Walimu wangehakikisha kwamba wasichana na wavulana wanachukua nafasi sawa wakishiriki katika kazi za makundi, mijadala na midahalo.

- **Elimu kuhusu amani na maadili:** Katika mchakato wa ufundishaji, mwalimu analazimika kuwahimiza wanafunzi kuwa na uvumilivu, ushirikiano, kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa pamoja, kusaidiana kwa pande zote, kuheshimu maoni ya wengine, kuheshimu maagizo na kuwepo kwa mazingira mazuri ya kujifunzia.

- **Mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji:** Katika mchakato wa ufundishaji, wanafunzi wanalazimika kutunza vizuri vifaa vya shuleni na kutoviharibu kama vile vitabu, madaftari, madawati, n.k. Mwalimu pia anaweza kuwasaidia kuchagua vitabu vya

kusoma vinavyohusiana na masomo yao lakini vinavyokubaliwa katika mfumo wa elimu ya Rwanda.

- **Mazingira na maendeleo endelevu:** Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji masuala ya mazingira na maendeleo endelevu yatashughulikiwa kama ifuatavyo:

- Mwalimu aeleze wanafunzi umuhimu wa mazingira safi iwe nyumbani, shuleni, n.k.
- Wanafunzi wasichafue madarasa kwa kutupa karatasi au uchafu wowote katika mazingira ya shule wakati wa kusoma na baada ya masomo. Washauriwe kutotema mate au kupenga ovyo mahali popote.
- Mwalimu aweke maagizo ya kufanya usafi darasani na katika busitani za shule.

- **Mafunzo kuhusu uzalishajimali/ujasiriamali:** Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji mafunzo kuhusu uzalishajimali/ujasiriamali yatashughulikiwa wakati ambapo: Wanafunzi wanao uwezo wa kutunga mashairi, hadithi na michezo ya kuigiza wakashiriki katika mashindano tofauti na kupewa zawadi au wakaunda klabu za michezo ya kuigiza na ambapo wanawaalika watu kutazama michezo ya kuigiza na kulipa pesa za kuingia (kiingilio). Hii inawasaidia wanafunzi kufahamu kuwa Kiswahili kinaweza kuwa chanzo cha shughuli za uzalishaji mapato na kujipatia ajira.

- **Elimu kuhusu ufahamu wa jinsia:** Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu atoe maagizo na kazi zisizochochea unyanyasaji wa kijinsia. Pia, anaweza kutoa kazi au vifungu vya habari vinavyoshughulikia afya ya uzazi na mpango wa kuboresha uzazi.

- **Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari:** Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu atoe kazi na mada za kuzungumzia au kujadili madhara ya mauaji ya kimbari kwa jamii na jinsi ya kutupilia mbali itikadi yake.

Mwalimu awasaidie wanafunzi kuingiza masuala mtambuka haya katika kila somo wanalojifunza na kutafuta suluhisho kuhusu masuala hayo.

### 1.2.3. Mwongozo wa Tathmini

Tathmini ni jambo muhimu sana katika njia hii ya ufundishaji na ujifunzaji. Lengo kuu la tathmini ni kupima maendeleo ya somo ambapo mwalimu huweza kuchagua aina ya tathmni kulingana na malengo yake.

- **Tathmini Endelezi**

Tathmini hii hulenga kupima jinsi ufundishaji na ujifunzaji unavyoendelea au kama makusudi au malengo ya ufundishaji na ujifunzaji yamefikiwa kwa kiwango fulani ili kuamua kuhusu uboreshaji wa baadaye. Tathmni hii inafanywa wakati masomo yangali yanaendelea na hulenga kuangalia uhusiano uliopo kati ya ufundishaji na ujifunzaji yaani uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Hujumuisha upimaji wa mwenendo wa somo kabla somo lifikie kikomo. Tathmini endelezi inapaswa kuwa na dhima mwafaka katika ufundishaji na ujifunzaji. Inambidi mwalimu kuwahamasisha wanafunzi kufanya mazoezi na majaribio binafsi, mazoezi ya makundi, kwa kutumia mbinu zinazoegemea kwenye uwezo, maadili na mwenendo mwema kulingana na kila somo husika.

- **Tathmini ya jumla**

Kila tathmini huwa na dhima yake katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, tathmini ya mwishoni mwa mada itafikiriwa na itafanyika mwishoni mwa mada nzima kabla ya kutangulia mada nyingine. Aidha, tathmini inayofanyika mwishoni mwa muhula na mwishoni mwa mwaka zitakuwa mojawapo ya tathmini za jumla na wakati huu hulenga kurekodi ujuzi, uwezo, maadili na mwenendo mwema miongoni mwa wanafunzi kiasi kwamba walimu, viongozi wa shule na wazazi hupata na kuchunguza matokeo ya tathmini iliyofanywa. Tathmini zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi zitamwelekeza mwalimu kubashiri matatizo yaliyopo kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kiwango cha kuwaelekeza wanafunzi kupata uwezo walio nao katika somo hili. Hivyo basi, tathmini zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi ni msingi wa mambo mengine ambayo mwanafunzi atayakuta katika miaka mingine ya masomo yake ya Kiswahili kwa shule za sekondari.

### 1.2.4. Mbinu na Mikakati ya Kuendeleza Ufundishaji na Ujifunzaji

Katika kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu achunguze mambo yafuatayo:

- Upekee wa somo,
- Kielelezo cha somo,
- Malengo maalum ya kutimiza,
- Kuchunguza idadi ya vipindi mahususi kwa madhumuni ya kutimiza malengo ya somo,
- Maelekezo muhimu kuhusu vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopatikana katika mazingira halisi,
- Jinsi wanafunzi watakavyokaa darasani,
- Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu,
- Uwezo na mtindo wa ujifunzaji.

### 1.2.5. Mbinu za Ufundishaji Zinazokuza Shughuli ya Ujifunzaji Shirikishi

Ili kufanikisha malengo ya somo lake, mwalimu azingatie njia zifuatazo:

- **Njia Shirikishi**: Njia shirikishi hutumia makundi ya wanafunzi ambapo mwalimu huwawezesha wanafunzi kushiriki katika kitendo cha ufundishaji na ujifunzaji. Kinachopaswa kufanywa hapa ni kuwapatia wanafunzi wote fursa ya kushiriki katika shughuli zinazopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi. Hali hii hutokana na mazingira yanayojengwa na mwalimu ambapo kila mwanafunzi ndiye ambaye huchukuliwa kama kiini cha ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo basi, wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya shughuli zote watakazoombwa na mwalimu kama vile majadiliano, midahalo na mazungumzo ya aina tofauti kama yalivyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi.
- **Njia ya kibinafsi:** Njia hii inahusu kazi binafsi za kila mwanafunzi ambapo atapewa kazi ama mazoezi yake binafsi ili aweze kufikia kiwango cha umilisi wa lugha kinachotarajiwa. Baada ya kufanya kazi na mazoezi hayo, ni vyema mwalimu akumbuke kuambatanisha njia aliyoitumia na njia shirikishi kwa kumwomba mwanafunzi achunguze maoni na hoja za wanafunzi wenzake katika makundi yao. Katika njia ya kibinafsi, mwalimu anaweza kuomba mwanafunzi kwa mfano kujisomea kifungu cha habari, kutambua maana za maneno mapya na kuyatumia katika sentensi zake, n.k.

- **Maswali na majibu**: Mara nyingi somo huchukua mwelekeo wa majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Kwa upande mwingine, wanafunzi wanaweza kumwuliza mwalimu wao naye akawajibu. Vilevile, maswali na majibu haya yanaweza kujitokeza kati ya wanafunzi wenyewe. Katika hali hii, mwalimu atawaelekeza wanafunzi wake kujitafutia majibu kwa maswali wanayouliza huku akiwapa maelekezo muhimu au mwongozo unaofaa kwa kusahihisha makosa wanayoyafanya.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwanafunzi hupewa muda wa kushiriki yeye binafsi katika somo. Katika njia hii, mwalimu atakuwa mwelekezi na shughuli yake muhimu itaegemea kuwaongoza wanafunzi kupata ufahamu na uelewa unaofaa. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

**SEHEMU II: SAMPULI ZA MAANDALIO YA MASOMO**

**ANDALIO LA SOMO**

**Jina la shule**: ....................................**Jina la Mwalimu: ....................................**

| **Muhula** | **Tarehe** | **Somo** | **Kidato** | **Mada** | **Idadi ya masomo** | **Muda** | **Idadi ya wanafunzi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | 28/2/2018 | Kiswahili | 5 | 1 | Masomo 6 | Dakika 80 | 42 |

| | |
|---|---|
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao.** | Hakuna |
| **Mada** | Uwanja wa fasihi kama sanaa |
| **Uwezo unaopatikana katika mada** | Kufafanua tanzu za Fasihi Simulizi katika Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuindeleza jamii au nchi yake; Kubainisha sentensi kulingana na aina zake. |
| **Somo lenyewe** | Maana ya fasihi ya Kiswahili |
| **Malengo ya ujifunzaji** | Mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi ataweza:<br>• Kuelewa na kuweza kueleza fasihi ya Kiswahili |
| **Mahali somo litakapofundishiwa** | Darasani |
| **Vifaa au zana kwa wanafunzi wote** | Kitabu cha mwanafunzi, kitabu cha mwalimu, ubao, chaki, madaftari, kalamu. |

| | |
|---|---|
| **Vitabu vya rejea** | Kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano, Mwongozo wa mwalimu kidfato cha tano. |

| **Muda na hatua** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** | | **Uwezo wa jumla na masuala mtambuka vielezwe+maelezo mafupi** |
|---|---|---|---|
| | **Kazi katika makundi:** Mara nyingi wanafunzi watafanyia kazi yao katika makundi kwa kushirikiana ili wafanikiwe na mambo kadhaa.<br>**Kazi ya kibinafsi:** Wanafunzi watapata muda mfupi wa kufanya kazi ya kipekee. | | |
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| **Utangulizi**<br>Dakika 5 | Mwalimu achangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu fasihi, na maswali mengine kuhusu mchoro unaotangulia kifungu cha habari. Mwalimu akiuliza, achague wanafunzi wa kujibu kwa kuchanganya wavulana na wasichana. | Wanafunzi watajibu maswali yote yaliyoulizwa na mwalimu. | **Uwezo wa jumla:** Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na mawasiliano katika lugha rasmi.<br>**Masuala mtambuka:** Usawa wa kijinsia. |
| **Somo lenyewe**<br>Dakika 62 | - Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi wanne wanne ya wavulana kwa wasichana. Baadaye, awape vitabu vya wanafunzi na awaombe kusoma kimya kifungu cha habari cha "Dhana ya fasihi na fasihi ya Kiswahili." Awaombe kutumia | - Wanafunzi wakae katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kusoma kifungu walichopewa kwa kutumia muda maalum. | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi.<br>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha.<br>Mawasiliano katika lugha rasmi.<br>Utafiti: Kwa kujibu maswali ndani ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | dakika kumi.<br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma tena kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu katika dakika kumi.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kutafuta maneno magumu katika kifungu cha habari katika dakika nyingine kumi na kutumia kamusi kuyafafanua.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kumwambia maneno ambayo wameshindwa kuyafafanua.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi mwongozo wa kusoma kifungu cha habari katika dakika kumi.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi muda wa kusoma kwa sauti kubwa hivi akiwasahihisha katika dakika kumi na mbili. | - Wanafunzi wasome tena kifungu cha habari na wajibu maswali ya ufahamu.<br><br>- Wanafunzi watafute maneno magumu na kuyaandika mahali fulani, kisha wayafafanue kwa kutumia kamusi.<br><br>- Wanafunzi wamwambie mwalimu maneno yanayowashinda na kujaribu kuyafafanua pamoja na mwalimu.<br>-Wanafunzi wasikilize kwa makini namna mwalimu anavyosoma na waige mwenendo na lafudhi nzuri.<br>- Wanafunzi wasome mmoja baada ya mwingine kwa kubadilisha makundi. | makundi, wanafunzi watafanya utafiti, watashirikiana kupata majibu, na kuchagua viongozi wa makundi hivi wakiwasiliana katika lugha rasmi.<br>**Masuala mtambuka:**<br>Usawa wa kijinsia: Wanafunzi wafanye kazi pamoja; wasichana na wavulana na wapewe fursa sawa.<br><br>Mafunzo kuhusu amani na maadili: Kwa kufanyia kazi katika makundi, wanafunzi wajadiliane hivi wakitoa na kupokea fikra tofauti kwa amani. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | - Mwalimu awaombe wanafunzi kujichagulia wasimamizi wa kuandika majibu ya maswali ya ufahamu kwenye ubao kundi kwa kundi. Mwalimu awaongoze wanafunzi ili majibu yanayofanana yasiandikwe mara mbili kwa kutumia muda vizuri. Dakika kumi na tano zitumiwe hapa. Mwalimu asahihishe majibu ya wanafunzi itakiwavyo. | - Wanafunzi waandike matokeo ya makundi yao yenye kujibu maswali ya ufahamu wa kifungu cha habari kundi baada ya kundi jingine, mvulana na msichana kimpango. Wamfuate mwalimu iwapo kuna majibu ambayo yanahitaji masahihisho yake. | |
| **Hitimisho** Dakika 13 | - Mwalimu awape wanafunzi maelezo muhimu kimuhtasari katika dakika tatu.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi maswali matano ya tathmini la somo. Awape dakika kumi za kuyafanya kazi hiyo. | - Wanafunzi wamfuate mwalimu vizuri katika kutoa maelezo.<br><br>- Wanafunzi wajibu maswali hayo kwenye karatasi na kumpa mwalimu karatasi hizo ili azisahihishe. | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi na stadi ya utatuzi wa matatizo: wanafunzi wafikirie kwa upana na kujibu maswali wenyewe. |
| **Tathmini ya mwalimu** | | | |

**ANDALIO LA SOMO**

**Jina la shule**: ...................................**Jina la Mwalimu: ...................................**

| **Muhula** | **Tarehe** | **Somo** | **Kidato** | **Mada** | **Idadi ya masomo** | **Muda** | **Idadi ya wanafunzi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | 1/10/2021 | Kiswahili | 5 | 2 | Masomo 6 | Dakika 80 | 42 |

| | |
|---|---|
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao.** | Hakuna |
| **Mada** | Uwanja wa fasihi kama sanaa |
| **Uwezo unaopatikana katika mada** | Kufafanua tanzu za Fasihi Simulizi katika Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuindeleza jamii au nchi yake; Kubainisha sentensi kulingana na aina zake. |
| **Somo lenyewe** | Tanzu za fasihi simulizi ya kiswahili na vipera vyake |
| **Malengo ya ujifunzaji** | Kwa kupitia somo hili, wanafunzi waweze:<br>- Kutambua, kufafanua kwa kina na kuzieleza tanzu mbalimbali za fasihi simulizi na makundi yake makuu yaani semi, masimulizi, ushairi na mazungumzo. |
| **Mahali somo litakapofundishiwa** | Darasani |
| **Vifaa au zana kwa wanafunzi wote** | Kitabu cha mwanafunzi, kitabu cha mwalimu, ubao, chaki, madaftari, kalamu, redio. |
| **Vitabu vya rejea** | Kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano, Mwongozo wa mwalimu kidato cha tano. |

| **Muda na hatua** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** | **Uwezo wa jumla na masuala mtambuka vielezwe+maelezo mafupi** |
|---|---|---|
| | **Kazi katika makundi:** Mara nyingi wanafunzi watafanyia kazi yao katika makundi kwa kushirikiana ili wafanikiwe na mambo kadhaa. | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **Kazi ya kibinafsi:** Wanafunzi watapata muda mfupi wa kufanya kazi ya kipekee. | | |
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| **Utangulizi**<br>Dakika 5 | Mwalimu achangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali mawili kuhusu somo lililopita, na maswali mengine kuhusu mchoro unaotangulia kifungu cha habari. Mwalimu akiuliza, achague wanafunzi wa kujibu kwa kuchanganya wavulana na wasichana. | Wanafunzi watajibu maswali yote yaliyoulizwa na mwalimu | **Uwezo wa jumla:** Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na mawasiliano katika lugha rasmi.<br>**Masuala mtambuka:** Usawa wa kijinsia. |
| **Somo lenyewe**<br>Dakika 62 | - Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi wanne wanne ya wavulana kwa wasichana. Baadaye, awape vitabu vya wanafunzi na awaombe kusoma kimya kifungu cha habari cha "***Vipera vya tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili***." Awaombe kutumia dakika kumi.<br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma tena kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu katika dakika kumi.<br>- Mwalimu awaombe | - Wanafunzi wakae katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kusoma kifungu walichopewa kwa kutumia muda maalum.<br>- Wanafunzi wasome tena kifungu cha habari na wajibu maswali ya ufahamu.<br>- Wanafunzi | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi.<br>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha.<br>Mawasiliano katika lugha rasmi.<br>Utafiti: Kwa kujibu maswali ndani ya makundi, wanafunzi watafanya utafiti, watashirikiana kupata majibu, na kuchagua viongozi wa makundi hivi wakiwasiliana katika lugha rasmi.<br>**Masuala** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wanafunzi kutafuta maneno magumu katika kifungu cha habari katika dakika nyingine kumi na kutumia kamusi kuyafafanua.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kumwambia maneno ambayo wameshindwa kuyafafanua.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi mwongozo wa kusoma kifungu cha habari katika dakika kumi.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi muda wa kusoma kwa sauti kubwa hivi akiwasahihisha katika dakika kumi na mbili.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kujichagulia wasimamizi wa kuandika majibu ya maswali ya ufahamu kwenye ubao kundi kwa kundi. Mwalimu awaongoze | watafute maneno magumu na kuyaandika mahali fulani, kisha wayafafanue kwa kutumia kamusi.<br><br>- Wanafunzi wamwambie mwalimu maneno yanayowashinda na kujaribu kuyafafanua pamoja na mwalimu.<br>-Wanafunzi wasikilize kwa makini namna mwalimu anavyosoma na waige mwenendo na lafudhi nzuri.<br>- Wanafunzi wasome mmoja baada ya mwingine kwa kubadilisha makundi.<br><br>- Wanafunzi waandike matokeo ya makundi yao yenye kujibu maswali ya ufahamu wa kifungu cha habari kundi baada ya kundi jingine, | **mtambuka:**<br>Usawa wa kijinsia: Wanafunzi wafanye kazi pamoja; wasichana na wavulana na wapewe fursa sawa.<br><br>Mafunzo kuhusu amani na maadili: Kwa kufanyia kazi katika makundi, wanafunzi wajadiliane hivi wakitoa na kupokea fikra tofauti kwa amani. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wanafunzi ili majibu yanayofanana yasiandikwe mara mbili kwa kutumia muda vizuri. Dakika kumi na tano zitumiwe hapa. Mwalimu asahihishe majibu ya wanafunzi itakiwavyo. | mvulana na msichana kimpango. Wamfuate mwalimu iwapo kuna majibu ambayo yanahitaji masahihisho yake. | |
| **Hitimisho** Dakika 13 | - Mwalimu awape wanafunzi maelezo muhimu kimuhtasari katika dakika tatu.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi maswali matano ya tathmini la somo. Awape dakika kumi za kuyafanya. | - Wanafunzi wamfuate mwalimu vizuri mwalimu katika kutoa maelezo.<br><br>- Wanafunzi wajibu maswali hayo kwenye karatasi na kumpa mwalimu karatasi hizo ili azisahihishe. | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi na stadi ya utatuzi wa matatizo: wanafunzi wafikirie kwa upana na kujibu maswali wenyewe. |
| **Tathmini ya mwalimu** | | | |

**ANDALIO LA SOMO**

**Jina la shule: ...................................Jina la Mwalimu: ....................................**

| Muhula | Tarehe | Somo | Kidato | Mada | Idadi ya masomo | Muda | Idadi ya wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **3** | **8/5/2021** | **Kiswahili** | **5** | **3** | **Masomo 3** | **Dakika 40** | **53** |

| | |
|---|---|
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao.** | 1: Mwenye ulemavu wa mkono<br>1: Mwenye ulemavu wa miguu |
| **Mada** | Utungaji wa barua rasmi, simu na matangazo |
| **Uwezo unaopatikana katika mada** | Kuandika barua rasmi, simu na matangazo; Kuchanganua sentensi katika Kiswahili. |
| **Somo lenyewe** | Barua rasmi |
| **Malengo ya ujifunzaji** | Kabla ya somo hili kumalizika, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa:<br>- Kusoma na kufahamu kifungu (barua)<br>- Kujibu maswali ya ufahamu<br>- Kutumia msamiati kuhusu kifungu (barua) |
| **Mahali somo litakapofundishiwa** | Darasani |
| **Vifaa au zana kwa** | Kitabu cha mwanafunzi, mwongozo wa mwalimu, ubao, chaki, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **wanafunzi wote** | madaftari, kalamu. | | |
| **Vitabu vya rejea** | Kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano, Mwongozo wa mwalimu kidato cha tano | | |
| **Muda na hatua** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** | | **Uwezo wa jumla na masuala mtambuka vielezwe+maelezo mafupi** |
| | Kazi katika makundi: Mara nyingi wanafunzi watafanyia kazi yao katika makundi kwa kushirikiana ili wafanikiwe katika mambo kadhaa.<br><br>Kazi ya kibinafsi: Wanafunzi watapata muda mfupi wa kufanya kazi ya kipekee. | | |
| | **Wajibu wa Mwalimu** | **Wajibu wa mwanafinzi** | |
| **Utangulizi**<br><br>**Dakika 5** | - Mwalimu awaamkie wanafunzi<br>- Mwalimu aulize maswali ya kuwachangamua wanafunzi.<br>- Mwalimu akiuliza, achague wanafunzi wa kujibu kwa kuchanganya wavulana na wasichana, wenye mahitaji maalumu na wasio nayo. | - Wanafunzi waiitikie maamkizi ya mwalimu.<br>- Wanafunzi watajibu maswali yote yatakayoulizwa na mwalimu | **Uwezo wa jumla:**<br>❖ **Tafakuri tunduizi.**<br>❖ **Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha.**<br>❖ **Mawasiliano katika lugha rasmi.**<br>❖ **Utafiti:** Kwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Somo lenyewe**<br><br>**Dakika 25** | - Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi watano watano ya wavulana kwa wasichana. Baadaye, awape vitabu vya wanafunzi na awaombe kusoma kwa sauti ndogo kifungu (barua) "***Barua rasmi au ya kikazi***".<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma tena kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kutafuta maneno magumu katika kifungu cha habari na kutumia kamusi kwa kuyafafanua.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kumwambia maneno ambayo | - Wanafunzi wakae katika makundi ya wanafunzi watano watano na kusoma kifungu watakachopewa kwa kutumia muda maalum.<br><br>- Wanafunzi wasome tena kifungu cha habari na wajibu maswali ya ufahamu.<br><br>- Wanafunzi watafute maneno magumu na kuyaandika mahali fulani, kisha wayafafanue kwa kutumia kamusi.<br><br>-Wanafunzi wamwambie | kujibu maswali katika makundi, wanafunzi watafanya utafiti, watashirikiana kupata majibu, na kuchagua viongozi wa makundi hivi wakiwasiliana katika lugha rasmi.<br><br>**Masuala mtambuka:**<br><br>- **Usawa wa kijinsia:** Wanafunzi wafanye kazi pamoja; wasichana na wavulana na wapewe fursa sawa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wameshindwa kuyafafanua.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi mwongozo wa kusoma kifungu cha habari.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi muda wa kusoma kwa sauti kubwa hivi akiwasahihisha.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kujichagulia wasimamizi wa kuandika majibu ya maswali ya ufahamu kwenye ubao kundi kwa kundi. Mwalimu awaongoze wanafunzi ili majibu yanayofanana yasiandikwe mara mbili kwa kutumia muda vizuri. Mwalimu asahihishe majibu ya | Mwalimu maneno yanayowashinda na kujaribu kuyafafanua pamoja na Mwalimu.<br><br>-Wanafunzi wasikilize kwa makini namna mwalimu anavyosoma na waige mwenendo na lafudhi nzuri.<br><br>- Wanafunzi wasome mmoja baada ya mwingine kwa kubadilisha makundi.<br><br>- Wanafunzi waandike matokeo ya makundi yao yenye kujibu maswali ya ufahamu wa kifungu cha habari kundi baada ya kundi jingine, mvulana na msichana | - **Mafunzo kuhusu amani na maadili:** Kwa kufanyia kazi katika makundi, wanafunzi wajadiliane hivi wakitoa na kupokea fikra tofauti kwa amani.<br><br>- **Mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji:** wanafunzi watakutana na mifano kuhusu suala hili.<br><br>- **Elimu jumuishi:** wanafunzi wote watapewa fursa katika somo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wanafunzi itakiwavyo. | kimpango. Wamfuate mwalimu iwapo kuna majibu ambayo yanahitaji masahihisho yake. | |
| **Hitimisho**<br><br>**Dakika 10** | - Mwalimu awape wanafunzi maswali matano ya tathmini la somo.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kazi waliyopewa. | - Wanafunzi wajibu maswali hayo kwenye karatasi na kumpa mwalimu karatasi hizo ili azisahihishe.<br><br>- Wanafunzi wasahihishe kazi waliyopewa. | |
| **Tathmini ya Mwalimu** | | | |

## SEHEMU YA III: UUNDAJI WA MADA

## MADA KUU YA 1: UWANJA WA FASIHI KAMA SANAA

## MADA NDOGO: NADHARIA YA FASIHI SIMULIZI KATIKA KISWAHILI

### 1.1 Uwezo upatikanao katika mada

- Kufafanua tanzu za Fasihi Simulizi katika Kiswahili na kuzitumia kama sanaa ya kuindeleza jamii au nchi yake;
- Kubainisha sentensi kulingana na aina zake.

### 1.2 Ujuzi wa awali

Katika kidato cha nne, wanafunzi walisoma masomo ambayo yanahusu fasihi kwa ujumla na fasihi simulizi. Masomo hayo yanapatikana katika sura ya 2 iitwayo "***Lugha katika Sanaa.***" Masomo hayo ni kama vile:

- Somo la 9: Dhima ya fasihi
- Somo la 11: Hadithi
- Somo la 12: Methali
- Somo la 13: Nahau

Vilevile wanafunzi hawa walipata ujuzi huu katika sura ya 3 iitwayo "***Uhakiki wa hadithi za masimulizi katika Kiswahili***" katika masomo yafuatayo:

- Somo la 16: Fani katika hadithi simulizi
- Somo la 17 : Maudhui katika hadithi simulizi
- Somo la 18 : Uhakiki wa hadithi simulizi

### 1.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake

#### 1.3.1. Kidokezo cha mada

Kwa kutangulia mada hii, mwalimu aulize maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua mada hii. Maswali hayo yanapaswa kuzingatia maudhui ya mada nzima. Hapa, mwalimu anaweza kuuliza maswali yafuatayo:

- Fasihi ni nini?

- Tanzu za fasihi ni zipi?
- Fasili fasihi simulizi.
- Taja tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake.

### 1.3.2. Maelekezo kuhusu kidokezo cha mada

- Mwalimu atoe mwongozo wa kutoa jibu kwa kila kazi
- Wanafunzi wanaweza kushindwa wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia kazi nyingine zilizotayarishwa au masomo ya mada nzima.

## 1.4. Orodha ya masomo

| | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | Tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake | **Maarifa na ufahamu:** Kuonesha tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake.<br><br>**Stadi :** Kutofautisha tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuheshimu maonyo kutoka tanzu za fasihi simulizi katika kuimarisha ustawi wa jamii. | 10 |
| 2 | Dhana ya hadithi simulizi | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya hadithi simulizi<br><br>**Stadi**: Kutunga hadithi simulizi.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: | 12 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Kuthamini kazi ya utungaji wa hadithi simulizi kama njia ya kurekebisha mwenendo. | |
| 3 | Dhana ya methali za Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya methali za Kiswahili<br><br>**Stadi**: Kutumia methali za Kiswahili na kuzihusisha na maisha ya kila siku katika jamii.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujenga busara inayopatikana katika methali. | 12 |
| 4 | Dhana ya nahau na misemo ya Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya nahau na misemo katika Kiswahili<br><br>**Stadi :** Kutumia nahau na misemo ya Kiswahili katika vifungu vya habari mbalimbali<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuimarisha thamani ya lugha kwa kutumia nahau na misemo | 14 |
| 5 | Dhana ya vitendawili vya Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja vitendawili mbalimbali vya kiswahili.<br><br>**Stadi**: Kutega na kutegua vitendawili mbalimbali katika Kiswahili.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** | 6 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Kukuza fikra na kutatua tatizo haraka. | |
| 6 | Dhana ya ushairi simulizi wa Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya ushairi simulizi wa Kiswahili katika fasihi simulizi na taratibu za utungaji.<br><br>**Stadi:** Kughani na kutunga mashairi.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuendeleza kipaji cha utungaji wa mashairi. | 14 |
| - | Sarufi: Aina za sentensi za Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha aina za sentensi za Kiswahili<br><br>**Stadi:** Kutunga na kuchambua sentensi mbalimbali kwa kuzingatia aina zake.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kujenga tabia ya kufanya mambo kwa mpango au mwelekeo unaopendekezwa. | - |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Vipindi vyote vya mada ya kwanza** | | | 72 |

Kila somo huwa na kazi za aina saba ambazo ni:

- Kazi zinazohusu kusoma na ufahamu
- Kazi zinazohusu msamiati
- Kazi za sarufi

- Kazi zinazohusu matumizi ya lugha
- Kazi za kusikiliza na kuzungumza
- Kazi za kuandika

**Tnbh:** Sarufi huja kila wakati ndani ya kila somo baada ya ufundishaji wa msamiati.

## SOMO LA 1: TANZU ZA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI NA VIPERA VYAKE

### i. Malengo ya ujifunzaji

Katika somo hili, mwanafunza ataweza:

- Kuonesha tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake,
- Kutofautisha tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama: Kitabu cha mwongozo wa mwalimu, kitabu cha mwanafunzi, vitabu vya fasihi, ubao, uhaki,redio,michoro ya watu wanaokaa wakizungumza, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu Kazi za ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wane, n.k. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaeleze wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**iv. Majibu**

***Kazi ya 1:(uk. 25)***

*Katika jozi, wanafunzi watazame michoro kwenye ukurasa husika kisha watoe maoni yao kuhusu michoro hiyo. Pendekezo la jibu:*

*Kuna picha inayoonyesha funiko la kitabu ambapo pameandikwa "Methali na Nahau." Kuna pia methali ya Kiswahili "Usiache mbachao kwa msala upitao." Picha nyingine inaonyesha wasichana wanaopiga densi.*

***Kazi ya 2: (uk.25)***

*Katika jozi wanafunzi wazungumzie maana ya kauli inayoonekana kwenye mchoro wa kwanza.*

***Maana ya kauli yenyewe***

*"Usiache mbachao kwa msala upitao." Maana yake ni usishtushwe na mambo mapya yenye mng'ao (au yanayomeremeta) wa muda mfupi bali chagua yale unayoyazoea yanayoweza kudumu.*

***Kazi ya 3: (uk.25)***

*Katika jozi wanafunzi watazame picha na wajadiliane kuhusu picha hiyo. Pendekezo la jibu:* Picha ya kwanza inahusu "methali" lakini picha ya pili inahusu utanzu wa "nyimbo".

***Kazi ya 4 (uk. 25)***

Katika makundi, wanafunzi watofautishe picha hizo mbili kutokana na tanzu za fasihi simulizi zinazoziwakilisha. Mmoja kati yao awasomee wengine matokeo ya kazi hiyo. Pendekezo la jibu:

Picha ya kwanza inahusu “methali” lakini picha ya pili inahusu utanzu wa “nyimbo”. Tanzu hizo ni za fasihi simulizi. (*Zote zimezungumziwa katika kifungu cha habari Vipera vya tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili*.)

**Kusoma na ufahamu: Vipera vya tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili**

***Kazi ya 5 (Uk.7)***

*Katika makundi, wanafunzi wasome kifungu cha habari kilichotolewa na kujibu maswali ya ufahamu. Yafuatayo ni mapendekezo ya majibu:*

1. Sifa bainifu tano za fasihi simulizi ya Kiswahili ni:

- Husambazwa kikalima;
- Huwa na hadhira mahususi iliyo hai;
- Huwasilishwa kwa wakati na mahali maalumu kama vile jioni baada ya kazi, katika sherehe na kadhalika;
- Huwa na mwanzo na mwisho maalumu wa kiada. Muundo wake ni rahisi kufuatika;
- Ni mali ya jamii kwani mtunzi hajulikani;
- Hubadilika kulingana na wakati hasa inapowasilishwa kupitia ufaraguzi;
- Huwa na wahusika wengi tofauti yaani wahusika wa aina mbalimbali. Msimulizi ndiye mhusika wa kati;
- Huwa na tanzu nyingi zenye vipera vingi;
- Hutungwa kila wakati na baadhi yake huzuka papo hapo;
- Hutumia sauti, mdomo na ishara za mwili. Kwa hiyo, si lazima fanani au hadhira wajue kusoma. Kiungo muhimu katika mapokezi ni masikio;
- Huhusu visa vya kubuni na vya kihistoria na huhifadhiwa akilini mwa wanajamii;
- Huwa na uzuri unaotegemea ubingwa wa fanani;
- Ni kongwe kwani ilianza tu lugha ilipoanza.

2. “Jambo linalobabaisha leo ni upungufu wa idadi ya watu wanaoendelea kujivunia ubunifu wa kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili.” Chanzo cha jambo hili ni:

- **Uvumbuzi wa maandishi**: Katika enzi za kale, fasihi simulizi ndiyo iliyokuwa sanaa ya pekee ya lugha. Kupitia fasihi hii, vizazi viliweza kurithi kazi mbalimbali za vizazi vingine. Walakini, wanajamii walizipoteza kazi nyingi kutokana na njia hiyo ya masimulizi. Uvumbuzi wa maandishi ndio uliorahisisha kuhifadhi mila na tamaduni zao. Vilevile, kazi mbalimbali za fasihi simulizi zilihifadhiwa.
- **Mfumo mpya wa elimu na maendeleo**: Awali, watoto walikuwa wakijumuika kwenye moto nyakati za jioni ili kusimuliwa hadithi au vitendawili. Siku hizi, wanajumuika kwenye kumbi na madarasa yanayoangaziwa kwa kutumia umeme. Wao wametekwa na vifaa vipya kama vile redio, runinga, vitabu na kadhalika. Mfumo huu mpya wa elimu hutilia pia mkazo masomo mengine huku fasihi simulizi ikipuuzwa. Elimu ya vitabu ndiyo inayoshughulikiwa mno kuliko ile ya mapokeo.
- **Mwingiliano na mgusano wa jamii mbalimbali**: Kule kuingiliana kwa jamii mbalimbali ulimwenguni kulipunguza uhalisia wa fasihi simulizi ya Kiswahili. Vinyume vya mwingiliano huo ni kama vile kutoweza kujieleza kwa lugha moja, kutoweza kujigamba mbele ya hadhira na kadhalika. Kumeibuka jamii ya Waswahili yenye utamaduni mseto na lugha iliyopunguziwa nguvu zake.

3. Mfumo wa elimu mpya na maendeleo huchangia katika kupunguka kwa idadi ya kazi za fasihi simulizi kwa namna hii:

Awali, watoto walikuwa wakijumuika kwenye moto nyakati za jioni ili kusimuliwa hadithi au vitendawili. Siku hizi, wanajumuika kwenye kumbi na madarasa yanayoangaziwa kwa kutumia umeme. Wao wametekwa na vifaa vipya kama vile redio, runinga, vitabu na kadhalika. Mfumo huu mpya wa elimu hutilia pia mkazo masomo mengine huku fasihi simulizi ikipuuzwa. Elimu ya vitabu ndiyo inayoshughulikiwa mno kuliko ile ya mapokeo.

4. Ili kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili ziendelee kutungwa:

- Ni lazima wanajamii wasisitizie utafiti wa tanzu na vipera vya fasihi simulizi hiyo;
- Ni vizuri jamii husika iunde mikakati thabiti ya kufundisha fasihi hiyo shuleni;
- Ni lazima jamii husika ihimize uhifadhi wa kazi za sanaa za fasihi hiyo;
- Ni lazima lugha ya Kiswahili itumiwe kwa ufasaha ili kupambana na lugha za kikoloni. Kwa hiyo, wanajamii wanatakiwa kutopuuza fasihi simulizi ya Kiswahili.

5. Utanzu wa fasihi simulizi ya Kiswahili unaoingia katika kundi la masimulizi ni hadithi. Vipera vya utanzu huu ni ngano, hekaya na hurafa.

Msamiati (uk. 29-30)

***Kazi ya 6:*** Soma sentensi zifuatazo na kuzikamilisha kama zilivyotumiwa katika kifungu cha habari:

Kigezo muhimu cha kuainisha fasihi ni namna msanii anavyoupitisha ujumbe wake yaani masimulizi ...........................................................................................huhusu visa vya kubuni na vya kihistoria na huhifadhiwa akilini mwa wanajamii.

3. Ni lazima lugha ya Kiswahili itumiwe kwa ufasaha ili ..................................... ......................

4. Ili mazungumzo yaitwe .........................................., ni lazima yawe na usanii wa aina fulani.

*Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujaza sentensi. Majibu yaliyopendekezwa ni haya yafuatayo:*

……………………. **ya mdomo au ya maandishi**.

**Fasihi simulizi ya Kiswahili** …………………

………………..**kupambana na lugha za kikoloni**.

….. **kazi ya fasihi** ………………………

***Kazi ya 7:*** Shirikiana na mwenzako na kutafuta katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu maana ya maneno yafuatayo yanayopatikana katika kifungu cha habari: Kigezo, Kalima, Kiada, Ufaraguzi, Fanani.

*Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutafuta maana za msamiati. Yafuatayo ni mapendekezo ya majibu:*

**Kigezo**: Mtu, kitu au jambo la kuigwa

**Kalima**: Tamko; kauli

**Kiada**: Kwa utaratibu wake; vizuri; vema

**Ufaraguzi**: Hali ya kutenda jambo bila kutarajiwa kufanywa.

**Fanani**: Msanii katika fasihi simulizi hasa anayesimulia hadithi, methali, vitendawili,... au anayecheza ngoma.

***Kazi ya 8:*** Shirikiana na mwenzako na kutafuta katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu maana ya maneno yafuatayo yanayopatikana katika kifungu cha habari: Kigezo, Kalima, Kiada, Ufaraguzi, Fanani.

*Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanaandika sentensi sahihi wakitumia maneno waliyopewa na awaelekeze panapohitajika.*

***Kazi ya 9:*** Tunga sentensi zinazohusu "kutunza na kulinda mazingira na maendeleo ya kudumu" kwa kutumia maneno yafuatayo yanayopatikana katika kifungu cha habari cha hapo juu: Mfumo....................................

Jamii……………………………………

Mbuzi……………………………

*Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kutunga sentensi na ahakikishe kwamba sentensi hizo zinaanza na maneno hayo. Hapa, kila mwanafunzi atatunga sentensi zake.*

**Sarufi: Aina za sentensi za Kiswahili (98-99)**

***Kazi ya 10:*** Hii ni mifano ya sentensi tofauti zilizotumiwa katika kifungu cha habari chetu. Soma sentensi hizo kwa makini ukizingatia aina zake.

- Ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya Kabeba.
- Ng'ombe hawa ni mali ya Bucyana.
- Mfalme aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea.

Linganisha mifano hiyo ya kwanza na sentensi hizi zifuatazo:

- Mimi ninaona ua.
- Kalisa amekanyaga mtoto.
- Mtoto anakuja hapa

  - *Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma sentensi na kuzilinganisha baadaye. Yafuatayo ni mapendekezo ya majibu:*

**Kulinganisha mifano ya sentensi tatu za kwanza na sentensi tatu zinazofuata:**

Kwa kuzingatia uainishaji wa sentensi kimuundo, aina za sentensi hizi ni:

- Ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya KABEBA. // Sentensi sahili.
- Ng'ombe hawa ni mali ya BUCYANA. // Sentensi sahili.

- MFALME aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea. //Sentensi changamano.

Kwa kuzingatia uainishaji wa sentensi kimaana, aina za sentensi hizi ni:

- Mimi ninaona ua. // Tungo tata.
- Kalisa amekanyaga mtoto. // Tungo tata.
- Mtoto anakuja hapa. // Tungo nyoofu/nyofu.

***Kazi ya 11:*** Shirikiana na mwenzako na kutafuta kwenye intaneti au katika vitabu aina za sentensi za Kiswahili. Msisahau kuwasomea wenzenu matokeo ya kazi yenu.

- ➢ *Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi, katika jozi, wamefanya utafiti kuhusu aina za sentensi na kuwasilisha matokeo ya utafiti wao baadaye.*

**Aina za sentensi kulingana na muundo ( Uainishaji wa sentensi kimuundo) ni:**

- Sentensi sahili
- Sentensi tegemezi
- Sentensi changamano
- Sentensi ambatano
- Sentensi shurutia

***Kazi ya 12:*** Katika jozi hiyo, kamilisheni sentensi hizi kwa istilahi inayotakiwa:

1. Sentensi isiyojitosheleza kimaana na kutegemea sentensi nyingine ili kuleta taarifa kamili huitwa sentensi..........................
2. Sentensi ambayo inajengwa na kitenzi kimoja na kujitosheleza kimaana huitwa sentensi..............................................
3. Sentensi ambazo huwa na virejeshi vyenye dhana za masharti ambayo yamejikita katika mofimu za -nge, -ngeli- na -ngali- huitwa sentensi.......................................

- ➢ *Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi ili wakamilishe sentensi. Majibu ni haya yafuatayo:*

1. ……….. **sentensi tegemezi**.
2. …………**sahili**.
3. …………. **shurutia**.

**Matumizi ya Lugha (uk. 31)**

***Kazi ya 13:*** Katika jozi, changanueni tanzu na vipera vifuatavyo kutokana na makundi mawili ya hapa chini:

| **Maneno** | **Fasihi simulizi** | **Fasihi andishi** |
|---|---|---|
| Maombolezo<br>Tamthilia<br>Ngano<br>Hekaya<br>Riwaya<br>Hurafa<br>Tanzia | 1. Fasihi simulizi ya Kiswahili | 2. Fasihi andishi ya Kiswahili |

- *Katika makundi ya wanafunzi wanne, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuchanganua tanzu na vipera vya fasihi simulizi na fasihi andishi.Majibu ni haya yafuatayo:*

| **Maneno** | **Fasihi simulizi** | **Fasihi andishi** |
|---|---|---|
| Maombolezo | Maombolezo | Tamthilia |
| Tamthilia | Ngano | Riwaya |
| Ngano | Hekaya | Tanzia |
| Hekaya | Hurafa | |
| Riwaya | | |
| Hurafa | | |
| Tanzia | | |

**Kusikiliza na kuzungumza (uk. 31)**

***Kazi ya 14: (☞Kitabu cha Mwanafunzi: Kazi ya 18)***

*Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi amepewa fursa ya kueleza wenzake umuhimu wa televisheni katika* kulitatua tatizo la uhaba wa kazi za fasihi simulizi. Majibu yaliyopendekezwa ni haya yafuatayo:

- Hii ni televisheni au runinga.
- Runinga huhabarisha watu;
- Huelimisha watu;
- Huburudisha watu;
- Runinga inaweza kutumiwa kwa kueneza fasihi simulizi;
- Runinga inaweza kutumiwa kwa kufundisha fasihi simulizi, n.k.

**Kuandika (uk. 33)**

***Kazi ya 15:*** Andikeni na kusomea wenzenu maelezo mafupi kuhusu kila utanzu wa fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake.

- ➢ *Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi amefanya kazi hii kwa kuandika insha akieleza utanzu wa fasihi simulizi na vipera vyake.*

## SOMO LA 2: DHANA YA HADITHI SIMULIZI

### i. Malengo ya ujifunzaji

Katika somo hili kila mwanafunzi ataweza:

- Kueleza dhana ya hadithi simulizi,
- Kutunga hadithi simulizi.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

- Kitabu cha mwanafunzi, kamusi ya Kiswahili sanifu,
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Ubao, chaki, kalamu na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne, nk.. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaeleze wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

### iv. Majibu

Majibu ya somo hili yanapatikana chini ya somo lenyewe katika 1.5.1. Maelekezo ya ziada kwa mwalimu.

## SOMO LA 3: DHANA YA METHALI ZA KISWAHILI

### i. Malengo ya ujifunzaji

Katika somo hili mwanafunzi ataweza:

- Kueleza dhana ya methali za Kiswahili,
- Kutumia methali za Kiswahili na kuzihusisha na maisha ya kila siku katika jamii.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

- Kitabu cha mwanafunzi, kamusi ya Kiswahili sanifu,
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu.
- Ubao, chaki, kalamu na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

### iv. Majibu

***Kazi ya 1: (Uk.49)***

*Katika makundi madogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutazama picha na kueleza wanachoona kwenye picha hizo.*

***Dokezo***

Kuna:

- Picha ya 1: Kanga (pameandikwa methali “Mapenzi ni kikohozi hayawezi kufichika”);
- Picha ya 2: Mzee mmoja ambaye anawafundisha watoto methali.

***Kazi ya 2: (Uk.49)***

*Katika makundi madogo, wanafunzi wajadiliande kuhusu picha na kujibu swali linalohusiana na picha hizo.*

***Dokezo:***

Picha zinahusu utanzu wa “methali.”

***Kazi ya 3: (Uk.49)***

*Katika makundi madogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma kifungu na kukihusisha na picha*

***Dokezo***

Picha zinahusu “methali”, jambo ambalo linazungumziwa katika habari.

**Kusoma na ufahamu: Methali hutajirisha lugha**

**Majibu ya maswali ya ufahamu *(uk.53)***

***Kazi ya 4:*** *Katika makundi madogo madogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujibu maswali ya ufahamu.*

***Majibu:***

1. Asili ya utamu wa methali ni lugha nyepesi inayopenya moja kwa moja katika mioyo ya wasikilizaji.

2. Dhima ya methali katika jamii ni:

    - Kuelimisha wanajamii kuhusu masuala mbalimbali yanayoikabili jamii yao.

    - Kuonya wanajamii yaani kuipa jamii maadili bora.

- Kukosoa jamii na kurekebisha mwenendo wake.
- Kuhamasisha wanajamii na kuwatia moyo.

3. “Kazi ya kutafsiri methali huwa ngumu kwa sababu watu hufikiri kuwa ni kazi inayofanywa neno kwa neno yaani “tafsiri sisisi”. Ukweli ni kwamba ni jambo la kumakinikia. Kwa mfano, mtu akisema “mtaka cha uvunguni, sharti ainame”. Kauli hii hutumiwa kwa kumhamasisha mtu afanye kazi ili apate faida. Kwa kuitafsiri neno kwa neno katika Kinyarwanda [ushaka ikiri munsi y’ameza, agomba kunama], inapoteza utamu wake. Ni lazima kutafuta methali ya Kinyarwanda yenye maana sawa na ile ili utamu wake ubakie. Methali ya Kinyarwanda yenye maana sawa na ile ni “ushaka inka aryama nka zo”.
4. “Wanafasihi wengi wanajua methali zote za Kiswahili”. Kauli hii haina ukweli kwa sababu hakuna mtu anayeweza kujidai kuwa anajua yote kuhusu methali.
5. Methali zote zilizotumiwa katika hadithi “Linalowezekana leo lisingoje kesho”.

- Chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako
- Ndege aamkaye asubuhi hula wadudu watamu
- Linalowezekana leo lisingoje kesho
- Wakati una mabawa
- Wakati titi la nyati hukamuliwa kwa mashaka
- Haraka haraka haina Baraka
- Ngoja ngoja huumiza matumbo
- Mchumia juani hulia kuvulini
- Maneno mengi hayavunji mfupa
- Kesho kesho nitafanya
- Mwoga hukimbilia wanawe
- Kitamu hutokea kwa mwenye nguvu

**Msamiati (uk.54)**

***Kazi ya 5:*** Kwa kutumia kamusi, jadiliana na mwenzako juu ya maana ya maneno yafuatayo: Kunata, Kupenya, Anasa, Kuganga, Maktaba.

- ➢ *Katika jozi, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wameeleza maana za maneno waliyopewa kisha watunge sentensi kwa kutumia maneno hayo. Yafuatayo ni mapendekezo ya majibu:*
- **Kunata**: Kushika mahali kwa nguvu kama vile inavyoshika gundi
- **Kupenya**: Kupitia kwenye tundu ndogo, ufa au mwanya finyu na kuingia ndani
- **Anasa**: Mambo au hali ya raha nyingi
- **Kuganga**: Kufanyia mgonjwa matibabu; kutengeneza kilichovunjika au kuharibika
- **Maktaba**: Mkusanyo wa vitabu vingi; nyumba ambamo watu huenda kujisomea au kuazima vitabu

**Sarufi (uk. *98-99)***

***Kazi ya 6 :*** Tunga wewe mwenyewe sentensi zinazohusu amani na maendeleo kwa kutumia maneno matano ya hapo juu.

- ➢ *Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ametunga sentensi kuhusu amani na mendeleo kwa kutumia maneno aliyopewa katika msamiati.*Sarufi: Aina za sentensi

***Kazi ya 7:*** Hii ni mifano ya sentensi tofauti zilizotumiwa katika kifungu cha habari chetu. Soma sentensi hizo kwa makini ukizingatia aina zake.

• Ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya Kabeba.

• Ng'ombe hawa ni mali ya Bucyana.

• Mfalme aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea. Linganisha mifano hiyo ya kwanza na sentensi hizi zifuatazo:

• Mimi ninaona ua.

• Kalisa amekanyaga mtoto.

• Mtoto anakuja hapa.

- ➢ *Kupitia makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma sentensi za mfano wa kwanza kwa makini na kuzilinganisha na nyingine za mfano wa pili. Majibu*

*yanajikita katika aina za sentensi kwa msingi wa muundo na aina za sentensi kwa msingi wa maana kama ifuatavyo:*

❖ *Kwa msingi wa muundo:*

- Ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya KABEBA. // Sentensi sahili
- Ng'ombe hawa ni mali ya BUCYANA. // Sentensi sahili
- MFALME aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea. // Sentensi changamano

❖ *Kwa msingi wa maana:*

- Mimi ninaona ua. // Tungo tata
- Kalisa amekanyaga mtoto. // Tungo tata
- Mtoto anakuja hapa. // Tungo nyoofu

***Kazi ya 8:*** Sentensi mbili (Mimi ninaona ua / Kalisa amekanyaga mtoto) zinaweza kuwa na maana mbili. Eleza vizuri.

➢ *Kupitia makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujibu swali la kazi hii.Majibu yaliyopendekezwa ni haya yafuatayo :*

**Mimi ninaona ua:**

- "Ua" yaani sehemu ya mmea inayochanua, aghalabu huwa ndiyo sehemu ya uzazi ya mmea;
- "Ua" yaani mzunguko au boma lililofanywa kwa miti, mabati, makuti,... aghalabu huwa nyuma ya nyumba

**Kalisa amekanyaga mtoto:**

- "Mtoto" yaani kiumbe kinachozaliwa na mtu;
- "Mtoto" yaani kisanduku kidogo kinachoingizwa katika kabati (mtoto wa meza).

Ni kusema kuwa tungo hizi zinatatanisha kutokana na maana yake.

***Kazi ya 9:*** "Sentensi nyoofu" na "sentensi tata" ni nini? Eleza na kutoa mifano.

- *Kupitia makundi mdogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujibu swali la kazi hii.*

***Dokezo:***

Kwa kawaida, sentensi huwa na maana moja tu na wazi. Sentensi hiyo huitwa "sentensi / tungo nyoofu."

**Mfano:** Mama analima shamba.

Lakini, sentensi inaweza kuwa na maana zaidi ya moja (maana zisipo wazi kabisa). Sentensi hii inaweza kueleweka hivi na vile na kila maana ikawa sahihi katika mazingira yake. Kutokana na utata huo, inaitwa "sentensi / tungo tata".

**Mifano:**

[Hakuna maua!] Mfano huu unaweza kuwa na maana ya "maua" kama "sehemu ya mmea inayochanua" au "hakuna faida". Huo ndio utata unaojitokeza.

**Matumizi ya lugha (uk. 55)**

***Kazi ya 10:*** Kwa njia ya mazungumzo, jaza jedwali lifuatalo kwa kutumia methali inayofaa kwa kila hali:

| **Hali** | **Methali** |
|---|---|
| Tabia ya kuombaomba vitu humfanya mwombaji kuwa mnyonge au duni. | …………………………………………. |
| Mkubwa wao akiondoka, walio chini yake hujiona kuwa huru na hufanya mambo wapendavyo | …………………………………………….. |
| Usiporekebisha kosa dogo tangu mwanzo, hatimaye utapata hasara kubwa. | ……………………………………………. |

- *Kupitia makundi madogomadogo, mwalimu awelekeze wanafunzi kwa kujaza jedwali. Majibu ni yafuatayo :*

| **Hali** | **Methali** |
|---|---|
| Tabia ya kuombaomba vitu humfanya mwombaji kuwa mnyonge au duni. | Ombaomba huleta unyonge. |
| Mkubwa wao akiondoka, walio chini yake hujiona kuwa huru na hufanya mambo wapendavyo | Paka akiondoka, panya hutawala. |
| Usiporekebisha kosa dogo tangu mwanzo, hatimaye utapata hasara kubwa. | Usipoziba ufa, utajenga ukuta. |

**Kusikiliza na kuzungumza (uk. 56)**

***Kazi ya 11:*** Kwa njia ya mazungumzo, waelezee wenzako jinsi utakavyofanya ili uweze kupevuka katika methali kama Kimezeo.

- *Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi atazungumzia wengine na kutoa maoni yake kuhusu jinsi atakavyofanya ili aweze kupevuka katika methali kama Kimezeo.*

**Kuandika**

***Kazi ya 12: (☞ Kitabu cha Mwanafunzi: Kazi ya 23: uk. 58)***

*Mwalimu amwelekeze kila mwanafunzi kwa kuandika methali zinazolingana na michoro na kuzitumia katika hadithi.*

***Methali:***

1. Dalili ya mvua ni mawingu.
2. Mchumia juani hulia kivulini.
3. Shukrani za punda ni mateke.
4. Ganda la muwa la jana, chungu kaona kivuno.

## SOMO LA 4 : DHANA YA NAHAU NA MISEMO YA KISWAHILI

### i. Malengo ya ujifunzaji

Kupitia somo hili mwanafunzi ataweza:

- Kueleza dhana ya nahau na misemo katika Kiswahili,
- Kutumia nahau na misemo ya Kiswahili katika vifungu vya habari mbalimbali.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

- Kitabu cha mwanafunzi, kamusi ya Kiswahili sanifu,
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu.
- Ubao, chaki, kalamu na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

### iv. Majibu

***Kazi ya 1: (Uk. 60)***

*Katika makundi madogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutazama picha na kueleza wanachoona kwenye picha hizo.*

**Dokezo:**

Picha inaonyesha kitabu ambacho ni “Kamusi ya misemo na Nahau.”

***Kazi ya 2: (Uk.60)***

*Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuwa kutofautisha nahau na misemo.*

**Dokezo:**

Wanafasihi husema kuwa “nahau” ni semi zinazodai kitenzi maalumu ndani yake ili ziwe na maana ilhali “misemo” ni semi zisizokuwa na au zisizohitaji vitenzi. Maana kamili ya “misemo” haihitaji kitenzi ili kueleweka ingawa inaweza kutumiwa pamoja na vitenzi.

***Kazi ya 3: (Uk. 60)***

*Katika makundi madogo madogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma kifungu na kukihusisha na na picha kwa njia ya majadiliano.*

**Dokezo**

Picha inaonyesha kitabu ambacho ni “Kamusi ya misemo na Nahau”. Na habari yetu inazungumza kuhusu nahau na misemo.

**Kusoma na ufahamu: Kutumia nahau na misemo ni kupevuka katika lugha**

***Kazi ya 4: (Uk.64)***

*Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujibu maswali ya ufahamu.*

***Majibu***

1. Kichwa cha habari ni “Tamaa mbele, mauti nyuma”. Hii ni methali. Maana yake ni kuwa “tamaa huangamiza”. Mtu akitamani sana kitu fulani, ni lazima ajihadhari kwani mwisho wake unaweza kuwa kifo. Mfano ni ule wa ajali iliyotokea na watu wengi wakatamani sana kuyateka mafuta ya bwerere. Walakini, mambo hayakuwa mema kwa sababu mtu mmoja kati yao alipowasha sigara, moto mkali ulizuka na wengi wao wakateketea kabisa. Ni kusema kuwa tamaa yao ya kuyachota mafuta ya mahonyo iliwaletea kifo”.

2. Wanafasihi husema kuwa “nahau” ni semi zinazodai kitenzi maalumu ndani yake ili ziwe na maana ilhali “misemo” ni semi zisizokuwa na au zisizohitaji vitenzi. Maana kamili ya “misemo” hayahitaji kitenzi ili kueleweka ingawa inaweza kutumiwa pamoja na vitenzi. Kwa mfano, “kupigwa kalamu”, “kumwaga unga”, “kugonga mwamba” ni nahau lakini “lila na fila”, “mdomo na pua”, hii ni misemo. Walakini, kutokana na tofauti hiyo ndogo, wanafasihi wengi hupendelea kutumia maneno hayo mawili pamoja yaani “nahau na misemo”.

a. Nahau na misemo ni semi zinazopunguza ukali wa maneno. Siku za leo, mataifa yote yanapigana na janga la ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI ambalo linaendelea kuangamiza watu wengi sana. UKIMWI si kama tetekuwanga au kifaduro kwani haina dawa. Kwa hiyo, ni lazima walewenye kiini au virusi vya ugonjwa huo watunzwe vizuri kama vile:

- kupatiwa dawa zinazowasaidia katika maisha yao na ambazo wanahitaji;
- kutofanyiwa ubaguzi wowote na kutotengwa na watu wengine;
- kutotumia kauli zinazoweza kuwafanya wadharauliwe na kadhalika.

Kuhusu kauli hizi, badala ya kusema kuwa “fulani aliweza kuvumilia” ingawa yuko katika hali mbaya ya kiafya kutokana na kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI, unaweza kusema kuwa “fulani anajikaza kisabuni”. Kama “amekufa”, unaweza kutumia tamko la “kuaga dunia”. Hii ni nahau na inaeleweka kuwa inapunguza ukali wa maneno ya kwanza.

3. Nahau na misemo:

- Anga ikavaa joho jeusi: Giza ikatawala
- Usiku ukashika hatamu: Usiku ukaongoza
- Baadhi yao walisikika wakitia chumvi: Kuongeza maelezo yenye kusifu jambo kupita kiasi
- Kakangu ya kujipatia jiko: Kuoa
- Wasiwasi wa mwasi ukanivaa: ukanitawala
- Lakini nilipiga moyo konde: Kuwa jasiri
- Wengi wao walikula mwande: Kukosa ulichotumainia
- Lakini nikagonga mwamba: Kutofanikiwa
- Kwa kweli, lila na fila havitangamani: Mema na mabaya
- Niliponea katika tundu la sindano: Kuponea kwa bahati
- Maneno tamaa, pupa na papara niliyazika katika kaburi la sahau: Kutupilia mbali jambo ili kulisahau kabisa

4. Methali zote zilizotumika katika matini “Tamaa mbele mauti nyuma”:

- Mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo: kama kuna dalili za jambo Fulani, ni kusema kwamba bila shaka litatendeka
- Fumbo hufumbiwa mjinga mwerevu akatambua: Unapomwambia kitu mtu mpumbavu hawezi kutambua haraka unalolizungumzia. Lakini mwerevu anatambua upesi.
- Aliye kando haangukiwi na mti: Asiyehusika na jambo, madhara yake hayawezi kumfikia.
- Tamaa mbele, mauti nyuma: Vinyume vya hamu kubwa ya kupata kitu ni kifo. Usitamani sana kitu ili usije ukafikiwa na janga kubwa.

**Msamiati (uk. 65-66)**

***Kazi ya 5 :*** Katika jozi, tumieni Kamusi ya Kiswahili Sanifu na kuchunguza maana ya maneno yafuatayo: Darubini, Majungu, Kuzagaa, Kushamiri, Umbu, Kochokocho, Kugwengwenya, Kutuama, Libasi, Jakamoyo, Ushamba, Bwege, Bwerere, Dafrau.

➢ *Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutafuta maana za maneno waliyopewa. Majibu haya yamependekezwa :*

- **Darubini:** Chombo chenye lensi kinachofanya vitu vilivyo mbali vionekane karibu na vidogo vionekane vikubwa.
- **Majungu:** Vyungu vikubwa (Chungu ni chombo kilichofinyangwa kwa udongo na kitumiwacho kwa kupikia).
- **Kuzagaa:** Kuwa kila mahali; kuenea kila mahali.
- **Kushamiri:** Kuenea kwa jambo au habari; kuzagaa; kutapakaa.
- **Umbu:** Jina wanaloitana ndugu wazawa wa kike na wa kiume.
- **Kochokocho:** Kwa wingi; tele.
- **Kugwengwenya:** Kubandua kwa meno kama vile nyama kwenye mfupa; kuguguna.
- **Kutuama:** Kushuka kutoka mahali fulani na kwenda kulala chini.
- **Libasi:** Mavazi au nguo.
- **Jakamoyo:** Masumbufu ya rohoni; kero la moyo.
- **Ushamba:** Tabia za kijinga zinazofikiriwa kuwa ni za mtu anayeishi mbali na miji yaani katika vitongoji vya mbali.

- **Bwege:** Mtu mjinga au mpumbavu.
- **Bwerere:** Kitu cha bure au cha mahonyo.
- **Dafrau:** Mgongano wa nguvu baina ya vitu viwili au zaidi (Kupigwa dafrau=Kugongwa na).

***Kazi ya 6:*** Katika jozi hiyo, tungeni sentensi kwa kila neno kati ya hayo ya hapa juu.

- *Katika jozi, mwalimu ahakikishe kuwa kila kundi limetunga sentensi zake kwa kutumia maneno waliyopewa.*

***Kazi ya 7: (☞Kitabu cha Mwanafunzi : Kazi ya 12 : Uk.66)***

*Kupitia makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutazama picha/ michoro na kutafuta nahau inayolingana na kila picha/ mchoro.*

**Majibu:**

1. Kupiga mbizi
2. Kupiga mwayo
3. Kupiga mluzi
4. Kupiga darubini

**Sarufi : Aina za sentensi za Kiswahili**

***Kazi ya 8:*** *Katika makundi yao wanafunzi wasome tena maelezo juu ya tungo nyoofu na tungo tata kisha wataje aina za sentensi zifuatazo kulingana na maana.*

a. Simba amekuja.

b. Aje Jumapili.

c. Kalisa alienda sokoni jana.

d. Niliona vifaru.

e. Alimnunulia kanzu nzuri mtoto wake.

**Dokezo**

a. Sentensi tata : ina maana mbili (Simba anaweza kuwa mnyama au mtu anayeitwa Simba).

b. Sentensi tata : ina maana mbili (Mtu fulani aje kwenye siku ya Jumapili au Mtu anayeitwa Jumapili aje).

c. Sentensi nyoofu : ina maana moja.

d. Sentensi tata : ina maana mbili (Vifaru wanaweza kuwa wanyama au magari ya kijeshi.)

e. Sentensi nyoofu : ina maana moja.

**Matumizi ya lugha (uk. 68)**

***Kazi ya 9 :*** Panga kauli zifuatazo katika makundi yake haya:

| | | |
|---|---|---|
| Cheche huzaa moto<br><br>Alimpiga pambaja mwandani<br><br>Uchungu wa mwana aujuaye mzazi<br><br>Usimpe nyama ya ulimi<br><br>Kaza kamba ndugu!<br><br>Yote yang'aayo si dhahabu | Nahau | Methali |

- *Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kupanga kauli katika makund husikai. Yafuatayo ni majibu :*

| **Kauli** | **Nahau** | **Methali** |
|---|---|---|
| - Cheche huzaa moto<br>- Alimpiga pambaja mwandani<br>- Uchungu wa mwana aujuaye mzazi<br>- Usimpe nyama ya ulimi<br>- Kaza kamba ndugu!<br>- Yote yang'aayo si | - Alimpiga pambaja mwandani<br>- Usimpe nyama ya ulimi.<br>- Kaza kamba ndugu! | - Cheche huzaa moto.<br>- Uchungu wa mwana aujuaye mzazi.<br>- Yote yang'aayi si dhahabu. |

| | | |
|---|---|---|
| dhahabu | | |

**Kusikiliza na kuzungumza (uk. 69)**

***Kazi ya 10 :*** Shirikiana na mwenzako mtafute kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu au kwa majirani zenu nahau mbalimbali za Kinyarwanda na maana zake na kuzitafsiri katika Kiswahili. Msisahau kuwasomea wenzenu matokeo ya kazi yenu.

- *Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutafuta nahau za Kinyarwanda na kuzitafsiri kwa Kiswahi kisha wawasilishe.*

**Kuandika (uk. 70)**

***Kazi ya 11 :*** Katika jozi, tungeni aya moja ambamo mtatumia nahau tano tofauti na zile mlizorudia darasani.

- *Kwa kazi hii, kila mwanafunzi atatunga hadithi yenye matumizi ya nahau na misemo tofauti. Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi ametunga hadithi.*

## SOMO LA 5: DHANA YA VITENDAWILI VYA KISWAHILI

### i. Malengo ya ujifunzaji

Katika somo hili, mwanafunzi ataweza:

- Kutaja vitendawili mbalimbali vya kiswahili,
- Kutega na kutegua vitendawili mbalimbali katika Kiswahili.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

- Kitabu cha mwanafunzi, kamusi ya Kiswahili sanifu,
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu.
- Ubao, chaki, kalamu na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo. Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

iv. **Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.71)***

*Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutazama picha na kutaja vitu vinavyoonekana kwenye picha yenyewe.*

**Dokezo :**

Kinachoonekana kwenye picha:

- Mume na mke pamoja na watoto watatu. Wanatega na kutegua vitendawili.

***Kazi ya 2: (uk.71)***

*Katika makundi madogmadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma kifungu cha habari na kukihusisha na picha.*

**Dokezo**

Picha inaonyesha mume na mke wanaokaa pamoja na watoto watatu wakitega na kutegua vitendawili. Kifungu cha habari nacho kinazungumzia kuhusu vitendawili.

**Kusoma na ufahamu: Vitendawili hukuza uwezo wa kufikiri**

***Kazi ya 3: (uk.74)***

*Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujibu maswali ya ufahamu.*

**Majibu**

1. Vitendawili hukuza uwezo wa kufikiria na kukumbuka kwa sababu kutegua kitendawili huhitaji kukumbuka kitendawili ambacho kimetolewa, kufikiri kuhusu mazingira yake na kujaribu kupata jibu. Katika shughuli hii, mteguaji huwaza sana kuhusu mazingira hayo na kulinganisha majibu mbalimbali yanayoweza kutolewa. Hii ni namna moja ya kukuza uwezo wake wa kukumbuka na kufikiria.

2. Vitendawili hutegwa kwa njia ya uchangamfu na ushindani kwa sababu vitendawili huzingatia mfumo wa kutega (yaani kuuliza swali) na kutegua (au kujibu swali). Mtegaji na mteguaji hutii utaratibu ufuatao:

   Mtegaji: Kitendawili!

   Mteguaji: Tega!

   Mtegaji: (Anatoa kitendawili chake yaani "kutega kitendawili").

   Mfano: Nimeanika mpunga wangu juani lakini kulipopambazuka sikuuona

   Mteguaji: (Anatoa jibu yaani "kutegua kitendawili").

   Jibu: Nyota

   Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huitisha apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. Anapopewa anachotaka ndipo anakubali kutoa jibu. Hapa, inaonekana wazi kwamba vitendawili hutegwa kwa njia ya kufurahisha yaani uchangamfu na njia ya kupima ujuzi na uwezo wa kufikiri wa mtu yaani ushindani.

3. Kuna tofauti kati ya vitendawili na mafumbo kuhusu namna michezo hiyo inavyochezwa.

   Kitendawili ni tungo fupi ambayo huwa na swali wazi yaani swali linaloulizwa kwa kutumia lugha ya mafumbo. Mafumbo hayo ndiyo yanayoufanya utanzu huu uwe wa sanaa ya hali ya juu.

   Majibu hutolewa kwa makusudi ya kupima ufahamu wa hadhira kuhusu mazingira yake. Kujibu kunahitaji ujuzi mkubwa kulingana na tamaduni za mazingira ya jamii husika. Mtu hujibu kiufundi kwa kuzingatia utaratibu wa kuvutia.

   Mtegaji na mteguaji hutii utaratibu ufuatao:

   Mtegaji: Kitendawili!

   Mteguaji: Tega!

   Mtegaji: (Anatoa kitendawili chake yaani "kutega kitendawili").

   Mfano: Nimeanika mpunga wangu juani lakini kulipopambazuka sikuuona

   Mteguaji: (Anatoa jibu yaani "kutegua kitendawili").

   Jibu: Nyota

   Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huitisha apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. Anapopewa anachotaka ndipo anakubali kutoa jibu.

   Kuna kipengele kingine cha fasihi simulizi kinachofanana kwa kiasi na vitendawili lakini chenye utaratibu wake wa kipekee. Kipengele hicho ni "mafumbo". Mafumbo ni kauli

zinazoeleza jambo kwa njia fiche yaani isiyo wazi. Msimulizi anatoa fumbo lake na kazi ya wasikilizaji ni kulifumbua.

Katika mchezo huu wa ushindani wa mafumbo, msimulizi anasema “Fumbo mfumbie mjinga”. Msikilizaji anajibu “Mwerevu hiling’amua” na kufumbua jambo linalozungumziwa.

Mifano ya mafumbo na ufumbuzi wake:

Mimi na ndugu yangu tulinunua fahali mmoja kutoka sokoni. Baada ya mwaka mmoja alijifungua ndama wawili. Je, kila mtu alipata wangapi? / [Ufumbuzi: Fahali hajifungui].

4. Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huitisha apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. Anapopewa anachotaka ndipo anakubali kutoa jibu.
5. Vitendawili:
   - Huburudisha watu;
   - Huunganisha jamii;
   - Huhamasisha watu kuhusu mazingira yao;
   - Hukuza uwezo wa kufikiria na kukumbuka;
   - Hukuza na kuhifadhi amali na tamaduni za jamii;
   - Vilitumika kwa muda mrefu kupitisha wakati na kuwafanya watoto wasilale mapema kabla ya chakula kuwa tayari.
6. Hapana. Vitendawili ni kipengele cha semi.

**Msamiati (75-76)**

***Kazi ya 4:*** Katika jozi, tumieni Kamusi ya Kiswahili Sanifu na kuchunguza maana za maneno yafuatayo: Kizibao, Dema, Chane, Popoo.

- *Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutafuta maana za maneno ya hapa juu.Yafuatayo ni majibu:*

- **Kizibao:** Vazi kama koti fupi lisilo na mikono
- **Dema:** Mtego wa samaki uliofumwa kwa matete au vijiti
- **Chane:** Shada moja la mkungu wa ndizi (kundi dogo la ndizi zinazojifungia kwenye fundo moja)
- **Popoo:** Tunda gumu lenye umbo la duara lililofunikwa na makumbi kama vile nazi, ambalo hukatwa vipande vyembamba na kutafunwa pamoja na tambuu.

***Kazi ya 5:*** Katika jozi hiyo, tungeni sentensi kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

- *Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutunga sentensi wakitumia maneno waliyopewa.*

***Mifano:***

- Mwanamke yule amevaa kizibao.
- Mvuvi alivua samaki kwa kutumia dema.
- Nilinunua chane moja kwa faranga mia tano.
- Nyani hupenda kula popoo.

**Sarufi: Aina za sentensi za Kiswahili**

***Kazi ya 6*** *: Katika makundi yao, wanafunzi wasome tena maelezo juu aina za sentensi kisha wabainishe vifupisho vinavyosimamia kila sentensi na kila aina ya neno.*

- **Vifupisho vya sentensi**

- S/T : Sentensi/Tungo
- SS/TS : sentensi sahili/ Tungo sahili
- ST/TT : Sentensi tegemezi/ Tungo tegemezi
- SCH/TCH: Sentensi changamano/ Tungo changamano
- SA/TA : Sentensi ambatano/ Tungo ambatano
- SSH/TSH : Sentensi shurutia/Tungo shurutia

**Vifupisho vya maneno**

- Kitenzi (T) kinachoweza kuwa “kitenzi kikuu” (T) au “kitenzi kisaidizi” (TS) au “kitenzi kishirikishi” (t)
- Nomino (N)
- Kivumishi (V)
- Kiwakilishi (W)
- Kielezi (E)
- Kiunganishi (U)
- Kihisishi (H)

- Kihusishi (HU)

***Kazi ya 7**: Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kufanya zoezi la kuonyesha aina za sentensi na vipashio vyake kwa kutumia vifupisho.*

*a. Baba alikuwa akipanda miti msituni.*
*b. Yeye angali mwanajeshi.*
*c. Wanafunzi wanalala katika bweni zuri lakini wao wapigi deki.*
*d. Alipoingia msituni alikutana na tembo.*
*e. Yeye angejua kwamba mvua ingenyesha leo angeleta mwavuli.*

***Majibu***

*a. Baba alikuwa akipanda miti msituni.(SS)*
*N TS T N E*

*b. Yeye angali mwanajeshi.(SS)*
*W t N*

*c. Wanafunzi wanalala katika bweni zuri lakini wao hawapigi deki.(SA)*
*N T HU N V U W T N*

*d. <u>Alipoingia msituni</u> alikutana na tembo.(SCH)*
*(ST)*
*T E T U N*

*e. Yeye angejua kwamba mvua ingenyesha leo angeleta mwavuli.(SSH)*
*W T U N T E T N*

**Matumizi ya lugha (uk. 78)**

***Kazi ya 8:*** Jiunge na wenzako wawili na kujadili dhima ya mafumbo katika kufundisha lugha. Msisahau kuwasomea wanafunzi wengine matunda ya kazi yenu.

- *Katika makundi madogomadogo wanafunzi wajadiliane kuhusu dhima ya mafumbo katika kufundisha lugha.*

**Mifano ya majibu**:

- Huburudisha watu.
- Huunganisha jamii.
- Husaidia watu kwa kufikiri.

**Kusikiliza na kuzungumza (uk: 81)**

***Kazi ya 9:*** Katika kundi la wanafunzi wanne, tafuteni kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu au ulizeni majirani zenu vitendawili ishirini (20) vya Kiswahili na majibu yake.

- ➢ *Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutafuta mtandaoni vitendawili ishirini na kuwasomea wenzao.Watoe majibu ya vitendawili hivyo.*

## Kuandika

***Kazi ya 10****: Kila mwanafunzi atatunga kifungu kinachoonyesha umuhimu wa witendawili kwa jamii ya Wanyarwanda.*

*Baadhi ya hoja (chunguza umuhimu wa vitendawili)*

## SOMO LA 6: DHANA YA USHAIRI SIMULIZI WA KISWAHILI

i. **Malengo ya ujifunzaji**

Katika somo hili, mwanafunzi ataweza:

- Kueleza dhana ya ushairi simulizi wa Kiswahili katika fasihi simulizi na taratibu za utungaji
- Kughani na kutunga mashairi.

ii. **Zana au vifaa vya ufundishaji**

- Kitabu cha mwanafunzi, kamusi ya Kiswahili sanifu,
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu.
- Ubao, chaki, kalamu na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

iii. **Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

iv. **Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.83)***

*Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuchunguza michoro.*

**Dokezo**:

- Kuna watoto wanaokaa chini kwa duara, mke mwenye mtoto mgongoni anayesimama kando na mume mwenye fimbo anayecheza. Labda mume huyu anajigamba.

***Kazi ya 2: (uk.81)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekezi wanafunzi kwa kusoma kifungu na kukihusisha na michoro.*

☞Picha inahusu "mashairi" na habari yenyewe inazungumzia kuhusu "mashairi."

**Kusoma na ufahamu: Ushairi simulizi wa Kiswahili**

***Kazi ya 3: (uk.86)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma kifungu upya na kujibu maswali ya ufahamu.*

**Majibu**

1. Shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalumu wa lugha ya mkato katika usemi, maandishi au wimbo. Mtungo huo unaeleza wazo au mawazo, hisi au tukio juu ya maisha. Hufuata utaratibu wa urari na muwala maalumu unaoheshimu na kuzingatia kanuni za utunzi wa shairi unaohusika. Muundo maalumu ndio unaoletea shairi utamu unaotakiwa.

   Ushairi ni kazi au namna ya kutunga mashairi na kipengele chenyewe kinachoundwa na mashairi.
2. Mashairi ya Kiswahili ya mwanzoni (kabla ya karne ya pili BK) hayakuwa na utaratibu wa vina, mizani na beti kama ilivyo katika mashairi ya kisasa. Mashairi ya siku hizo yalifanana sana na nyimbo kwani ndizo zilizokuwa chimbuko lake.

3. Kutokana na kazi alizokuwa akifanya, binadamu alianza kutunga maneno na sauti za muziki zilizokuwa zikifuata mapigo ya kazi. Wimbo wa kazi ukawa ndio utanzu wa fasihi wa mwanzo. Polepole, ushairi wa Kiswahili ulianzishwa kwa kuiga mapigo ya nyimbo.
4. Mabadiliko mengi ya kimaudhui yalifanyika wakati wa majilio ya Waarabu sehemu za pwani ya Afrika ya Mashariki.

5. Mashairi ya Waarabu yalikuwa na beti, mizani, vina na maudhui ya kidini.

**Msamiati (uk: 88)**

***Kazi ya 4:*** Katika pea, tumieni Kamusi ya Kiswahili Sanifu na kuchunguza maana ya maneno yafuatayo: Muwala, Ustaarabu, Sime.

- *Kazi hii ifanyike katika jozi/pea. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutoa maana za maneno. Mapendekezo ya majibu ni haya yafuatayo:*

- **Muwala**: Uwiano wa vipengele vya kisanaa na maudhui katika ushairi
- **Ustaarabu**: Hali ya kustaarabika au kuwa na vitendo, tabia na mwenendo unaolingana na maadili ya jamii inayohusika
- **Sime**: Kisu kikubwa chenye makali pande zote mbili

***Kazi ya 5 :*** Tunga sentensi moja kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno waliyopewa.*

**Sarufi**

***Kazi ya 6****: Kazi hii ifanyike kwa makundi. Wanafunzi wapewe kazi inayohusiana na kuonyesha aina za maneno katika sentensi hizi.*

1. Mtoto wa tajiri akilia hupewa picha ya kuchezea.
2. Akilia mtoto wa tajiri huletewa kigari akapanda.
3. Mvua ilinyesha jana ikasababisha mafuliko nchini.
4. Licha ya nyimbo na vitendawili, mashairi ni nyenzo kuu za burudani katika jamii.
5. Mashairi ya kuomboleza au maombolezo ni yale yanayozungumzia msiba au wakati wa huzuni.

**Majibu ya kazi hii:**

1. Mtoto wa tajiri akilia hupewa picha ya kuchezea.

N V N T T N V T

2. Akilia mtoto wa tajiri huletewa kigari akapanda.

   T N V N T N T

3. Mvua ilinyesha jana ikasababisha mafuliko makali nchini.

   N T E T N V E

4. Licha ya nyimbo na vitendawili, mashairi ni nyenzo kuu za burudani katika jamii.

   HU N U N N t N V V N HU N

5. Mashairi ya kuomboleza au maombolezo ni yale yanayozungumzia msiba au wakati wa

   N V T U N t W T N U N V

   huzuni.

   N

**Matumizi ya lugha (uk: 89)**

***Kazi ya 7:*** Jiunge na wenzako watatu, mjadili istilahi zinazotumiwa katika ushairi wa Kiswahili. Msisahau kuwasomea wanafunzi wengine matunda ya kazi yenu.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujadiliana kuhusu istilahi zinazotumiwa katika ushairi.*

**Kusikiliza na kuzungumza (uk: 90)**

***Kazi ya 8:*** Jiunge na wenzako wawili na kujadili kwa njia ya mdahalo "athari za ushairi simulizi wa Kinyarwanda katika maendeleo ya jamii ya Wanyarwanda."

- *Kazi hii ifanyike kwa makundi madogo au jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika majadiliano yao.* Kila kundi litatoa maoni yake.

**Kuandika (uk: 91)**

***Kazi ya 9:*** Tunga shairi moja lenye beti tano kuhusu "Maendeleo". Jaribu kulikariri na kulisimulia wenzako darasani.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ametunga shairi na kulikariri kisha awasilishe.*

## 1.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

### 1.5.1. Maelezo ya ziada kwa mwanafunzi

## SOMO LA 2: DHANA YA HADITHI SIMULIZI

### 2.1. Kusoma na Ufahamu: KABEBA

***Kazi ya 1:*** *Katika jozi, someni hadithi hii ya "Kabeba", kisha mjibu maswali umliyopewa katika sehemu ya ufahamu.*

KABEBA

Hapo zamani paliishi Mfalme na Kabeba, Mheshimiwa Panya. Siku moja ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya Kabeba. Jambo hili lilitokana na kuwa katika enzi hizo, watu walikuwa hawajaunda mikakati thabiti ya kutunza vizuri mazingira kwa kuwachungia ng'ombe zizini. Wachungaji walijitahidi kuwatafuta ng'ombe hao lakini hawakuwaona. Wapita njia waliwapa habari kwamba ng'ombe hao walikuwa wameyavamia na kuyaharibu mashamba ya Kabeba. Kufuatana na jambo hilo, Mheshimiwa Panya alikuwa amewafungia nyumbani kwake. Alikuwa na nia ya kuwauza ili kuboresha kazi zake za uzalishajimali.

Wachungaji waliposikia habari hiyo, waliamua kwenda moja kwa moja hadi nyumbani kwa Kabeba. Walipofika huko, walimsalimu wakisema, "Heri kwenu enyi mnaoishi kuliko na ng'ombe wanaojichunga na kujirudisha wenyewe zizini". Panya akajibu, "Naam! Ni kweli kuwa ng'ombe hawa wanajichunga na kujirudisha wenyewe zizini lakini siyo bila sababu. Ng'ombe hawa wanatoka kwa Bucyana. Mheshimiwa huyu ni:

a) Bwana Mwenda-mbio na Mwenda-pole-na-taratibu;
b) Bwana Mkubwa wa juu mbinguni ambaye anaweza kuwakata, bila kusita, vidole vyenu vidogo ambavyo vingetawanyika ardhini;
c) Bwana ambaye angewapakulia ugali ambao kila anayekula kufumba na kufumbua ungemnenepesha".

Wachungaji waliposikia hivyo, walighairi na kukimbia bila kuangalia nyuma.

Kisa hiki cha ng’ombe hakikukawia kumfikia Mfalme. Mfalme aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea. Alipofika huko, alimwamkia kama kawaida, “Heri kwenu enyi mnaoishi kuliko na ng’ombe wanaojichunga na kujirudisha wenyewe zizini”. Mheshimiwa Panya akajibu, “Ng’ombe hawa wanajichunga na kujirudisha wenyewe zizini kwa sababu maalum. Ng’ombe hawa ni mali ya Bucyana. Huyu ni:

a) Mwenda-shoti na Mwenda-pole-na-taratibu;
b) Bwana Mkubwa wa huko juu ambaye anaweza kukukata kidole chako kidogo na kukiangusha chini ardhini;
c) Bwana ambaye hupika ugali ambao kila aulaye, kufumba na kufumbua, humnenepesha”.

Mfalme kusikia hivyo, alikimbia bila kuangalia nyuma.

Bwana Mbwa aliposikia yaliyotokea alimwambia Mheshimiwa Mfalme, “Ewe Mfalme wetu, endapo utaniahidi kunichinjia fahali mdogo kati ya ng’ombe hao waliochukuliwa. Mimi binafsi nitafanya jitihada ya kuwarudisha ng’ombe wako”. Mfalme akakubali na Bwana Mbwa akaondoka mara moja na kwenda nyumbani kwa Kabeba. Alipofika huko, alimwamkia kama walivyokuwa wamefanya wengine, “Heri kwenu mnaoishi pamoja na ng’ombe wanaojichunga na kujirudisha wenyewe zizini”. Bwana Panya akamjibu kama alivyokuwa amewajibu wengine. Lakini, badala ya Bwana Mbwa kuogopa na kwenda zake, akafanya hatua moja mbele. Panya kuona vile, aliruka na kuingia ndani ya nyumba yake.

Mbwa alimwamkia tena, “Heri kwenu mnaoishi pamoja na ng’ombe wanaojichunga na kujirudisha wenyewe zizini”. Panya alirudia maneno yale ya kujigamba. Mbwa aliendelea kupiga hatua mbele. Panya naye aliruka na kuingia ndani ya nyumba. Mbwa alipomwamkia mara ya tatu, kimya kilitawala. Basi ndipo Mbwa aliichukua fimbo ya wachungaji na kuwarejesha ng’ombe katika maskani ya Mfalme. Naye Mfalme alimfanyia sikukuu Mbwa wake kwa kutimiza ahadi yake. Alimchinjia ndama dume. Kuwa na mkuki siyo kuwa na nguvu.

Huu ndio mwisho wa hadithi!

**Maswali ya ufahamu**

1. Habari hii ni ya aina gani? Eleza kinagaubaga.
2. Je, ni lipi jambo lililosababisha mawasiliano kati ya Mfalme na Mbwa wake?

3. Mheshimiwa Panya alifanya nini ili wachungaji na Mfalme wasije wakawachukua ng'ombe wake?
4. Zungumzia kidogo shukrani za Mfalme kwa Mbwa wake.
5. Eleza waziwazi kauli hii « Kuwa na mkuki siyo kuwa na nguvu ».

**2. 2. Msamiati kuhusu hadithi ya Kabeba**

**Kazi ya 2: Katika jozi elezeni maneno yafuatayo**

- Zizi
- Hatua
- Maskani
- Kwenda shoti
- Fahali

**Kazi ya 3:** *Katika jozi, tumieni maneno haya kwa kujenga sentensi zinazoonyesha kuwa mnaelewa maana za maneno vizuri*

**2.2. Sarufi: Aina za sentensi**

**Kazi ya 4:** *Katika jozi, tazameni sentensi zifuatazo kisha mzianishe*

a) Ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya Kabeba.
b) Ng'ombe hawa ni mali ya Bucyana.
c) Mfalme aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea.
d) Mfalme angejua kuwa alikuwa akizungumza na Kabeba asingekimbia.
e) Mbwa alipomwamkia mara ya tatu, kimya kilitawala.

**Kazi ya 5:** *Katika jozi tungeni sentensi shurutia tano*

***Kazi ya 6 :*** *Katika jozi, tungeni sentensi tegemezi tano.*

**2.3. Matumizi ya lugha : Dhana ya hadithi**

***Kazi ya 7:*** *Katika jozi someni maelezo yanayofuata ili uweze kueleza dhana ya hadithi na kujibu maswali yatakayofuata.*

Hadithi ni mtungo wa fasihi simulizi wenye visa vya kubuni unaosimuliwa kwa lugha ya nathari kwa kusudi la kuburudisha, kukuza maadili na kuunganisha jamii. Msimulizi wake huitwa fanani au mtambaji.

Hadithi huainishwa kulingana na wahusika. Hapo ndipo tuasema khurafa, hekaya, ngano, mighani na mazimwi. Vilevile hadithi huainishwa kulingana na maudhui: usuli, visasili na mtanziko. Kwa maelezo zaidi, khurafa ni hadithi ambazo wahusika ni wanyama. Hekaya ni hadithi yenye wahusika ambao ni watu tu. Ngano ni hadithi zenye wahusika ambao ni mchanganyiko wa watu, wanyama, miungu, mazimwi na vitu vingine ambavyo hupewa uhai na kutenda kama watu. Mighani ni hadithi za mashujaa. Mazimwi huwa na wahusika majitu au mazimwi. Usuli huelezea chanzo cha jambo au hali fulani. Visasili huelezea asili au chimbuko la jamii au mambo ya kiada k.v mauti, ndoa na tohara, ambapo mtanziko humwacha mhusika katika hali ya kutojua chaguo linalofaa. Kila achagualo lina matukio mabaya. Hadithi huwa na mianzo na mwisho maalum.

**Maswali:**

a) Hadithi ni nini?
b) Hadithi huwa na umuhimu gani katika jamii?
c) Taja aina za hatithi kulingana na wahusika.
d) Baada ya kusoma maelezo muhimu kuhusu dhana ya hadithi, kifungu ulichosoma hapo mwanzoni ni hadithi ya aina gani?
e) Hadithi huwa na mianzo maalum. Onyesha mianzo hiyo.

## 2.4. Kusikiliza na kuzungumza

***Kazi ya 8:*** *Mbele ya wanafunzi wenzako, simulia hadithi moja unaoyoifahamu kwa kuzingatia mianzo na miisho ya hadithi za kimapokeo kama zilivyoonyeshwa hapo juu.*

## 2.5. Kuandika

***Kazi ya 9:*** *Kwa kutumia Kiswahili fasaha, tunga hadithi moja unayoifahamu kutoka katika jamii ya Rwanda.*

### 1.5.2. Maelekezo ya ziada kwa mwalimu

Katika mada hii tumeongeza kazi mbalimbali ambazo zitamwongoza mwalimu kufanikisha kazi yake. Katika masomo yote ya mada hii tumeingiza sarufi. Kazi za sarufi nyingi zimo katika Kitabu cha Mwanafunzi lakini kurasa hazilingani sawasawa. Ndiyo maana mwalimu alielekezwa kwa namna ya kutafuta kazi hizo katika Kitabu cha Mwanafunzi. Zile ambazo hazipatikani ndani ya Kitabu cha Mwanafunzi ni zile zilizotayarishwa upya ili kukamilisha zile zilizomo katika kitabu cha mwanafunzi. Aidha, katika mada hii tumeingiza somo linalohusiana na "***Dhana ya hadithi simulizi"*** pamoja na kazi zote zinazohusiana na somo hilo zikiwa pamoja na majibu. Hii ni kwa sababu somo hili halimo katika kitabu cha mwanafunzi na linafaa kushughulikiwa katika mada hii. Yafuatayo ni majibu ya maswali yaliyoulizwa kwenye somo hilo:

***Kazi ya 1***

*Katika jozi, wanafunzi wasome kifungu cha habari kisha wajibu maswali ya ufahamu.*

**Kusoma na ufahamu: Kabeba**

***Kazi ya 1***

*Katika jozi, wasome kifungu kisha wajibu maswali ya ufahamu.*

**Majibu**

Habari hii ni hadithi simulizi ambayo ni ngano kwa sababu wahusika wake ni wanyama na binadamu.

Jambo lililosababisha mawasiliano kati ya MFALME na MBWA wake ni kitendo cha panya cha kuwafungia zizini kwake ng'ombe wa Mfalme walipoyavamia na kuyaharibu mashamba ya KABEBA.

Ili wachungaji na MFALME wasije wakawachukua ng'ombe wake, Mheshimiwa PANYA aliwafungia zizini na kutisha wachungaji kila mara walipojaribu kuja kuwachukua ng'ombe wa Mfalme. Maneno ya kuwatisha yalikuwa haya "Ni kweli kuwa ng'ombe hawa wanajichunga na kujirudisha wenyewe zizini lakini siyo bila sababu. Ng'ombe hawa wanatoka kwa BUCYANA. Mheshimiwa huyu ni Bwana Mwenda-mbio na Mwenda-pole-na-taratibu, Bwana Mkubwa wa juu mbinguni ambaye anaweza kuwakata, bila kusita, vidole vyenu vidogo ambavyo

vingetawanyika ardhini, Bwana ambaye angewapakulia ugali ambao kila anayekula kufumba na kufumbua ungemnenepesha”.

MBWA alipowarudisha ng’ombe wa Mfalme, MFALME alimfanyia sikukuu MBWA wake kwa kutimiza ahadi yake na kumchinjia ndama dume.

“Kuwa na mkuki siyo kuwa na nguvu“. Kauli hii inamaanisha kuwa kuwa na uwezo wa kujilinda siyo kushinda. Ni kusema kwamba wachungaji wa ng’ombe wa Mfalme walikuwa na mikuki na silaha nyingine za kutumia ili kujilinda na kupigania ng’ombe wa Mfalme lakini PANYA hakuwa na kitu chochote. Walakini, walipokuja kuwachukua ng’ombe hao, PANYA aliwatisha kwa kutumia ulimi wake tu na kuweza kuwakimbiza. Jambo hili linaonyesha kwamba kuwa na silaha siyo kushinda.

**Msamiati**

***Kazi ya 2*:**

*Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutafuta maana za misamiati.*

**Zizi**: boma liliojengwa maalumu kwa minajili ya kufugia mifugo.

**Hatua**: nafasi kati ya wayo huu na wayo huo wa mtu anayetembea.

**Maskani**: mahali anapokaa mtu; makao

**Kwenda shoti**: kwenda mbio

**Fahali**: ng’ombe dume; dume la mnyama

**Kazi ya 3:**

*Katika makundi madogomadogo, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wameandika sentensi sahihi wakitumia maneno waliyopewa na awaelekeze panapohitajikwa.*

**Sarufi: Aina za sentensi za Kiswahili**

***Kazi ya 4:***

*Katika makundi yao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuanisha sentensi.*

a) Ng’ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya Kabeba. (sentensi sahili)
b) Ng’ombe hawa ni mali ya Bucyana. (Sentensi sahili)

c) Mfalme aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea. (sentensi ambatano)
d) Mfalme angejua kuwa alikuwa akizungumza na Kabeba asingekimbia. (Sentensi shurtia)
e) Mbwa alipomwamkia mara ya tatu, kimya kilitawala. (sentensi changamano)

***Kazi ya 5:***

*Katika jozi, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanaweza kutunga sentensi shurtia.*

***Kazi ya 6:***

*Katika jozi, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanaweza kutunga sentensi tegemezi.*

**Matumizi ya lugha: Dhana ya hadithi simulizi**

***Kazi ya 7:*** *Katika jozi, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamesoma maelezo muhimu kuhusu dhana ya hadithi kisha wajibu maswali.*

***Majibu:***

a) Hadithi ni mtungo wa fasihi simulizi wenye visa vya kubuni unaosimuliwa kwa lugha ya nathari.
b) Hadithi huwa na umuhimu wa kuburudisha, kukuza maadili na kuunganisha jamii.
c) Khurafa, hekaya, ngano, mighani na mazimwi
d) Hadithi hii ni ngano kwa sababu ina wahusika ambao ni mchanganyiko wa watu na wanyama.
e) **Hadithi huwa na fomula yake katika utangulizi wake**

   **Ifuatayo ni mifano:**

   Mianzo ya hadithi za kimapokeo

   **Mtambaji**: Paukwa

   **Hadhira**: Pakawa

   **Mtambaji**: Paukwa

   **Hadhira**: Pakawa

   **Mtambaji**: Kaondokea chanjagaa
   Kajenga nyumba kaka
   Mwanangu mwana siti

Vijino kama chikichi

Cha kujengea kikuta

Na vilango vya kupitia

Atokeani

Hapo zamani za kale………………….

1. **Mtambaji**: Paukwa

   **Hadhira**: Pakawa

   **Mtambaji**: Sahani!

   **Hadhira**: Ya mchele!

   **Mtambaji**: Giza

   **Hadhira**: La mwizi

   **Mtambaji**: Baiskeli

   **Hadhira**: ya mwalimu! n.k.

   **Mtambaji**: Hadithi hadithi!

   **Hadhira**: Hadithi njoo!

   **Mtambaji**: Hadithi hadithi!

   **Hadhira**: Hadithi njoo!

   **Mtambaji**: Hapo zamani za kale palikuwepo na …………………………

2. **Msimulizi**: Atokaeni!

   **Hadhira**: Naam Twaibu!

   **Msimulizi**: Kaondokea chanjagaa, n.k.

**Kusikiliza na kuzungumza**

***Kazi ya 8:***

*Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi atasimulia hadithi moja anaoyoifahamu kwa kuzingatia mianzo na miisho ya hadithi za kimapokeo.*

**Kuandika**

***Kazi ya 9:***

*Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ametunga hadithi moja anayoifahamu kutoka katika jamii ya Rwanda kwa kutumia Kiswahili fasaha.*

## 1.6. TATHMINI YA MADA YA KWANZA

☞ (***Uk. 103)***

*Mwalimu ahakikishe kuwa tathmini hii itafanyika kama kazi binafsi ili kupima kiwango cha weredi wa mwanafunzi kuhusu mada husika.*

**Majibu**

1. Fasihi simulizi ni hazina ya kazi za kubuni za sanaa inayotumia lugha yaani maneno kama njia ya kuwasilisha mambo yake.
2. “Nadharia ya msambao”: Waasisi wa nadharia hii niJacob na Wilhem Grimm. Baadaye mawazo yao yaliendelezwa na Maxmuller na Mmarekani Stere Thomson. Licha ya tofauti ndogondogo, wataalamu wa nadharia hii wanaamini kwamba chimbuko la fasihi simulizi ni moja lakini kutokana na maingiliano ya kijamii, fasihi simulizi ilisambaa hasa kutoka jamii zilizostaarabika (Ulaya) kuja katika jamii zisizostaarabika (Afrika). Baadhi yao walisema kuwa hadithi simulizi zilisambazwa na makundi ya wahamiaji kutoka India na kufika huko Magharibi kwa njia ya msambao.

3. Mdhamini ndiye anayeainisha nyanja za kufanyia utafiti, aula za utafiti na watafiti wenyewe. Ndiye anayetoa fedha na nyenzo za utafiti na kupokea matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, mtafiti analazimishwa kuwa karagosi wa mdhamini na matokeo ya utafiti yataathiriwa na mawazo ya mdhamini.
4. (Kila mwanafunzi atatunga shairi lake).
5. Toa maana ya semi fupi hizi:
   - Kuponda raha: Kuishi kwa furaha na amani
   - Kuona cha mtemakuni: Kupata mateso

- Jogoo la shamba haliwiki mjini: Yeyote aliye ugenini inampasa kufanya mambo kwa tahadhari ili kulingana na mazingira ya hapo
- Uchungu wa mwana aujuaye mzazi: Mwenye kuthamini kitu chochote kile ni yule mwenye kitu hicho kwani ndiye aliyetaabika katika kukitafuta na kukipata

6. **Tegua vitendawili hivi:**
- Hazikauki umande // Pua za mbwa
- Mtoto ana ndevu mzazi hana // Hindi

**Kuainisha sentensi:**

1. Tungepata bomba za kutosha, tungekunywa maji safi. (Sentensi shurutia/ SSH)
2. Wanyarwanda walifurahi *waliposikia serikali yao imeunda mikakati thabiti ya kutunza*
   SS ST
*mazingira*. (Sentensi changamano/ SCH)
3. Viongozi wote ulimwenguni ni watumwa wa raia. (Sentensi sahili/ SS)
4. Wanafunzi hawa wakisoma kwa bidii watafaulu mtihani wa taifa. (Sentensi shurutia/ SSH)
5. Walioshindwa *si wanafunzi wa shule yetu*. (Sentensi changamano)

   ST SS

6. Walimu wetu wasingalikuwa na muda wa kutosha wasingaliweza kutusaidia katika kazi zetu. (Sentensi shurutia/ SSH)

## 1.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI

### 1.7.1. Kazi za urekebishaji

Mapendekezo ya maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wasio na uelewa wa haraka.

1. Taja tanzu kuu za fasihi simulizi na vipera vyake.

a. Hadithi ni nini?

b. Toa nahau tano zenye kitenzi “kupiga”

c. Malizia methali hizi

- Chelewachelewa.........
- Tamaa mbele........

d. Tegua vitendawili vifuatavyo:
   - Nyumba yangu haina mlango.
   - Popoo mbili zavuka mto.
e. Taja mifano mitano ya mashairi
f. Taja aina za sentensi kulingana na maana.

**Majibu**

1. *Tanzu za fasihi simulizi ni hadithi, methali, nahau, vitendawili, nyimbo na mashairi*
2. *Hadithi ni mtungo wa fasihi simulizi wenye visa vya kubuni unaosimuliwa kwa lugha ya nathari*
3. *Kupiga deki, kupiga mswaki, kupiga kalamu, kupiga kura, kupiga moyo konde, ...*
4. *Kumalizia methali*
   - *Chelewachelewa* ***utamkuta mtoto si wako.***
   - *Tamaa mbele* ***mauti nyuma.***
5. *Tegua vitendawili vifuatavyo:*
   - *Nyumba yangu haina mlango:* ***yai***
   - *Popoo mbili zavuka mto:* ***Macho***
6. *Kuna mashairi ya wasifu, mashairi ya simango, mashairi ya waadhi, mashairi ya kashifa, mashairi ya uzinduzi, ...*
7. *Kuna sentensi nyoofu na sentensi tata.*

### 1.7.2. Kazi za uimarishaji

1. Fasihi simulizi ni kongwe. Eleza.
2. Hadithi huwa na umuhimu katika jamii. Eleza.
3. Ni tofauti gani iliyoko baina ya nahau na misemo?
4. Linganisha methali za kinyarwanda zinazolingana na hizi za Kiswahili.

   - Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

- Zimwi likujualo halikuli likakwisha.

**Majibu**

1. *Fasihi simulizi ni kongwe kwa sababu ni fasihi ya zamani za kale. Hatujui wakati iliapoanza.*
2. *Hadithi huwa na umuhimu wa kuburudisha, kukuza maadili na kuunganisha jamii.*
3. *Nahau hudai kitenzi lakini misemo haidai kitenzi.*
4. *Kulinganisha methali za Kinyarwanda zinazolingana na hizi za Kiswahili.*

   - *Asiyesikia la mkuu huvunjika guu : Uwanze kumvira se na nyina yumvira ijeri.*

   - *Zimwi likujualo halikuli likakwisha : Impyisi y'iwanyu ikurya ikurundarunda.*

### 1.7.3. Kazi za wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Mapendekezo ya maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wenye uelewa wa haraka.

1. Namna gani fasihi inavyoweza kusababisha utengamano wa jamii?
2. Mtu alitenda matendo ya kishujaa katika jamii kisha akatungiwa hadithi, hadithi hiyo itaiwaje?
3. Ni methali ipi inayoweza kutumiwa wakati mtu fulani ameshindwa kutimiza aliyoyasema?
4. "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo." Methali hii inamaanisha nini?
5. Ushairi wa Kiswahili ulianzishwa namna gani?

**Majibu**

1. Fasihi inaweza kuwa chanzo cha madhara katika jamii inapotumiwa vibaya kupitia nyimbo na methali zinazochochea ubaguzi na uadui baina ya wanajamii. Mfano ni jinsi nyimbo zilivyochochea uhasama baina ya wananchi na kuishia kwenye Mauaji ya Kimbari dhidi ya Watusti yaliyotokea nchini Rwanda mnamo mwaka wa 1994.
2. Hadithi hiyo itaitwa mighani.

3. Ahadi ni deni.

4. “Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo” Methali hii inamaanisha kwamba jinsi unavyomlea mtoto wako ndivyo atakavyokua. Yaani ukimpa malezi mazuri naye atakuwa mzuri, yakiwa mabaya naye atakuwa mbaya vile vile.

5. Kutokana na kazi alizokuwa akifanya, binadamu alianza kutunga maneno na sauti za muziki zilizokuwa zikifuata mapigo ya kazi. Wimbo wa kazi ukawa ndio utanzu wa fasihi wa mwanzo. Polepole, ushairi wa Kiswahili ulianzishwa kwa kuiga mapigo ya nyimbo.

## MADA KUU YA 2: UHAKIKI NA UWASILISHAJI KATIKA FASIHI SIMULIZI

## MADA NDOGO: UHAKIKI WA FANI NA MAUDHUI KATIKA FASIHI SIMULIZI

### 2.1. Uwezo upatikanao katika mada

- Kuhakiki fani na maudhui katika fasihi simulizi ya Kiswahili;
- Kuchambua sentensi kufuatana na muundo wake.

### 2.2. Ujuzi wa awali

Katika kidato cha nne, wanafunzi walisoma masomo ambayo yanahusu uhakiki wa kazi za Fasihi simulizi hasa uhakiki wa hadithi simulizi. Masomo hayo yanapatikana katika mada kuu ya 3 ambayo ni "***Uhakiki wa hadithi za masimulizi katika Kiswahili***." Masomo hayo ni kama vile:

- ➢ Somo la 16: Fani katika hadithi simulizi
- ➢ Somo la 17: Maudhui katika hadithi simulizi
- ➢ Somo la 18: Uhakiki wa hadithi simulizi

### 2.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake

#### 2.3.1. Kidokezo cha mada

Kwa kutangulia mada, mwalimu aulize maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua mada hii. Maswali hayo yanapaswa kuzingatia maudhui ya mada nzima. Hapa mwalimu anaweza kuuliza maswali yafuatayo:

- Uhakiki wa fasihi simulizi katika Kiswahili ni nini?
- Ni nini umuhimu wa uhakiki?
- Mbinu za uhakiki wa kazi za fasihi simulizi ni zipi?

#### 2.3.3. Maelekezo kuhusu kidokezo cha mada

- Mwalimu atoe mwongozo wa kutoa jibu kwa kazi.
- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia kazi nyingine zilizotayarishwa au masomo ya mada nzima.

## 2.4. Orodha ya masomo

| | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | Dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi katika Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi katika Kiswahili<br><br>**Stadi :** Kujadili dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi katika Kiswahili pamoja na mbinu za uhakiki.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuimarisha tabia ya kusoma na kufanya uhakiki wa kazi zilizosomwa | 6 |
| 2 | Uhakiki wa hadithi katika Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha vipengele vya uhakiki wa hadithi simulizi.<br><br>**Stadi**: Kuchambua hadithi simulizi kwa kuzingatia fani na maudhui.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kukuza fikra na tafakuri tunduizi katika uhakiki wa kazi za fasihi. | 16 |
| 3 | Uhakiki wa methali katika Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza matumizi ya methali mbalimbali<br><br>**Stadi**: Kuchambua methali mbalimbali kulingana na vipengele vya uchambuzi.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujenga busara, maadili na adabu kupitia methali za Kiswahili. | 12 |
| 4 | Uhakiki wa vitendawili katika Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha sehemu kuu za kitendawili.<br><br>**Stadi:** Kuchambua vitendawili mbalimbali. | 8 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | **Maadili na mwenendo mwema:** Kufurahia mchezo wa chemshabongo kutokana na utegaji na uteguaji wa vitendawili. | |
| 5 | Uhakiki wa nahau na misemo katika Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza muundo wa nahau na misemo katika Kiswahili<br><br>**Stadi**: Kuchambua nahau na misemo.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuimarisha tabia ya kuwa wazi na kutumia lugha ya mkato katika mawasiliano. | 14 |
| 6 | Uhakiki wa mashairi simulizi katika Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kutambua umbo la shairi simulizi katika Kiswahili.<br><br>**Stadi :** Kuhakiki shairi<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kukuza fikra na tafakuri tunduizi katika uhakiki wa mashairi. | 14 |
| - | Sarufi: Muundo wa sentensi | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha sehemu kuu za sentensi<br><br>**Stadi :** Kuchambua sentensi kwa kuonyesha sehemu zake kuu.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema** Kuwa na utaratibu wa kuainisha, kulinganisha au kutofautisha mambo. | - |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Vipindi vyote vya mada ya kwanza** | | | **72** |

**Tnbh:** Sarufi huja kila wakati ndani ya kila somo baada ya kufundisha msamiati.

☞ **Kila somo huwa na kazi za aina sita :**

- Kazi zinazohusu kusoma na ufahamu
- Kazi zinazohusu msamiati
- Kazi za sarufi
- Kazi zinazolingana na matumizi ya lugha
- Kazi za kusikiliza na kuzungumza
- Kazi za kuandika

## SOMO LA 1: DHANA YA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI KATIKA KISWAHILI

### i. Malengo ya ujifunzaji

Katika somo hili, mwanafunzi ataweza:

- Kueleza dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi katika Kiswahili;
- Kujadili dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi simulizi katika Kiswahili pamoja na mbinu za uhakiki.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Vitabu vya fasihi,
- Ubao,

- Chaki,
- Redio,
- Michoro mbalimbali, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

**iii. kuhusu kazi za ujifunzaji**

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**i. Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.105)***

*Kazi hii ifanyike katika makundi madogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kueleza kichwa cha kitabu kinachoonekana kwenye picha.*

**Dokezo**:

Nadharia ni maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani. Uhakiki ni dhana ya kueleza na kuchunguza kwa makini kazi ya sanaa. Kwa hiyo, “nadharia ya uhakiki wa fasihi” ni maelezo yanayohusu kueleza na kuchunguza fasihi.

***Kazi ya 2: (uk. 105)***

*Katika makundi yao, wanafunzi wasome kifungu cha habari kisha wakihusishe na picha.*

**Dokezo**:

Kwenye picha kumeandikwa “Nadharia za uhakiki wa fasihi” na jambo hilo ndilo linaloshughulikiwa katika matini yetu.

**Kusoma na ufahamu: Uhakiki wa kazi za fasihi simulizi**

***Kazi ya 3: (uk.108)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma kifungu upya na kujibu maswali ya ufahamu.*

**Majibu**

1. Uhakiki unaweza kuchukuliwa kama kitendo cha kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalumu. Ni kusema kuwa uhakiki ni uchambuzi wa ndani kabisa wa jambo lililozingatiwa na fikra za mchambuzi.
2. Uhakiki wa kazi za fasihi ni mkongwe kwa sababu kuwepo kwake kulianza wakati binadamu alipokuwa na uwezo wa kuzungumza na kuadhiri maoni na maisha ya wengine.
3. Vipengele vya uhakiki wa kazi za fasihi vinavyoshughulikiwa ni maudhui na fani.
4. Maudhui hujumuisha vigezo kama vile kichwa cha habari, dhamira (kuu na ndogondogo), ujumbe, falsafa ya mtunzi, migogoro na muhtasari wa habari. Fani huundwa na wahusika, muundo, mtindo au matumizi ya lugha na mandhari.
5. Dhima ya uhakiki wa kazi za fasihi katika maisha ya mwanafunzi ni:

- Kumwezesha kuielewa, kuieleza na kuifaidi kazi ipasavyo;
- Kumwezesha kulinganisha kazi tofauti za fasihi;
- Kumwezesha kuchambua na kufafanua mifumo na picha za kisanaa zinazotumika katika kazi za fasihi ili kupevuka katika lugha;

- Kumwezesha kuchambua na kuweka hadharani maonyo yanayopati kana katika kazi za fasihi. Maonyo hayo tunaweza kuyatumia kwa kuwa kosoa wanajamii wengine.

**Msamiati (uk: 110)**

***Kazi ya 4:*** Katika pea, tumieni Kamusi ya Kiswahili Sanifu na kuchunguza maana ya maneno yafuatayo: 1. Ukongwe 2. Kuadhiri 3. Kutathmini 4. Janga 5. Tajiriba

- *Kazi hii iyanyike kwa makundi madogomadogo au pea. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutafuta maana za maneno waliyopewa. Yafuatayo ni mapendekezo ya majibu:*

- **Ukongwe:** hali ya kuzeeka,
- **Kutathmini**: kuchanganua kitu kwa makini ili kukadiria ubora wake; kutia kitu thamani; kuthamini
- **Tajiriba:** uzoefu mtu alio nao katika kutenda jambo
- **Kuadhiri:** kuvunjia heshima; kuaibisha
- **Janga:** balaa; hatari; tabu

***Kazi ya 5:*** Katika pea hiyo, tungeni sentensi kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

- *Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo au pea. Mwalimu ahakikise kwamba kila kundi limetunga sentensi sahihi.*

**Mfano**: Uzoefu mtu alionao katika kutenda jambo huitwa tajiriba.

**Sarufi: Miundo ya sentensi (uk. 195-196)**

***Kazi ya 6 :*** Soma sentensi zifuatazo:

1. Viwanda huhitaji malighafi na vipuli.

2. Nchi zetu hukitazama kilimo kama uti wa mgongo wa maendeleo yake.

3. Vitu vyote hivi ni matokeo ya kazi za viwanda.

4. Nchi nyingi hushindwa kuagiza malighafi muhimu na hupata hasara viwandani.

Ni yapi maoni yako kuhusu muundo wa sentensi hizo?

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma sentensi na kutoa maoni kuhusu miundo yake.*

**Jibu lililopendekezwa:** Muundo wa sentensi hizi si sawa unapozingatia aina ya maneno yanayoziunda lakini zote zina kiima na kiarifu.

***Kazi ya 7 :*** *Katika jozi, onyesheni aina za maneno yanayoziunda sentensi hizo (tumieni vifupisho kama vile N, T, W,...).*

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuonyesha aina za maneno zinazounda sentensi walizopewa kwa kutumia vifupisho.Majibu ni haya yafuatayo:*

1. Viwanda huhitaji malighafi na vipuli.
   N T N U N
2. Nchi zetu hukitazama kilimo kama uti wa mgongo wa maendeleo yetu.
   N V T N U N V N V N V
3. Vitu vyote hivi ni matokeo ya kazi za viwanda.
   N V V t N V N V N

4. Nchi nyingi hushindwa kuagiza malighafi muhimu na hupata hasara viwandani.
   N V Ts T N V U T N E

***Kazi ya 8 :*** Shirikiana na mwenzako na kutafuta kwenye intaneti au katika vitabu maelezo mbalimbali kuhusu muundo wa sentensi za Kiswahili. Msisahau kuwasomea wenzenu matokeo ya kazi yenu.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kufanya utafiti kuhusu muundo wa sentensi kisha wawasilishe matokeo. Kila kundi litatoa matokeo ya utafiti.*

***Kazi ya 9:*** Kwa kushirikiana na mwenzako, elezeni kwa kutoa mifano maana ya vipashio vifuatavyo:

a) Kiima b) Kiarifu c) Shamirisho d) Chagizo e) Kipashio

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu ahakikishe kuwa kila kundi limeeleza maneno yaliyotolewa. Yafuatayo ni maelezo kwa kila kipashio:*

a. "Kiima": ni neno au fungu la maneno katika sentensi ambalo hutangulia kitenzi. Aghalabu huonyesha mtenda.

b. "Kiarifu": ni sehemu ya sentensi yenye kitenzi, shamirisho na chagizo.

c. "Shamirisho": ni sehemu ya sentensi inayowakilisha kitu kilichofanyiwa jambo. Ni mtendwa au mtendewa katika sentensi. Ni sehemu inayojibu swali "nini?", "nani?"

d. "Chagizo" : hutueleza zaidi kuhusu kiima na shamirisho. Aghalabu, chagizo ni kielezi.

e. "kipashio" : kipande cha tungo ambacho kinaweza kujengwa na neno moja au zaidi.

**Matumizi ya lugha *(uk. 111)***

***Kazi ya 10 :*** Katika jozi, changanueni maneno haya kufuatana na maana yake na kuyaandika katika vikundi vyake halisi:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Dhamira<br>Mshairi<br>Udongo<br>Mandhari<br>Wahusika<br>Chandarua<br>Mtindo | Fani | Maudhui | Mengine |

- *Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadog au jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuchanganua maneno na kuyaandika katika vikundi vyake. Yafuatayo ni majibu:*

| Maneno | Fani | Maudhui | Mengine |
|---|---|---|---|
| Dhamira<br>Mshairi<br>Udongo<br>Mandhari<br>Wahusika<br>Chandarua<br>Mtindo | Mshairi<br>Mandhari<br>Wahusika<br>Mtindo | Dhamira | Udongo<br>Chandarua |

**Kusikiliza na kuzungumza *(uk.111)***

***Kazi ya 11:*** Jiunge na wenzako wawili na kueleza vizuri kauli ifuatayo: "Vigezo vya uhakiki huainishwa kulingana na wajibu unaohitajika kutekelezwa na kazi fulani na utanzu unaohusika."

- *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kueleza vizuri kauli waliyopewa.*

**Dokezo**:

"Vigezo vya uhakiki huainishwa kulingana na wajibu unaohitajika kutekelezwa na kazi fulani na utanzu unaohusika." Ni kusema kwamba kuna vipengele viwili vya uhakiki lakini vigezo vinavyoainishwa katika vipengele hivyo si sawa kwa tanzu zote. Kuna tanzu zinazofanyiwa uhakiki kwa kupendelea vigezo fulani na kuacha vingine. Vilevile, mtu anaweza kuchagua vigezo mbalimbali atakavyopendelea katika uhakiki wake kutokana na lengo analotaka kufikia. Lengo hili ndilo linalochukuliwa kama wajibu unaohitajika kutekelezwa au kazi fulani.

**Kuandika *(uk.111)***

***Kazi ya 12:*** Kwa njia ya mazungumzo, shirikiana na mwenzako na kueleza kauli hii: "Maswali yanayojibiwa katika uhakiki ni nini, nani na vipi."

- ➢ *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila manafunzi ameeleza kauli aliyopewa.*

**Maelekezo**: **-Nini?**: Ni kusema linalozungumziwa;

**-Nani?**: Ni kusema anayesema au anayefanya kazi fulani;

**-Vipi?**: Ni kusema namna gani jambo fulani linavyofanyika.

## SOMO LA 2 : UHAKIKI WA HADITHI KATIKA KISWAHILI

### i. Malengo ya ujifunzaji

Kapitia kwa somo hili mwanafunzi ataweza:

- Kubainisha vipengele vya uhakiki wa hadithi simulizi.
- Kuchambua hadithi simulizi kwa kuzingatia fani na maudhui.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

- ➢ Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- ➢ Kitabu cha mwanafunzi
- ➢ Vitabu vya fasihi
- ➢ Ubao
- ➢ Chaki, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu ulani.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, ula. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro ulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**iv. Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.114)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutazama picha na kutoa maoni kuhusu picha hiyo.*

***Dokezo**:*

Picha hii inaonyesha wasichana wawili pamoja na mvulana mmoja. Nyuma yao kuna viumbe wengine.

***Kazi ya 2: (uk.114)***

*Katika makundi yao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma kifungu cha habari na kukihusisha na picha.*

***Dokezo***

Picha hii inaonyesha Nyambere na Mariya katika safari yao kuelekea kwa mumewe Mariya baada ya kufunga ndoa. Wameandamana na viumbe wengine ambao ni mazimwi, jambo ambalo linazungumziwa katika kifungu cha habari.

**Kusoma na ufahamu: NYAMBERE**

***Kazi ya 3: (uk.117)***

*Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma kifungu cha habari upya na kujibu maswli ya ufahamu.*

**Majibu**:

1. Hadithi hii ni ngano kwa sababu wahusika wake ni binadamu wanaochanganywa na mazimwi.
2. “Mariya alikuwa msichana asiye na makini.” Jambo linalodhihirisha kauli hii ni kwamba Mariya alipoelezewa habari hii, aliipuuza na kusema kwamba ni uvumi.
3. Watu walioambatana na mumewe Mariya katika safari yake kwenda kumchukua mchumba wake walikuwa vichaka. Vichaka hivyo vilikuwa vimegeuzwa na zimwi hilo kuwa watu.
4. Maajabu yaliyofanywa na mumewe Mariya ni kama vile:
   - Kujigeuza kuwa zimwi;
   - Kumkatakata Mariya vipande vipande wakati wa usiku na ilipofika asubuhi, kuviunga vipande hivyo tena na kumtengeneza Mariya;
   - Kuning’inia kwenye paa;
   - Kula mijusi kafiri ambayo haikupikwa;
   - Kujigeuza kuwa kware na kadhalika.

**Msamiati (uk.118-119)**

***Kazi ya 4:*** Kwa kutumia kamusi, jadiliana na mwenzako juu ya maana ya maneno yafuatayo: Dondoo, Uchumba, Mkwe.

- ➢ *Kazi hii ifanyike kwa makundi madogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutafuta maana za maneno katika kamusi.Yafuatayo ni majibu:*

- **Dondoo:** Tabia ya uzinifu; uzinzi
- **Uchumba:** Makubaliano ya pande mbili baina ya mwanamke na mwanamume wanaotaka kuoana
- **Mkwe:** Jina la heshima aitwalo baba, mama, au ndugu wa mzazi ambaye ulan wake ameoa au kuolewa na mtu fulani wa ulan huyo; mcheja
- **Kichaka:** Mahali penye miti mifupimifupi na nyasi, miiba na kadhalika; kituka

***Kazi ya 5:*** Kila mmoja kati yenu atunge sentensi moja kwa kila neno kati ya haya manne ya hapa juu.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ametunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno aliyopewa.*

**Mfano:** Katika utamaduni wa Wanyarwanda, mama mkwe hawezi kuchangia chakula na mkwe wake.

***Kazi ya 6:*** Kamilisha sentensi zifuatazo zilizotumiwa katika kifungu chetu cha habari:

| |
|---|
| 1. Kumbe ilikuwa sauti ya..................aliyekuwa akiyarudia maneno ya Nyambere kabla ya kutoroka. |
| 2. Katika nchi ya mumewe kulikuwako na ............. wengi ambao walikuwa wameletwa kutoka nchi za mbali na kuolewa huko. |
| 3. Mume naye alijigeuza kuwa zimwi na kuanza ............... akiwafuata Mariya na nduguye. |

- *Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujaza sentensi. Yafuatayo ni majibu:*

| |
|---|
| 1.Kumbe ilikuwa sauti ya **kasuku** aliyekuwa akiyarudia maneno ya Nyambere kabla ya kutoroka. |
| 2.Katika nchi ya mumewe kulikuwako na **wanawake** wengi ambao walikuwa wameletwa kutoka nchi za mbali na kuolewa huko. |
| 3.Mume naye alijigeuza kuwa zimwi na kuanza **kupaa juu** akiwafuata Mariya na nduguye. |

**Sarufi: Muundo wa sentensi (uk. 196)**

***Kazi ya 7:*** Shirikiana na mwenzako na kuonyesha muundo wa sentensi zifuatazo:

1. Serikali ya Rwanda iliunda mikakati thabiti ya kuboresha uzazi.

2. Umoja wa wananchi ni nguzo muhimu ya amani na maendeleo.

3. Nchi yake huagiza malighafi kutoka Rwanda.

- *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuonyesha miundo ya sentensi. Majibu ni haya yafuatayo:*

1. Serikali ya Rwanda iliunda mikakati thabiti ya kuboresha uzazi.(*Mikakati thabiti ya*
   Kiima Kiarifu
*kuboresha uzazi: Shamirisho*)

2. Umoja wa wananchi ni nguzo muhimu ya amani na maendeleo. (*Nguzo muhimu ya amani*
   Kiima Kiarifu
*na maendeleo*: Kijalizo)
3. Nchi yake huagiza malighafi kutoka Rwanda.(*Malighafi kutoka Rwanda*: Shamirisho)
   Kiima Kiarifu

***Kazi ya 8:*** Katika jozi hiyo, kamilisheni sentensi hizi kwa istilahi inayotakiwa:
1. ................... ni neno au fungu la maneno katika sentensi ambalo hutangulia kitenzi. Aghalabu huonyesha mtenda.
2. ........................ ni sehemu inayoundwa na kitenzi, shamirisho na chagizo.
3. ................. ni sehemu ya sentensi inayowakilisha kitu kilichofanyiwa jambo yaani mtendwa au mtendewa katika sentensi.

- *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kujaza sentensi.Yafuatayo ni majibu:*

1. **Kiima** ni neno au fungu la maneno katika sentensi ambalo hutangulia kitenzi. Aghalabu huonyesha mtenda.
2. **Kiarifu** ni sehemu inayoundwa na kitenzi, shamirisho na chagizo.

3. **Shamirisho** ni sehemu ya sentensi inayowakilisha kitu kilichofanyiwa jambo yaani mtendwa au mtendewa katika sentensi.

**Matumizi ya lugha (uk. 121)**

***Kazi ya 9:*** Andika jedwali hili katika daftari lako na kujaza sentensi zifuatazo kama zilivyo katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. Mariya alipoona mumewe amegeuka kuwa zimwi, alishikwa na woga na ........... ovyo. |
| 2. Basi Nyambere, kwa kutumia vijiti na ..................... za kuvifanya vitu mbalimbali viruke angani, aliitengeneza ndege na kuweka mlango mdogo. |
| 3. Basi mwanamume huyu alipomwuliza Mariya kama .......... naye, alikubali bila kusita. |

- *Kazi hii iwe ya kibinafsi. Kila mwanafunzi ajaze sentensi hizi kama zilivyo katika kifungu cha habari. Yafuatayo ni majibu:*

| |
|---|
| 1. Mariya alipoona mumewe amegeuka kuwa zimwi, alishikwa na woga na kutetemeka ovyo. |
| 2. Basi Nyambere , kwa kutumia vijiti na nguvu zake za kichawi za kuvifanya vitu mbalimbali viruke angani, aliitengeneza ndege na kuweka mlango mdogo. |
| 3. Basi mwanamume huyu alipomwuliza Mariya kama angeweza kuolewa naye, alikubali bila kusita |

**Kusikiliza na kuzungumza (uk. 128)**

***Kazi ya 10:*** Jiunge na wenzako wawili na kuchagua hadithi simulizi moja ya Kiswahili. Baada ya kuisoma polepole na kuielewa, muifanyie uhakiki kwa kuzingatia mwongozo wa uchambuzi uliotolewa. Msisahau kuwasilisha matokeo ya kazi yenu kwa wanafunzi wengine.

- *Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutafuta hadithi na kuifanyia uhakiki kisha waiwasilishe kazi yao darasani.*

**Kuandika**

***Kazi ya 11:***

*Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi: Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ametunga hadithi na kuifanyia uhakiki.*

## SOMO LA 3: UHAKIKI WA METHALI KATIKA KISWAHILI

**i. Malengo ya ujifunzaji**

Kapitia kwa somo hili mwanafunzi ataweza:

- Kueleza matumizi ya methali mbalimbali;
- Kuchambua methali mbalimbali kulingana na vipengele vya uchambuzi.

**ii. Zana au vifaa vya ufundishaji**

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kitabu cha mwanafunzi
- Vitabu vya fasihi
- Ubao
- Chaki, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu,  ula. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro ulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**iv. Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.128)***

*Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutazama picha na kueleza kilichoandikwa juu.*

**Dokezo**:

Kwenye picha kuna wanyama wawili wanaopambana na kumeandikwa “Fahali wawili wakipigana, nyasi huumia.”

***Kazi ya 2: (uk.128)***

*Kazi hii ifanyike kwa jozi. Mwalimu awaagize wanafunzi kutaja* utanzu wa Fasihi Simulizi unaolingana na picha waliyopewa.

- Ni methali ya Kiswahili.

***Kazi ya 3: (uk. 128)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma kifungu cha habari na kukihusisha na picha.*

**Dokezo**

Kwenye picha kumeandikwa “Fahali wawili wakipigana, nyasi huumia”. Hii ni methali na kifungu cha habari kinazungumzia kuhusu “uhakiki wa methali”.

**Kusoma na ufahamu: Vipengele muhimu vya uhakiki wa methali**

**Kazi ya 4:** *Majibu ya maswali ya ufahamu ni yafuatayo:*

1. "Methali huwa na maana ya nje na maana ya ndani au maana yenyewe". Hebu tutoe mfano wa methali "Kidole kimoja hakivunji chawa". Chawa ni kidudu kinachokaa kwenye mwili wa binadamu hasa katika nywele na nguo chafu na hunyonya damu yake. Ufafanuzi wake au maana yake ya nje ni kuwa mtu hawezi kumwua chawa kwa kidole kimoja. Ni lazima ambanie katikati ya vidole viwili. Maana yake ya ndani ni kuwa "mtu mmoja hawezi kufanya kazi inayohitaji watu wengi."
2. "Methali huwa na mazingira yake". Kila methali huelezea uwanja fulani wa maisha ya mtu kama vile ukulima, amani na maendeleo, usawa wa jinsia, uzalishajimali, burudani, uimbaji na kadhalika.
3. Methali hutambuliwa haraka kutokana na muundo na lugha yake.
4. Methali hizi huzungumzia uwanja (mazingira) gani ya maisha?
   - Mpanda farasi wawili hupasuka msamba // Ufugaji
   - Mchovya asali hachovyi mara moja // Chakula
   - Mbuzi wa maskini hazai mapacha // Ufugaji

**Msamiati (uk. 133)**

***Kazi ya 4 :*** Shirikiana na mwenzako na kutumia kamusi ili kutafuta maana ya maneno yafuatayo: Mkizi, Utengano, Udhaifu, Ukinzani, Ndwele ,Kuganga.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi. Mwalimu awaagize wanafunzi kutoa maana za maneno. Yafuatayo ni majibu:*

- **Mkizi:** Aina ya samaki wa baharini ambaye anaweza kuruka sana
- **Utengano:** Hali ya kuweka mtu kando
- **Udhaifu:** Hali ya kudhoofika au kutokuwa na nguvu au kuwa mnyonge
- **Ukinzani:** Hali ya ukaidi; upinzani
- **Ndwele (uwele):** Maumivu mwilini; ugonjwa

- **Kuganga**: Kufanyia mgonjwa matibabu; kutengeneza kilichovunjika au kuharibika

***Kazi ya 5:*** Katika pea, tumieni maneno hayo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika kifungu cha habari kifuatacho:

• Dunia ni mti mkavu wenye maajabu mengi. Linaloshangaza ni kuwa watu wake wengi hawapendi kushirikiana na wenzao. Wao husahau kwamba hawana budi kuutupilia mbali.....................ili waishi katika utengemano. Hawajui kwamba hali hii ni................ kabisa! Unapowahamasisha kuhusu jambo hilo, wao hupinga na kuruka kama .............. baharini. Ni kweli kuwa ..................... huo ni kizuizi cha maendeleo yao binafsi na ya nchi zao. Kuepukana na jambo hili kunawezekana kwani dawa ya kuponya .................. huo haijakosekana. Ni lazima kila mtu arekebishe mwenendo wake na kufanya bidii ili ............... yajayo

- *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujaza nafasi wazi. Pendekezo la jibu ni hili lifuatalo:*

Dunia ni mti mkavu wenye maajabu mengi. Linaloshangaza ni kuwa watu wake wengi hawapendi kushirikiana na wenzao. Wao husahau kwamba hawana budi kuutupilia mbali *utengano* ili waishi katika utengamano. Hawajui kwamba hali hii ni *udhaifu* kabisa! Unapowahamasisha kuhusu jambo hilo, wao hupinga na kuruka kama *mkizi* baharini. Ni kweli kuwa *ukinzani* huo ni kizuizi cha maendeleo yao binafsi ulan nchi zao. Kuepukana na jambo hili kunawezekana kwani dawa ya kuponya *uwele* huo haijakosekana. Ni lazima kila mtu arekebishe mwenendo wake na kufanya bidii ili *kuganga* yajayo.

**Sarufi (196)**

***Kazi ya 6 :*** Katika jozi hiyo, kamilisheni sentensi hizi kwa istilahi inayotakiwa:

1. ................... ni neno au fungu la maneno katika sentensi ambalo hutangulia kitenzi. Aghalabu huonyesha mtenda.

2. ........................ ni sehemu inayoundwa na kitenzi, shamirisho na chagizo.

3. ................. ni sehemu ya sentensi inayowakilisha kitu kilichofanyiwa jambo yaani mtendwa au mtendewa katika sentensi.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogo au jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kujaza sentensi. Mapendekezo ya majibu ni yafuatayo:*

1. Kiima ni neno au fungu la maneno katika sentensi ambalo hutangulia kitenzi. Aghalabu huonyesha mtenda.
2. Kiarifu ni sehemu inayoundwa na kitenzi, shamirisho na chagizo.
3. Shamirisho ni sehemu ya sentensi inayowakilisha kitu kilichofanyiwa jambo yaani mtendwa au mtendewa katika sentensi.

***Kazi ya 7 :*** Tunga sentensi 3 kwa kuzingatia maelezo yaliyomo katika kazi ya hapo juu.

- *Kazi ifanyike katika makundi madogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kutunga sentensi zenye shamirisho na chagizo.*

***Mfano:*** *Nyambere hupenda mama yake. (mama yake: shamirisho)*

*Kiima: Nyambere*

*Kiarifu: hupenda mama yake*

*Shamirisho: mama yake.*

**Matumizi la lugha (136)**

***Kazi ya 8 :*** Fanya uhakiki wa methali zifuatazo: 1. Cheche huzaa moto; 2. Chururu si ndo ndo ndo; 3. Maskini na mwanawe, tajiri na mali yake; 4. Maneno mema humtoa nyoka pangoni; 5. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na dunia.

- *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya uhakiki wa methali walizopewa. Yafuatayo ni majibu:*

**1. Cheche huzaa moto**

**Mazingira :** Moto.
**Maana:** Kitu kidogo huweza kuleta madhara makubwa.
**Matumizi:** Methali hii hutumika kuwatahadharisha wale wanaodharau mambo madogo kwani

huweza kusababisha madhara makubwa yasiyotegemewa.

**Muundo:** Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (cheche) na (huzaa moto).

**Lugha iliyotumiwa:**Ni methali inayotumia lugha ya kisasa.

2. **Chururu si ndo ndo ndo ;**

**Mazingira:** Mvujo.

**Maana :** Jambo kubwa si sawa na jambo dogo.

**Matumizi:** Methali hii inahamasisha watu ambao wana juhudi katika kufanya kazi ndani ya jamii kuwa waongeze juhudi.

**Muundo:** Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (Chururu) na (si ndo ndo ndo).

**Lugha iliyotumiwa:** Ni methali inayotumia lugha ya kisasa. Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni tanakali za sauti.

3. **Maskini na mwanawe, tajiri na mali yake ;**

**Mazingira:** Mali.

**Maana:** Methali inamaanisha kuwa matumaini ya mtu maskini ni wa toto wake lakini matumaini ya mtu tajiri ni pesa zake.

**Matumizi:** Methali hii inamkumbusha mtu yeyote (awe tajiri au fukara) kuwa kila mtu ana matumaini yake yanayotokana na maisha aliyo nayo.

**Muundo:** Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (Maskini na mwa nawe) na (tajiri na mali yake).

**Lugha iliyotumiwa:** Ni methali inayotumia lugha ya kisasa. Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni jazanda.

4. **Maneno mema humtoa nyoka pangoni ;**

**Mazingira:** Usemi.

**Maana:** Utumiaji ulani i mzuri humfanya mtu apate chochote anachohitaji.

**Matumizi:** Methali hii inamkumbusha mtu yeyote kuwa ni vizuri kuchagua maneno ya kutumia kabla ya kusema kwani uta mu wa maneno unamsaidia mtu kulifikia lengo lake.

**Muundo:** Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (Maneno mema) na (humtoa nyoka pangoni).

**Lugha iliyotumiwa:** Ni methali inayotumia lugha ya kisasa. Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni tashihisi.

5. **Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na dunia.**

**Mazingira:** Elimu.

**Maana:** Mzazi ndiye mwalimu wa kwanza wa mtoto. Ikiwa mtoto hakufunzwa na mama yake, dunia yenyewe itamfunza. Ni kusema kwamba ikiwa mtu anapuuza mashauri ya wa zazi wake, matatizo mbalimbali ambayo yatamfikia ndiyo yatakayomfunza.

**Matumizi:** Methali hii inamkumbusha mtu yeyote kuwa kupuuza ush auri wa wazazi wake huleta madhara mengi. Kwa hiyo, ni lazima kuzingatia mafunzo ya wazazi.

**Muundo:** Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (Asiyefunzwa na mamaye) na (hufunzwa na dunia).

**Lugha iliyotumiwa:** Ni methali inayotumia lugha ya kisasa. Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni jazanda.

**Kusikiliza na kuzungumza (uk. 136)**

***Kazi ya ya 8 :*** Jiunge na wanafunzi wawili kisha mtafute kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu methali mbalimbali na kuzifanyia uhakiki. Msisahau kuwasilisha matokeo ya kazi yenu kwa wenzenu.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kutafuta methali, kuzihakiki na kuziwasilisha. Kila kundi litatafuta methali zake.*

**Kuandika**

***Kazi ya 10: Tunga insha kwa kutumia methali ifuatayo: "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo."***

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ametunga insha kuhusu methali hii.*

Baadhi ya hoja:

- Kumpa mtoto malezi bora
- Kumkanya mtoto akifanya makosa
- Kumfundisha mtoto kuheshimu wengine

- Kufanya mema
- Kumshauri
- Kumpenda mtoto
- Kumfundisha adabu angali mdogo

## SOMO LA 4: UHAKIKI WA VITENDAWILI KATIKA KISWAHILI

### i. Malengo ya ujifunzaji

Kapitia kwa somo hili mwanafunzi ataweza:

- Kubainisha sehemu kuu za kitendawili;
- Kuchambua vitendawili mbalimbali.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kitabu cha mwanafunzi
- Vitabu vya fasihi
- Ubao
- Chaki,
- Redio,
- Rekodi, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu,  ula. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.

- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro ulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**iv. Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.138)***

Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kueleza picha kisha awapatie kitendawili cha kutegua ambacho ni “Mama nieleke.”

***Kazi ya 2: (uk. 138)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu cha habari na kukihusisha na picha.*

➢ Habari inahusu uhakiki wa vitendawili na picha yenyewe inaonyesha bikizee anayekaa na watoto wakitega na kutegua vitendawili.

**Kusoma na ufahamu: Vipengele muhimu vya uhakiki wa vitendawili**

***Kazi ya 3: (uk. 141)***

*Kazi hii ifanyike katika makundi madogo. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamesoma kifungu cha habari kisha wajibu maswali ya ufahamu.*

1. Vitu vitatu vinavyorejelewa na fumbo la vitendawili :
    - Vyombo vya jikoni ;
    - Matunda mbalimbali ;
    - Aina za nguo ;
    - Magonjwa ;
    - Mimea ;
    - Mashine na mitambo mbalimbali ;
    - Sehemu za mwili na kadhalika.

2. Kwa kawaida, muundo wa vitendawili unajitokeza namna hii:
   Hupitishwa baina ya pande mbili: upande unaotega kitendawili na upande unaokitegua.
   Huwa na muundo maalumu wa kuendelezwa yaani utangulizi, swali (au jaribio) na jibu.
   **Mtegaji** : Kitendawili!
   **Mteguaji** : Tega!
   **Mtegaji** : (Anatoa kitendawili chake yaani "kutega kitendawili").
   **Mfano** : Nimeanika mpunga wangu juani lakini kulipopambazuka sikuuona
   **Mteguaji** : (Anatoa jibu yaani "kutegua kitendawili").
   **Jibu** : Nyota
   Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huomba apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. Anapopewa anachotaka ndipo anakubali kutoa jibu.

3. Mbinu mbili za lugha zinazoweza kutumiwa katika vitendawili ni:
   **Tanakali za sauti:** Ni matumizi ya neno linaloiga sauti au hali fulani au namna kitendo kilivyofanyika yaani milio yake.
   **Mfano:** Drrrrrrrrrh mpaka ngambo" / [Buibui]";
   **Sitiari:** Ni tamathali ya usemi inayolinganisha moja kwa moja vitu viwili bila kutumia viunganishi

4. Tegua vitendawili hivi:
   Mchicha mzuri umechumwa na watu ulani // Dada yangu
   Anajipiga kisha analia // Jogoo
   Nimpigapo mwanangu watu hucheza // Ngoma

**Msamiati (uk. 142)**

***Kazi ya 4:*** Katika jozi, tumieni kamusi na kutafuta maana ya maneno yafuatayo: Mkungu wa ndizi, Mtemi, Buibu.

- ➢ *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaagize wanafunzi kutoa maana za maneno.*

- **Mkungu wa ndizi:** Sehemu ya mgomba yenye ndizi
- **Mtemi:** Mtawala wa kienyeji katika sehemu fulani za nchi mbalimbali

- **Buibui:** Mdudu anayetandaza utando wa kukamatia nzi na wadudu wengine

***Kazi ya 5:*** Tunga sentensi moja kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafuzi ametunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno aliyopewa.*

***Kazi ya 6:*** Kamilisha sentensi zifuatazo kama zilivyotumiwa katika habari:

1. Vitendawili hutumia mbinu mbalimbali za lugha (au .......................) ili fumbo lake liweze kuwa tamu. 2. Walakini, .....................huwa tofauti kidogo na ule unaofanyiwa habari mbalimbali zinazoingia katika kundi la masimulizi kama hadithi.

3. Vitendawili ni ...............................unaoweza kufanyiwa uhakiki.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujaza sentensi. Yafuatayo ni majibu:*

1. Vitendawili hutumia mbinu mbalimbali za lugha (au ***tamathali za usemi***) ili fumbo lake liweze kuwa tamu.
2. Walakini, ***uhakiki wa vitendawili*** huwa tofauti kidogo na ule unaofanywa kwa habari mbalimbali zinazoingia katika kundi la masimulizi kama hadithi.
3. Vitendawili ni ***utanzu wa fasihi simulizi*** unaoweza kufanyiwa uhakiki.

**Sarufi: Muundo wa sentensi**

***Kazi ya 7:*** *Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuonyesha sehemu za sentensi zifuatazo:*

1. Mchicha mzuri umechumwa na watu ulani.
2. Kuku wangu hutagia miibani.
3. Nyumba yangu haina mlango.
4. Nimpigapo mwanangu watu hucheza.
5. Yeye anasuka lakini halali chini.

**Majibu:**

1. Mchicha mzuri umechumwa na watu fulani. (Na watu fulani: Shamirisho)
   Kiima Kiarifu

2. Kuku wangu hutagia miibani. (Miibani: Chagizo)
   Kiima Kiarifu
3. Nyumba yangu haina mlango. (Mlango: Kijalizo)
   Kiima Kiarifu
4. Mkufu wangu mrefu unatembea.
   Kiima Kiarifu

5. Yeye anasuka lakini yeye halali chini. (Chini: Chagizo)
   Kiima Kiarifu Kiima Kiarifu

**Matumizi ya lugha (uk. 144)**

***Kazi ya 8:*** Fanya uhakiki wa vitendawili vifuatavyo:

1. Mifugo ya babu imetafuna ukuta / Panya ;

2. Ng'ombe wangu huchungiwa mlimani / Chawa;

- *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuhakiki vitendawili.Yafuatayo ni mapendekezo ya majibu:*

1. Mifugo ya babu imetafuna ukuta / Panya
   **Kitendawili chenyewe:** [Mifugo ya babu imetafuna ukuta]
   **Jibu:** [Panya]
   **Mazingira:** Ufugaji
   **Lugha iliyotumiwa:** Jazanda
   **Aina yake:** Kitendawili sahili
2. Ng'ombe wangu huchungiwa mlimani / Chawa
   **Kitendawili chenyewe:** [Ng'ombe wangu huchungiwa mlimani]
   **Jibu:** [Chawa]
   **Mazingira:** Ufugaji
   **Lugha iliyotumiwa:** Jazanda
   **Aina yake:** Kitendawili sahili

**Kusikiliza na kuzungumza (uk.144)**

***Kazi ya 9:*** Jiunge na wanafunzi wawili kisha mtafute kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu vitendawili mbalimbali na kuvifanyia uhakiki. Msisahau kuwasilisha matokeo ya kazi yenu kwa wenzenu.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutafuta vitendawili mtandaoni, kuvifanyia uhakiki na kuwasilisha kazi zao.* Kila kundi litatoa vitendawili vyake.

**Kuandika**

Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ametunga insha kulingana na maada ifuatayo:

"*Vitendawili huwa na umuhimu wa kuunganisha jamii*". Jadili.

**Baadhi ya hoja**

- kuwaleta watu pamoja
- kuwasiliana kati yao,
- kushirikiana,
- kuunga urafiki,
- kuwa na umoja, n.k.

## SOMO LA 5: UHAKIKI WA NAHAU NA MISEMO KATIKA KISWAHILI

### i. Malengo ya ujifunzaji

Kapitia kwa somo hili mwanafunzi ataweza:

- Kueleza muundo wa nahau na misemo katika Kiswahili
- Kuchambua nahau na misemo.

### ii. Zana na vifaa vya ufundishaji

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kitabu cha mwanafunzi
- Vitabu vya fasihi
- Ubao
- Chaki,
- Redio, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, ula. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.

- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro ulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**iv. Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.146)***

*Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutazama picha (michoro) na kuzifafanua.*

**Dokezo**:

Kwenye picha kumeandikwa "Misemo mipya" na "Kamusi ya Misemo na Nahau".

***Kazi ya 2: (uk.146)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu cha habari na kukihusisha na picha (michoro).*

**Dokezo***:*

Habari inahusu uhakiki wa nahau na misemo. Picha (michoro) nazo zinahusu « nahau na misemo ».

**Kusoma na ufahamu: Vipengele muhimu vya uhakiki wa nahau na misemo**

***Kazi ya 3 : (uk.148)***

*Kwa kupitia makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma kifungu cha habari na kijibu maswali ya ufahamu. Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa :*

1. Nahau mbili zinazorejelea vitu vinavyopatikana katika mazingira ya mitambo mbalimbali na maana yake:
    - Kutia jeki = Kuinua au kusaidia mtu

- Kupiga darubini = Kufanya uchunguzi

2. Vipengele vinavyozingatiwa katika uhakiki wa nahau na misemo kifani :
   - Muundo
   - Lugha
3. Toa maana ya nahau na misemo hii :
   - Kugonga mwamba = Kutofanikiwa
   - Kuwa na damu ya kunguni = Kuwa na bahati mbaya
   - Kuchapa maneno = Kubuni maneno ya uongo juu ya mtu
   - Kulea mtoto kwa hali na mali = Kulea mtoto vizuri uwezavyo
   - Mtu mwenye domo kaya = Mpayukaji ambaye hawezi kutunza siri

**Msamiati (uk. 149-150)**

***Kazi ya 4 :*** Kamilisha sentensi zifuatazo kama zilivyotumiwa katika habari:

1. Nahau huwa na kitenzi chake halisi (au maalumu) kinachotumiwa na kisichobadilika ilhali ................ kwani huweza kutumiwa bila kitenzi au pamoja na kitenzi chochote anachokipendelea msemaji.

2. Fulani alikubali kuambatana naye ................ upande.

- *Kazi hii ifanyike kwa jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujaza sentensi kama ifuatavyo:*

1. Nahau huwa na kitenzi chake halisi (au maalumu) kinachotumiwa na kisichobadilika ilhali **misemo haina kitenzi maalumu** kwani huweza kutumiwa bila kitenzi au pamoja na kitenzi chochote anachokipendelea msemaji.

2. Fulani alikubali kuambatana naye **shingo** upande.

***Kazi ya 5:*** Shirikiana na mwenzako na kutumia kamusi ili kutafuta maana ya maneno yafuatayo:

1. Mrija 2. Kukonda 3. Mtema kuni

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awahimize wanafunzi kutoa maana za maneno waliyopewa. Majibu ni haya yafuatayo:*

- **Mrija**: Chombo chenye uwazi ndani kinachotumika kufyonzea vitu viowevu au kutengenezea filimbi au kiko cha tumbaku; njia yoyote ya kujipatia faida ya binafsi kwa kuwanyonya wengine.
- **Kukonda**: Kuwa na wembamba wa mwili; kudhoofu
- **Mtemakuni**: Mtu akataye kuni

***Kazi ya 6:*** *Tunga sentensi moja kwa kila neno lililopo hapo juu.*

- Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ametunga sentensi sahihi.

**Sarufi : Muundo wa sentensi**

***Kazi ya 7:*** *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awahimize wanafunzi kuonyesha shamirisho, chagizo na kijalizo katika sentensi.*

1. Msichana huyu alivunja ungo.
2. Nyumba yake ni mbavu za mbwa.
3. Kagabo amekula chumvi nyingi.
4. Mama huyu aliwalea watoto wake kwa hali na mali.
5. Yeye ni mwenye domo kaya.

**Majibu**

1. Msichana huyu alivunja <u>ungo</u>.
   SH (Shamirisho)
2. Nyumba yake ni <u>mbavu za mbwa</u>.
   J (kijalizo)
3. Kagabo amekula <u>chumvi nyingi</u>.
   SH (Shamirisho)

4. Mama huyu aliwalea <u>watoto wake</u> <u>kwa hali na mali</u>.

   SH (Shamirisho)   CH( Chagizo)

5. Yeye ni <u>mwenye domo kaya</u>.

   J (Kijalizo)

**Matumizi ya lugha (uk. 151)**

***Kazi ya 8 :*** Fanya uhakiki wa nahau na misemo ifuatayo:

1. Kupiga umaridadi; 2. Amekula chumvi nyingi; 3. Kumwaga unga.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuhakiki nahau na misemo. Mapendekezo ya majibu ni haya yafuatayo:*

1. Kupiga umaridadi

   **Nahau yenyewe:** [Kupiga umaridadi]

   **Maana yake**: [Kuvaa vizuri]

   **Mazingira:** Mavazi

   **Lugha iliyotumiwa:** kuongeza ukali wa maneno

2. Amekula chumvi nyingi

   **Nahau yenyewe:** [Amekula chumvi nyingi

   **Maana yake:** [Ameishi maisha marefu]

   **Mazingira:** Chakula

   **Lugha iliyotumiwa:** Jazanda

3. Kumwaga unga

   **Nahau yenyewe:** [Kumwaga unga]

   **Maana yake:** [Kufukuzwa kazi]

   **Mazingira:** Chakula

   **Lugha iliyotumiwa:** kupunguza ukali wa maneno na jazanda

**Kusikiliza na kuzungumza (uk. 151)**

***Kazi ya 9:*** Jiunge na wanafunzi wawili kisha mtafute kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu nahau na misemo mbalimbali na kuifanyia uhakiki. Msisahau kuwasilisha matokeo ya kazi yenu kwa wenzenu.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaahimize wanafunzi kutafuta nahau na misemo, kuvihakiki na kuwasilisha kazi yao. Kila kundi litatoa nahau na misemo yake pekee.*

**Kuandika**

***Kazi ya 10***

*Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ametunga insha kulingana na mada ifuatayo: "**Nahau na misemo ni tanzu zenye umuhimu mkubwa katika jamii. Jadili."***

Baadhi ya hoja:

- Kupamba lugha
- Kupunguza ukali wa maneno
- Kuhifadhi lugha kama amali ya jamii

## SOMO LA 6: UHAKIKI WA MASHAIRI SIMULIZI KATIKA KISWAHILI

### i. Malengo ya ujifunzaji

Kapitia kwa somo hili mwanafunzi ataweza:

- Kutambua umbo la shairi simulizi katika Kiswahili
- Kuhakiki shairi

### ii. Zana na vifaa vya ufundishaji

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kitabu cha mwanafunzi
- Vitabu vya fasihi
- Ubao
- Chaki,
- Redio, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu    ulani.

**iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji**

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu,    ula. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro    ulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**iv. Majibu**

***Kazi ya 1: (uk. 165)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutazama picha na kutoa maoni.*

**Dokezo**

Kuna picha ya Mathias Mnyampala ambaye ni mshairi nchini Tanzania.

***Kazi ya 2: (uk.165)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafuzi kusoma kifungu cha habari na kukihusisha na picha.*

- Picha imaonyesha mshairi maalufu na matini inahusu uhakiki wa ushairi simulizi.

**Kusoma na ufahamu: Vipengele muhimu vya uhakiki wa mashairi simulizi ya Kiswahili**

***Kazi ya 3: (uk.167)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujibu maswli ya ufahamu.*

1. Mambo mbalimbali yanayoshughulikiwa katika kulichambua shairi kimaudhui ni:
   - Maisha ya mtunzi;
   - Kichwa cha shairi;
   - Aina ya shairi ;
   - Dhamira ;
   - Ujumbe au maadili ;
   - Falsafa au msimamo wa mshairi ;
   - Muhtasari kwa njia ya nathari.
2. Mambo hayo yanayoshughulikiwa katika kulichambua shairi kimaudhui si sawa na yale yanayoshughulikiwa katika kulichambua shairi kifani. Fani ya shairi inahusu mambo yafuatayo :
   - Wahusika (ikiwa shairi linahusisha wahusika);
   - Mtindo ;
   - Muundo au umbo la shairi ;
   - Uhuru wa mshairi.
3. Mambo yanayoshughulikiwa katika uchambuzi wa umbo la shairi ni:
   - Idadi ya beti;
   - Idadi ya mistari (au mishororo) kwa kila ubeti ;
   - Idadi ya vipande vya mstari ;
   - Idadi ya mizani kwa kila ubeti au nusu-mstari ;
   - Aina za vina (vya kati na vya mwisho) na mpangilio au urari wake ;
   - Bahari ama mstari wa mwisho. Iwapo mstari wa mwisho unaorudiarudia kwa kila ubeti unaitwa “kibwagizo” au “kiitikio”. Kama hakuna mstari wa mwisho unaorudiarudia, basi mstari huo utaitwa “kimalizio” au “kiishio”.

4. “Kuboronga sarufi” kunaleta urari wa vina au mdundo wa ushairi.

**Msamiati (uk. 168)**

***Kazi ya 4:*** Kwa kutumia kamusi, jadiliana na mwenzako juu ya maana ya maneno yafuatayo: Kuwekeza, Ubeti, Mshororo, Kina,Kuboronga.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kueleza maneno waliyopewa.Majibu ni haya yafuatayo:*

- **Kuwekeza:** Kutia kitu mahali fulani kwa ajili ya manufaa ya baadaye.
- **Ubeti:** Kifungu cha mishororo katika shairi.
- **Mshororo:** Mstari katika shairi.
- **Kina:** Silabi zenye sauti za namna moja zinazotokea baada ya kila mizani kadha hususa katikati na mwisho wa kila mstari wa ubeti wa shairi.

***Kazi ya 5:*** Tunga sentensi zenye msingi katika kuwekeza mali na kutegemea benki kwa kutumia maneno hapa juu

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ametunga sentensi kwa kuzingatia “kuwekeza mali na kutegemea benki”.*

Mfano: Serikali ya Rwanda inahimiza wananchi kuwekeza mali yao na kutegemea benki ili kuweza kuwa na maisha bora.

**Sarufi : Muundo wa sentensi**

***Kazi ya 6 : Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kuonyesha sehemu za sentensi na vipashio vya kila sehemu***

1. Mwanafunzi huyu anajizatiti na mashairi ya Kiswahili
2. Uhakiki huo huzingatia vipengele vya maudhui na fani.
3. Ubeti ni mkusanyiko wa mishororo.
4. Ushairi wa Kiswahili ni utanzu ulioanza zamani.
5. Mashairi simulizi ya Kiswahili kama tanzu nyingi za fasihi huweza kufanyiwa uhakiki.

**Majibu:**

**1.** Mwanafunzi huyu anajizatiti na mashairi ya Kiswahili

N V T U N V N

- **Mwanafuzi huyu**: Kiima
- **Anajizatiti na masahairi ya Kiswahili**: Kiarifu
- **Na mashairi ya Kiswahili**: Shamirisho

**2.** Uhakiki huo huzingatia vipengele vya maudhui na fani.

N V T N V N U N

- **Uhakiki huo**: Kiima
- **Huzingatia vipengele vya maudhui na fani** : Kiarifu
- **Vipengele vya maudhui na fani** : Shamirisho

**3.** Huo ni mkusanyiko wa mishororo.

W t N V N

- **Huo**: Kiima
- **Ni mkusanyiko wa mishororo**: Kiarifu
- **Mkusanyiko wa mishororo**: Kijalizo

**4.** Ushairi wa Kiswahili ulianza zamani.

N V N T E

- **Ushairi wa Kiswahili**: Kiima
- **Ulianza zamani**: Kiarifu
- **Zamani**: Chagizo

**5.** Mashairi simulizi ya Kiswahili kama tanzu nyingi za fasihi huweza kufanyiwa uhakiki.

N V V N U N V V N TS T N

- **Mashairi simulizi ya Kiswahili kama tanzu nyingi za fasihi** : Kiima
- **Huweza kufanyiwa uhakiki** : Kiarifu
- **Uhahihi** : Shamirisho

**Matumizi ya lugha (uk. 168-170)**

***Kazi ya 7:*** Panga maneno au vifungu vya maneno hivi katika vipengele husika vya uchambuzi wa habari:

| | | |
|---|---|---|
| Vina<br><br>Dhamira<br><br>Mishororo<br><br>Ujumbe wa mtunzi<br><br>Muhtasari wa shairi<br><br>Idadi ya beti | Fani | Maudhui |

➢ *Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kupanga maneno au vifungu katika vipengele husika. Majibu ni haya yafuatayo:*

- **Fani**: Vina, Mishororo, Idadi ya beti
- **Maudhui**: Dhamira, Ujumbe wa mtunzi, Muhtasari wa shairi

***Kazi ya 8:*** Katika jozi, fanyeni uhakiki wa habari hii. Mtakapomaliza, mmoja kati yenu awasomee wenzenu matokeo ya kazi yenu. ***(****☞Kitabu cha Mwanafunzi, uk. 170. Uchambuzi wa shairi* ***"Ujana).***

➢ *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma mfano wa uchambuzi wa shairi.*

**Kusikiliza na kuzungumza (173)**

***Kazi ya 9:*** Shirikiana na wenzako wawili na kutafuta kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu au kwa majirani zenu shairi moja la Kiswahili linalohusu "Wema." Baada ya kuandika na kusoma polepole shairi hilo, mlifanyie uhakiki kwa kuzingatia mwongozo wa uchambuzi uliotolewa.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awahimize wanafunzi kutafuta shairi linalohusu "wema", kulihakiki na kuwasilisha kazi yao (Ingekuwa vizuri kama wanafunzi wangetafuta shairi lililorekodiwa ili waweze kulisikiliza.). Kila kundi litakuwa na kazi yake pekee.*

**Kuandika**

***Kazi ya 10:*** *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kula mwanafunzi atatunga shairi la kimapokeo, lenye beti tano, linalohusu swala moja kati ya maswala mtambuka yanayoonekana katika somo la Kiswahili.* Kila mwanafunzi atatunga shairi lake.

## 2.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

### 2.5.1. Maelekezo ya ziada kwa mwalimu

Katika mada hii tumeongeza kazi mbalimbali ambazo zitamwongoza mwalimu kufanikisha kazi yake. Katika masomo yote ya mada hii tumeingiza sarufi. Kazi za sarufi nyingi zimo katika Kitabu cha Mwanafunzi lakini kurasa hazilingani sawasawa. Ndiyo maana mwalimu alielekezwa kwa namna ya kutafuta kazi hizo katika Kitabu cha Mwanafunzi. Zile ambazo hazipatikani ndani ya Kitabu cha Mwanafunzi ni zile zilizotayarishwa upya ili kukamilisha zile zilizomo katika kitabu cha mwanafunzi. Kwa hiyo, wakati wa ufundishaji mwalimu azingatie maelekezo haya.

## 2.6. TATHMINI YA MADA YA PILI

***(☞Kitabu cha Mwanafunzi: uk. 198)***

*Mwalimu ahakikishe kuwa tathmini hii itafanyika kama kazi binafsi ili kupima kiwango cha uelewa wa mwanafunzi kuhusu mada husika.*

Kujibu maswali:

a. "Uhakiki wa kazi za fasihi si jambo la hivi karibuni". Kuwepo kwa uhakiki ulianza wakati binadamu alipokuwa na uwezo wa kuzungumza na kuadhiri maoni na maisha ya wengine. Yeyote yule anayelinganisha kazi za fasihi na tajiriba yake maishani au na kazi nyingine huwa ameanza kufanya uhakiki. Uhakiki huanza katika kitendo cha kujaribu kuielewa kazi ya fasihi na kujibu maswali kama vile kwa nini, nani na vipi.

b. Mwanafunzi huhitaji kufanya mazoezi kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi kwa sababu:

- humwezesha kuielewa, kuieleza na kuifaidi kazi ipaswavyo;
- humwezesha kulinganisha kazi tofauti za fasihi;
- humwezesha kuchambua na kufafanua mifumo na picha za kisanaa zinazotumika katika kazi za fasihi ili kupevuka katika lugha;
- humwezesha kuchambua na kuweka hadharani maonyo yanayopatikana katika kazi za fasihi. Maonyo hayo tunaweza kuyatumia kwa kuwakosoa wanajamii wengine.

c. Kuchagua hadithi na kuifanyia uhakiki.

d. Kutafuta methali na kuzifanyia uhakiki.

e. Kutafuta vitendawili na kuvifanyia uhakiki.

f. Toa maana ya nahau hizi:

  - Kumwaga unga= Kufukuzwa kazi
  - Kugonga mwamba= Kutofanikiwa

g. Vipengele ambavyo hushughulikiwa katika kuhakiki shairi ni:

Uhakiki wa shairi kimaudhui:

- Maisha ya mtunzi (iwapo yanajulikana);
- Kichwa cha shairi;
- Aina (au kipera) ya shairi;
- Dhamira au wazo kuu;
- Ujumbe au fundisho au maadili au onyo;
- Falsafa au msimamo wa mshairi au mtazamo wa mshairi;
- Muhtasari (kwa nathari).

Uhakiki wa shairi kifani:

- Wahusika: Ikiwa shairi limehusisha wahusika;
- Mtindo;
- Muundo au umbo la shairi: Mambo yatakayozungumziwa hapa ni:
  - Idadi ya beti;
  - Idadi ya mistari (au mishororo) kwa kila ubeti;
  - Idadi ya vipande vya mstari;
  - Idadi ya mizani kwa kila ubeti au nusu-mstari;
  - Aina za vina (vya kati na vya mwisho) na mpangilio au urari wake;

- Kituo ama mstari wa mwisho. Iwapo mstari wa mwisho unaorudiarudia kwa kila ubeti unaitwa “kibwagizo” au “kiitikio” au “kituo bahari”. Kama hakuna mstari wa mwisho unaojirudiarudia, basi mstari huo utaitwa “kimalizio” au “kituo.”
- Uhuru wa mshairi.

h. Tunga sentensi tatu zinazohusu “amali na tamaduni na kuzalisha kwa kiwango”. Utakapomaliza, onyesha muundo wa sentensi hizo.
   - ➢ Kila mwanafunzi atatoa sentensi zake.

## 2.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI

### 2.7.1. Kazi za urekebishaji

Mapendekezo ya maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wasio na uelewa wa haraka katika masomo:

i. Uhakiki ni nini?
ii. Je, ni vipengele vipi vya uhakiki wa kazi za fasihi vinavyoshughulikiwa?
iii. Uhakiki wa methali kifani huzingatia nini?
iv. Taja sehemu kuu za sentensi.

**Majibu**

1. Uhakiki unaweza kuchukuliwa kama kitendo cha kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalumu. Ni kusema kuwa uhakiki ni uchambuzi wa ndani kabisa wa jambo lililozingatiwa na fikra za mchambuzi.
2. Vipengele vya uhakiki wa kazi za fasihi vinavyoshughulikiwa ni maudhui na fani.
3. Uhakiki wa methali kifani huzingatia muundo wake na lugha yake
4. Sehemu kuu za sentensi ni kiima na kiarifu.

### 2.7.2. Kazi za uimarishaji

1. Ni makundi gani ya wahusika yanayoshughulikiwa katika uhakiki wa hadithi.
2. Kitu gani kinachozifanya methali zitambuliwe haraka?
3. Zitaje na kuzieleza mbinu mbili za lugha zinazoweza kutumiwa katika vitendawili.
4. Vitaje vipengele vinavyozingatiwa katika uhakiki wa nahau na misemo kifani.
5. Je, ni upi umuhimu wa “kuboronga sarufi”?
6. Ni tofauti gani iliyoko baina ya shamirisho na chagizo?

**Majibu**

a. Wahusika wakuu, wahusika wadogo na wahusika wajenzi.

b. Methali hutambuliwa haraka kutokana na muundo na lugha yake.

c. Mbinu mbili za lugha zinazotumika katika vitendawili:

  - **Tanakali za sauti:** Ni matumizi ya neno linaloiga sauti au hali fulani au namna kitendo kilivyofanyika yaani milio yake.
  - **Sitiari:** Ni tamathali ya usemi inayolinganisha moja kwa moja vitu viwili bila kutumia viunganishi.

d. Vipengele vinavyozingatiwa katika uhakiki wa nahau na misemo kifani ni:

  - Muundo;
  - Lugha.

e. "Kuboronga sarufi" kunaleta urari wa vina au mdundo wa ushairi.

f. "**Shamirisho** (SH)" ni sehemu ya sentensi inayowakilisha kitu kilichofanyiwa jambo. Ni mtendwa au mtendewa katika sentensi. Ni sehemu inayojibu swali "alitenda nini?", "alitenda nani?" **ilhali** "**Chagizo (CH)**" hutueleza zaidi kuhusu kiima na shamirisho. Aghalabu, chagizo ni kielezi.

**2.7.3. Kazi za wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Mapendekezo ya maswali na majibu ya kazi hizi:

1. Je, ni mambo yapi yanayoshughulikiwa katika uchambuzi wa umbo la shairi?
2. Katika kazi yake, mshairi alipewa uhuru fulani. Uhuru huo ni upi?
3. Eleza istilahi za kishairi zifuatazo:

- Mshororo
- Kina
- Kibwagizo

4. Mara nyingi methali hujengwa na sehemu mbili. Onesha sehemu hizo katika methali zifuatazo:

- Asiyesikia la mkuu huvunjia guu.
- Tamaa mbele, mauti nyuma.
- Mtaka cha mvunguni, sharti ainame.

5. Lugha inayotumiwa katika vitendawili mara nyingi huwa ni tamathali ya usemi. Eleza ukitoa mifano.

6. Kijalizo hutofautianaje na chagizo?
7. Onyesha vipashio vinavyojenga sentensi zifuatazo:
    - Mifugo ya babu imetafuna ukuta.
    - Ng'ombe wangu huchungiwa mlimani.
    - Usiwatukane wakunga na uzazi ungalipo.

**Majibu**:

1. Katika uchambuzi wa umbo la shairi, mambo yatakayotiliwa mkazo ni haya yafuatayo:

- Idadi ya beti;
- Idadi ya mistari (au mishororo) kwa kila ubeti;
- Idadi ya vipande vya mstari;
- Idadi ya mizani kwa kila ubeti au nusu-mstari;
- Aina za vina (vya kati na vya mwisho) na mpangilio au urari wake;
- Kituo ama mstari wa mwisho. Iwapo mstari wa mwisho unaorudiarudia kwa kila ubeti unaitwa "kibwagizo" au "kiitikio." Kama hakuna mstari wa mwisho unaorudiarudia, basi mstari huo utaitwa "kimalizio" au "kituo".

2. Mshairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika kazi yake. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi lake liwe na umbo fulani. Kwa hiyo, msanii anaweza kutumia njia mbalimbali kama vile:

- "Inkisari" yaani kupunguza idadi ya silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo.
- "Mazda" yaani kuongeza idadi ya silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo.
- "Tabdila" yaani kubadilisha silabi ya mwisho ili kuwe na urari wa vina katika kipande bila kuathiri mizani.
- "Kuboronga sarufi" yaani kupangua mpangilio wa maneno ili kuleta urari wa vina au mdundo wa ushairi.
- "Tohozi" yaani kuswahilisha maneno kutoka lugha nyingine ili litamkike kwa Kiswahili.

3. Kueleza istilahi za kishairi

- Mshororo: mstari katika ushairi

- Kina: Silabi ya mwisho kwa kila kipande cha mshororo
- Kibwagizo: mstari wa mwisho wa kila ubeti unaorudiwarudiwa

4. Sehemu za methali:
   - Asiyesikia la mkuu huvunjia guu.
     1(chanzo)   2 (matokeo)
   - Tamaa mbele, mauti nyuma.
     1(chanzo)   2(matokeo)
   - Mtaka cha mvunguni, sharti ainame.
     1 (shida)   2(utatuzi wa shida)
5. Katika vitendawili kunatumika mara nyingi :
   - Jazanda : mf : Nyumba yangu haina mlango.
   - Tanakali sauti: mf: Parrrrr mpaka Maka"
6. Kijalizo ni neno lolote linalofuata kitenzi kishirikishi lakini chagizo hutueleza zaidi kuhusu kiima na shamirisho. Aghalabu, chagizo ni kielezi.
7. Vipashio vinavyojenga sentensi:

- Mifugo ya babu imetafuna ukuta.
  N V N T N
- Ng'ombe wangu huchungiwa mlimani.
  N V T E

- Usiwatukane wakunga na uzazi ungalipo.
  T N U N t

## MADA KUU YA 3: MAWASILIANO RASMI

## MADA NDOGO: UTUNGAJI WA BARUA RASMI, SIMU NA MATANGAZO

### 3.1. Uwezo upatikanao katika mada

- Kuandika barua rasmi, simu na matangazo;
- Kuchanganua sentensi katika Kiswahili.

### 3.2. Ujuzi wa awali

Katika kidato cha pili, wanafunzi walisoma masomo ambayo yanahusu utungaji wa barua kuhusu matembezi, barua za kirafiki, barua za mwaliko, simu na tangazo/ ilani. Masomo hayo yanapatikana katika sura ya 2 ambayo ni "***Utungaji***."

### 3.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake

#### 3.3.1. Kidokezo cha mada

Kwa kutangulia mada, mwalimu aulize maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua mada hii. Maswali hayo yanapaswa kuzingatia maudhui ya mada nzima. Hapa mwalimu anaweza kuuliza maswali yafuatayo:

- Ni njia zipi tuazotumia kwa kuwasiliana nchini Rwanda?
- Tunapotaka kupashana habari kwa njia ya maandishi tunatumia nini?
- Tunapotaka kupashana habari kwa njia ya mazungumzo tunatumia nini?
- Mtu anapotaka kutangaza jambo fulani anatumia njia gani?

#### 3.3.3. Maelekezo kuhusu kidokezo cha mada

- Mwalimu atoe mwongozo wa kutoa majibu kwa kazi.
- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia kazi nyingine zilizotayarishwa au masomo ya mada nzima.

### 3.4. Orodha ya masomo

| | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | Dhana ya barua rasmi na utungaji wake | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya barua rasmi na lengo lake na Kubainisha sehemu kuu za barua rasmi<br><br>**Stadi :** Kujadili dhana ya barua rasmi na lengo lake na kutunga barua rasmi kwa kuzingatia sehemu muhimu zake<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuheshimu kanuni za utungaji na kuonyesha ari ya kuboresha mawasiliano kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa | 18 |
| 2 | Dhana ya simu | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya simu na mwongozo wa uandishi wake<br><br>**Stadi**: Kujadili dhana ya simu na kutunga mfano wa simu<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kufurahia mawasiliano na wengine kwa matumizi ya vifaa vya kiteknolojia | 4 |
| 3 | Uandishi wa matangazo | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya tangazo na uandishi wake<br><br>**Stadi**: Kuandika matangazo mbalimbali kwa kuzingatia mwongozo na kuandika tangazo kwa usahihi<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuimarisha tabia | 8 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | ya kuwasiliana kwa njia ya maandishi sahihi | |
| | Sarufi: Uchanganuzi wa sentensi | **Maarifa na ufahamu:** Kuonyesha njia tofauti za uchanganuzi wa sentensi ya Kiswahili<br><br>**Stadi :** Kuchanganua sentensi kupitia njia ya matawi, njia ya mishale na njia ya jedwali<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kufurahia matumizi sahihi ya Kiswahili kwa kuzingatia uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili | |
| **Tathmini ya mada** | | | **2** |
| **Vipindi vyote vya mada ya kwanza** | | | **32** |

**Tnbh:** Sarufi huja kila wakati ndani ya kila somo baada ya kufundisha msamiati.

☞ **Kila somo huwa na kazi za aina sita :**

- Kazi zinazohusu kusoma na ufahamu
- Kazi zinazohusu msamiati
- Kazi za sarufi
- Kazi zinazolingana na matumizi ya lugha
- Kazi za kusikiliza na kuzungumza
- Kazi za kuandika

## SOMO LA 1: DHANA YA BARUA RASMI NA UTUNGAJI WAKE

### i. Malengo ya ujifunzaji

Katika somo hili, mwanafunzi ataweza:

- Kueleza dhana ya barua rasmi na lengo lake
- Kubainisha sehemu kuu za barua rasmi
- Kutunga barua rasmi kwa kuzingatia sehemu muhimu zake

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Barua,
- Bahasha,
- Ubao,
- Chaki,
- n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.

- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

iv. **Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.199)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuchunguza picha na kuieleza*

***Dokezo****:*

Kinachoonekana ni:

- Mkono ambao unachukua bahasha;

- Kwenye bahasha kumeandikwa jina "Kalisa."

***Kazi ya 2: (uk. 199)***

*Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu na kukihusisha na picha.*

**Dokezo**:

Picha inaonyesha picha ya bahasha na kifungu cha habari kinazungumzia kuhusu jinsi ya kuandika barua hasa ya kikazi.

**Kusoma na ufahamu: Barua rasmi au ya kikazi**

**Kazi ya 3: (uk.203)**

*Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu upya na kujibu maswali ya ufahamu.*

**Majibu:**

1. Barua au waraka ni maandishi kwa mtindo wa kinathari yanayopelekwa kwa mtu kutoka mtu mwingine kwa madhumuni ya:

- Kuarifu kwa haraka;
- Kuomba kitu kama vile kazi, ruhusa,...;
- Kuagiza bidhaa na kadhalika.

2. Sababu tatu zinazoweza kumlazimisha mtu kuandika barua rasmi ni kama vile kuomba kazi, kutoa ripoti, kuagiza bidhaa, kuandikia meneja wa gazeti na kadhalika.

3. “Barua ni risala au mjumbe mwepesi anayemwakilisha mtungaji wake kwa mtu mwingine na kuwasilisha taarifa yake kwa mtu huyo”. Anapoipokea mtu aliyetungiwa barua, anamwona mwandishi katika picha ya barua hiyo. Mawazo yanayopatikana ndani yake ni yale ya mwandishi. Ni kusema kuwa barua yenyewe inamwakilisha mwandishi wake na kumpelekea mwandikiwa ujumbe kutoka kwa mwandishi.

4. “Barua ni nusu ya kuonana.” Unapoipokea barua kutoka kwa mtu fulani, ni kama kumwona mtu huyo lakini si ana kwa ana bali kuna kitu yaani barua kinachomwakilisha. Ni kusema kuwa mwandikiwa amemwona mwandishi katika barua yake au amemwona kwa nusu tu.

5. Kwa maoni yangu, barua huandikwa kwa mtindo wa nathari.

**Msamiati *(uk.204)***

***Kazi ya 4 :*** Shirikiana na mwenzako na kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu ili kujua maana ya maneno yafuatayo:

1. Risala 2. Saini 3. Kuadhimisha 4. Nakala 5. Nadra

➢ *Katika makundi madogomadogo, mwalimu awahimize wanafunzi kutoa maana za maneno. Yafuatayo ni mapendekezo ya majibu :*

- **Risala**: Taarifa inayopelekwa kwa mtu au watu fulani aghalabu inayoeleza haja inayotakiwa
- **Kuadhimisha**: Kusherehekea jambo au siku kwa kuitukuza au kuisifu
- **Nadra**: Hali ya kutopatikana mara kwa mara
- **Saini**: Sahihi; maandishi ya jina la mtu ya kuthibitisha au kuidhinisha kutendeka au kupatikana kwa kitu au jambo fulani kwa kuandika jina lako
- **Nakala**: Kitu chochote kilichonukuliwa kama vile maandishi, mchoro, picha,...

***Kazi ya 5:*** Tunga sentensi zinazohusu Sikukuu ya Mashujaa nchini Rwanda kwa kutumia maneno ya hapo juu.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi ametunga sentensi sahihi kulingana na Sikukuu ya Mashujaa nchini Rwanda, kwa kutumia maneno aliyopewa katika kazi ya 4.*

**Sarufi: Uchanganuzi wa sentensi (219-222)**

***Kazi ya 6****: Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kufanya marudio kuhusu aina za sentensi na miundi yake.*

- **Aina za sentensi**

- Sentensi sahili (SS)
- Sentensi tegemezi (ST)
- Sentensi changamano (SCH)
- Sentensi ambatano (SA)
- Sentensi shurutia (SSH)

- **Miundo ya sentensi**

- Sentensi huundwa na sehemu kuu mbili: Kiima/Kikundi nomimo (K/KN) na Kiarifu/kiarifa/Prediketa/Kikundi kitenzi (A/P/KT).
- Kila sehemu ya sentensi huujengwa na vipashio mbalimbali. Vipashio hivyo ni :
  - Nonimo (N)
  - Kivumishi (V)
  - Kiwakilishi (W)
  - Kitenzi:
  - Kitenzi kikuu (T)
  - Kitenzi kisaidizi (TS)
  - Kitenzi kishirikishi (t)

- Kielezi (E)
- Kiunganishi (U)
- Kihusishi (HU)
- Kihisishi (H)

***Kazi ya 7: (☞Kitabu cha Mwanafunzi: Kazi ya 1: uk.219)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo.Mwalimu awaagize wanafunzi kuchunguza picha na kuieleza.*

**Dokezo***:*

Kinachoonekana ni mchoro wa sentensi ya Kiswahili ambayo imefanyiwa uchanganuzi.

***Kazi ya 8:*** Soma maelezo yafuatayo kisha yahusishe na picha ya hapo juu.

- *Mwalimu awaagize wanafunzi kusoma maelezo kuhusu uchanganuzi wa sentensi na kuyahusisha na picha ya kazi ya 1.*

**Dokezo**:

Picha inaonyesha mchoro wa sentensi ya Kiswahili ambayo imefanyiwa uchanganuzi. Na kifungu cha habari kinazungumzia uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili.

***Kazi ya 9:*** Soma mifano ya sentensi ifuatayo:

1. UKIMWI huo unaangamiza watu wengi.

2. Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini Sifa hataki kwenda shuleni.

Taja aina za sentensi hizo.

- *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaagize wanafunzi kwa kuchunguza sentensi na kuziainisha. Yafuatayo ni majibu:*

1. UKIMWI huo unaaangamiza watu wengi. (Sentensi sahili: SS)

2. Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini yeye hataki kwenda shuleni. (Sentensi changamano: SCH)

***Kazi ya 10:*** Katika jozi, changanueni sentensi hizo kwa njia ya visanduku au jedwali.

- *Kazi hii ifanyike kwa jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuchanganua sentensi kwa njia ya visanduku na kulinganisha maelezo na kazi ya 9 hapa juu. Mapendekezo ya majibu ni haya yafuatayo:*

1. UKIMWI huo unaangamiza watu wengi

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| SS | | | | |
| KN | | KT | | |
| N | V | T | KN | |
| | | | N | V |
| UKIMWI | huo | unaangamiza | watu | wengi |

2. Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini yeye hataki kwenda shuleni.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| SA | | | | | | | | |
| S1 | | | | U | S2 | | | |
| KN | | KT | | | KN | KT | | |
| N | V | T | N | | W | TS | T | E |
| Wanafunzi | wote | wameshinda | mtihani | lakini | yeye | kataki | kwenda | shuleni |

**Matumizi ya lugha (uk. 204)**

***Kazi ya 11:*** Waambie wenzako sehemu kuu zinazozingatiwa katika utungaji wa barua rasmi.

- *Kazi hii ifanyike kwa jozi. Mwalimu awelekeze wanafunzi kwa kueleza, kwa njia ya majadiliano, sehemu kuu za barua rasmi.* Sehemu kuu za barua rasmi ni:

- Kumbukumbu namba (ikiwa unayo)
- Anwani ya mwandishi na tarehe
- Anwani ya mwandikiwa
- (Kupitia kwa na anwani ya mwenye kusaini na kutia muhuri)
- Salaam
- Yahusu / Kuhusu / Yah. / Kuh.
- Mwanzo au utangulizi
- Ujumbe
- Mwisho au hitimisho

**Kusiliza na kuzungumza (uk. 206)**

***Kazi ya 12:*** "Umefuzu katika mtihani wa kitaifa, elimu ya sekondari, mchepuo wa Sheria. Mwandikie Waziri wa Sheria ukimwomba kazi ya kuwa msajili wa mahakama ya Rutsiro". Iga muundo wa hapo juu.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa lika mwanafunzi ameandika barua rasmi kwa kuiga mfano wa barua kwenye sehemu ya "F."*

***Kazi ya 13:*** Katika jozi, mwanafunzi mmoja atunge barua rasmi kuhusu "Kufunga shule" kisha mwenzake atoe jibu kulingana na ombi husika.

- *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu ahakikishe kuwa, katika jozi, mwanafunzi mmoja ametunga barua rasmi kuhusu "kufunga shule" na mwenzake amejibu barua hiyo kulingana na ombi husika. Baada ya kumaliza kila mmoja atasomea barua darasa zima.*

**Mfano:**

KUMB: GA/103/03/2016

Kijiji cha Gihaya
Kata ya Mubali
Tarafa ya Rubero
Wilaya ya Giti
Namba ya Simu: 0788521366
SLP 25 Rwamagana
JIMBO LA MASHARIKI
25/06/2022

Mkuu wa Shule ya Giti
SLP 48 Rwamagana
JIMBO LA MASHARIKI

Mkuu wa Shule,

**YAH: Kufunga shule**

Kichwa cha hapo juu chahusika.

Rejea barua yangu ya tarehe 20/0/2022 iliyokuwa ikiwataka kufunga shule kwa sababu ya ugonjwa wa kipindupindu uliojitokeza ghafla katika wilaya yetu.

Ni matumaini yangu kwamba barua hiyo uliipokea na hivyo, utekelezaji wake usingechelewa.

Ninapenda kukutumia barua hii tena kukuomba kufunga shule. Jambo hili ni la kuzingatia kwani likiendelea linaweza kusababisha madhara makubwa kwa wanafunzi na umma mzima.

Asante.

Wako mtiifu,

(Saini)

Mkuu wa Wilaya

**Kuandika (uk. 206)**

***Kazi ya 14:*** Umepata habari kwamba rafiki yako alifanya ajali ya barabara na kulazwa katika Hospitali kuu ya CHUK. Mwandikie barua mkurugenzi wako wa shule ukimwombea msaada rafiki yako.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi ametunga barua rasmi kulingana na maelekezo.*

## SOMO LA 2: DHANA YA SIMU

### i. Malengo ya ujifunzaji

Katika somo hili, mwanafunzi ataweza:

- Kueleza dhana ya simu na mwongozo wa uandishi wake
- Kujadili dhana ya simu
- Kutunga mfano wa simu

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Simu ya mkononi,
- Simu yenye waya,
- Ubao,
- Chaki,
- Michoro ya simu tofauti, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

**iii. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji**

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**iv. Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.207)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kutazama picha na kuzieleza.*

*Dokezo:*

Kenye picha kuna simu ya kawaida ya waya na simu ya mkononi.

***Kazi ya 2: (uk.20)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kotoa umuhimu wa vifaa vinavyoonekane kwenye picha.*

**Dokezo**:

Hizi ni simu. Simu ni vyombo vinavyotumiwa katika kuwasiliana kwa njia mbalimbali kama vile kupashana habari, kutuma ujumbe wa maandiko na kadhalika.

**Kusoma na ufahamu: Simu**

***Kazi ya 3:***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu na kujibu maswali ya ufahamu.*

**Majibu***:*

1. Simu ni chombo kinachotumia umeme na kuwawezesha watu wawili kuwasiliana. Chombo hicho hupelekea na kupokelea mawimbi ya sauti baina ya mtu na mtu papo kwa papo. Simu huweza pia kuwa ujumbe au habari zinazopokelewa kwa kutumia chombo hicho au kwa kutumia mtambo mwingine (kama vile faksi, teleksi,...) na kuandikwa baadaye.
2. Simu ya maneno huwa fupi sana kwa sababu mtu hana fursa ya kueleza mengi au kuzungumza moja kwa moja na yule anayempelekea taarifa.
3. Sifa za simu ya maneno ni:
   - Kuwa fupi sana;
   - Kwenda haraka zaidi kuliko barua za kawaida;
   - Kuwa na maneno machache;
   - Kuandikwa kwa kutumia herufi kubwa.
4. "Simu ni mjumbe mwepesi sana". Kwa kusafirishwa na mitambo mbalimbali, simu ya maneno humfikia mtu baada ya muda mfupi sana (sekunde chache sana).

**Msamiati (uk. 210)**

***Kazi ya 4:*** *Shirikiana na mwanafunzi mwenzako kwa kutafuta maana ya maneno yafuatayo:*

1. Waya 2. Umeme 3. Wimbi

- *Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutoa maana za maneno waliyopewa. Mfano:*

- **Waya**: Uzi wa madini ya chuma unaotumiwa katika kusafirisha umeme, mawimbi ya sauti na kadhalika
- **Umeme**: Miali ya moto inayoonekana kabla ya radi; nguvu zinazotoa cheche
- **Wimbi**: Mtutumko wa sauti au nuru zinazosafiri hewani au wa maji baharini au ziwani...

***Kazi ya 5 :*** Katika jozi hiyo, tungeni aya moja kuhusu mawasiliano kwa kutumia maneno ya hapo juu.

- *Katika jozi, mwalimu awaagize wanafunzi kutunga aya moja kuhusu mawasiliano kwa kutumia maneno waliyopewa.*

**Sarufi: Uchanganuzi wa sentenzi za Kiswahili (222)**

***Kazi ya 6 :*** *Katita jozi, mwalimu awaagize wanafunzi kufanya marudio kuhusu uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya visanduku kisha wawasilishe matokeo ya marudio hayo darasani.*

***Kazi ya 7:*** Katika jozi, changanueni sentensi hizi kwa njia ya mishale au mistari.

1. UKIMWI huo unaangamiza watu wengi.

2. Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini Sifa hataki kwenda shuleni.

- *Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuchanganua sentensi kwa njia ya mishale au mistari. Mapendekezo ya majibu ni haya yafuatayo:*

1. UKIMWI huo unaangamiza watu wengi.

SS → KN + KT

KN → N+V

N → UKIMWI

V → huo

KT → T+KN

T → unaangamiza

KN → N+V

N → watu

V → wengi

2. Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini yeye hataki kwenda shuleni.

SA → S1 +U+ S2

S1 → KN+KT

KN → N+V

N → Wanafunzi

V → wote

KT → T+N

T → wameshinda

N → mtihani

U → lakini

S2 → KN+KT

KN → N

W → Yeye

KT → Ts+T+ E

Ts → hataki

T → kwenda

E → shuleni

**Matumizi ya lugha (uk. 211-212)**

***Kazi ya 8: (☞Kitabu cha Mwanafunzi: Kazi ya 12)***

*Kwa mazungungumzo katika jozi, mwalimu awaagize wanafunzi kuhusisha picha ya mnara na somo lenyewe.*

**Dokezo**: Huu ni mnara wa mawasiliano. Mitambo mbalimbali ambayo inachangia katika kurahisisha mawasiliano inafungwa kwenye mnara huu. Na simu ya maneno inasafirishwa kupitia mitambo hiyo.

***Kazi ya 9:*** Fuata muundo huu wa sentensi na kujaza jedwali lifuatalo kwa kuzingatia sifa za simu ya maneno zilizotajwa katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| Simu ya maneno huwa fupi sana | huwa fupi sana |
| | .......................... |
| | .......................... |
| | ......................... |

- *Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujaza jedwali. Yafuatayo ni majibu:*

| | |
|---|---|
| Simu ya maneno | Huwa fupi sana |
| | Huenda haraka zaidi kuliko barua za kawaida |
| | Huwa na maneno machache |
| | Huandikwa kwa kutumia herufi kubwa |

**Kusikiliza na kuzungumza (212)**

***Kazi ya 10:*** Katika jozi, mwanafunzi mmoja ampelekee mwenzake ujumbe wa simu kwa niaba ya kiongozi wake na mwingine atoe jibu.

- *Katika jozi, mwalimu awaagize wanafunzi kuandikiana simu, kisha wawasilishe kazi zao. Kila kundi na kila mwanafunzi atatuna simu yake.*

**Kuandika (uk. 212)**

***Kazi ya 11:*** Mtungie simu ya maneno ndugu yako anayeishi mjini Kigali ili kumwarifu aje kukupokea kwenye Uwanja wa Ndege wa Kanombe kesho asubuhi saa mbili.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunze ametunga simu ya maneno kwa kufuatana na maagizo.*

## SOMO LA 3: UANDISHI WA MATANGAZO

### i. Malengo ya ujifunzaji

Katika somo hili, mwanafunzi ataweza:

- Kueleza dhana ya tangazo na uandishi wake
- Kuandika matangazo mbalimbali kwa kuzingatia mwongozo na kwa usahihi

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti,
- Mabango,
- Ubao,
- Chaki,
- Redio, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.

- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**iv. Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.213)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutazama picha na kueleza wanachoona kwenye picha hiyo.*

***Dokezo***

Kwenye picha kumeandikwa tangazo hili la Polisi "Kutumia njia za pembeni ni kuvunja sheria, kuharibu barabara na mazingira. AMRI: Fuata barabara kuu"

***Kazi ya 2: (uk.213)***

*Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu cha habari na kukihusisha na picha.*

***Dokezo***

Picha inaonyesha tangazo la polisi na kifungu cha habari chetu kinazungumzia utungaji wa matangazo.

**Kusoma na ufahamu: Ni rahisi kutunga matangazo**

***Kazi ya 3: (uk.215)***

*Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu upya na kujibu maswali ya ufahamu.*

**Majibu**

1. Tangazo ni maandishi ambayo yanatoa na kusambaza habari juu ya jambo fulani.

2. "Lengo la matangazo huwa na uhusiano wa karibu na jambo linalozungumziwa". Matangazo ni maandishi ambayo yanatoa na kusambaza habari juu ya jambo fulani na huainishwa

kufuatana na shughuli au jambo linalozungumziwa. Kwa hiyo, tutakuwa na matangazo ya serikali, matangazo ya biashara, matangazo ya kazi, matangazo ya kifo na kadhalika.

3. Matangazo huandikwa kwa muhtasari kwa sababu hutumia maneno machache ili kutomchosha mlengwa.

4. Katika matangazo ya biashara, lugha ya mvuto hutumiwa kwa sababu huwa nyepesi kukumbukwa na huwa inaeleweka kirahisi.

5. Mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji wa matangazo:

- Kuandika kichwa cha tangazo;
- Kutaja mtu au shirika linalotangaza;
- Kutaja watu ambao wanalengwa;
- Kuonyesha kiini (au wazo kuu) cha tangazo;
- Kuandika masharti ya tangazo;
- Kuonyesha anwani ya mtoa tangazo;
- Kujulisha jina, wadhifa na njia za mawasiliano (namba ya simu, faksi, tovuti, barua pepe) za mtu yule anayewasilisha tangazo.

***Kazi ya 4: (☞Kitabu cha Mwanafunzi : Kazi ya 6: uk.216)***

*Kazi hii ifanyike katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujadiliana kuhusu kazi hiyo.*

**Jibu:** Mtu kama huyu huonekana kijijini kwetu. Ni mtu anayeupelekea raia ujumbe wa viongozi wa ngazi mbalimbali hasa ujumbe kuhusu utekelezaji wa sera za serikali kama vile kazi za harambee yaani "Umuganda", kupiga kura na kadhalika. Ni kiunganishi kati ya ngazi za uongozi na raia.

**Msamiati (uk. 216)**

***Kazi ya 5:*** Jiunge na mwanafunzi mwingine na kutafuta maana za maneno yafuatayo: Mkataba, Tukio, Mtaji,Maarufu, Wadhifa.

- *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutoa maana za maneno. Mfano:*

- **Mkataba**: Makubaliano yanayofikiwa kwa kuandikiana baina ya watu au vikundi viwili au zaidi ili kufanya jambo au kazi fulani.
- **Tukio**: Jambo lililofanywa au lililotokea.
- **Mtaji**: Mali inayotumika kuanzishia biashara au kazi nyingine yoyote ya kuzalisha mali.
- **Maarufu**: Kinachojulikana mahali kote.
- **Wadhifa** (**nyadhifa**): Cheo ambacho mtu anakuwa nacho kazini; madaraka.

**Kazi ya 6 :** Tunga sentensi fupi kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikise kuwa kila mwanafunzi ametunga sentensi kwa kutumia maneno aliyopewa.*

***Kazi ya 7 :*** Kwa kuzingatia dhamira ya maridhiano, tunga setensi kwa kutumia maneno yafuatayo yanayopatikana katika kifungu cha habari:

1. Kusambaza.....................................

2. Kuwasiliana.......................................................

3. Kuepukana.........................................

- *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaagize wanafunzi kujaza sentensi hizi. Kila kundi litatunga sentensi zake.*

**Sarufi: Uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili (uk.222)**

***Kazi ya 8 :*** *Katita jozi, mwalimu awaagize wanafunzi kufanya marudio kuhusu uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya mishale au mistari. Kila kundi litafanya marudio peke yake.*


***Kazi ya 9:*** Katika jozi, changanueni sentensi hizi kwa njia ya matawi.

1. UKIMWI huo unaangamiza watu wengi.


2. Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini Sifa hataki kwenda shuleni.

➢ *Katika jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuchanganua sentensi hizi kwa njia ya matawi. Yafuatayo ni majibu:*

1. UKIMWI huo unaangamiza watu wengi.




2. Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini yeye hataki kwenda shuleni.



**Matumizi ya lugha** ***(uk. 217)***

***Kazi ya 10:*** *Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaagize wanafunzi kwa kujaza jedwali.Yafuatayo ni majibu :*

| **Lengo la tangazo** | **Mambo ya kuzingatia katika utungaji wa matangazo** |
|---|---|
| Tatangazo yanatoa na kusambaza habari juu ya jambo fulani. | - Kuandika kichwa cha tangazo;<br>- Kutaja mtu au shirika linalotangaza;<br>- Kutaja watu ambao wanalengwa;<br>- Kuonyesha kiini (au wazo kuu) cha tangazo;<br>- Kuandika masharti ya tangazo;<br>- Kuonyesha anwani ya mtoa tangazo;<br>- Kujulisha jina, wadhifa na njia za mawasiliano (namba ya simu, faksi, tovuti, barua pepe) za mtu yule anayewasilisha tangazo. |

**Kusikiliza na kuzungumza**

***Kazi ya 11: (☞Kitabu cha Mwanafunzi: kazi ya 12:uk.217)***

*Katikaa makundi madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kusoma tangazo na kujadiliana. Kila kundi litatoa hoja zake.*

**Kuandika (uk. 219)**

***Kazi ya 12 :*** Kama Meneja Mkuu wa kampuni ya BRALIRWA, tayarisha tangazo la kuwataka wateja wapende na watumie sana kinywaji cha “Sprite”.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameweza kutunga tangazo kulingana na maagizo. Kila mwanafunzi atatunga tangazo la kibiashara.*

## 3.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

### 3.5.1. Maelekezo ya ziada kwa mwalimu

Katika mada hii tumeongeza kazi mbalimbali ambazo zitamwongoza mwalimu kufanikisha kazi yake. Katika masomo yote ya mada hii tumeingiza sarufi. Kazi za sarufi nyingi zimo katika Kitabu cha Mwanafunzi lakini kurasa hazilingani sawasawa. Ndiyo maana mwalimu alielekezwa kwa namna ya kutafuta kazi hizo katika Kitabu cha Mwanafunzi. Zile ambazo hazipatikani ndani ya Kitabu cha Mwanafunzi ni zile zilizotayarishwa upya ili kukamilisha zile zilizomo katika kitabu cha mwanafunzi.

### MASWALI YA NYONGEZA KWA TATHMINI YA MADA YA TATU

*Mwalimu ahakikishe kuwa tathmini hii itafanyika kama kazi binafsi ili kupima kiwango cha uelewa wa mwanafunzi kuhusu mada husika.*

1. Barua ni nini?
2. Zitaje sababu tatu zinazoweza kumlazimisha mtu kuandika barua rasmi.
3. “Barua ni nusu ya kuonana”. Eleza kinagaubaga.
4. Simu ni nini?
5. Zitaje sifa za simu ya maneno unazojua.
6. Tangazo ni nini?
7. Kwa nini katika matangazo ya biashara, lugha ya mvuto hutumiwa?
8. “Umefuzu katika mtihani wa kitaifa, elimu ya sekondari, mchepuo wa Sheria. Mwandikie Waziri wa Sheria ukimwomba kazi ya kuwa msajili wa mahakama ya Rutsiro”.

**Majibu**

1. Barua au waraka ni maandishi kwa mtindo wa kinathari yanayopelekwa kwa mtu kutoka mtu mwingine kwa madhumuni ya:
    - Kuarifu kwa haraka;
    - Kuomba kitu kama vile kazi, ruhusa,...;
    - Kuagiza bidhaa na kadhalika.

2. Sababu tatu zinazoweza kumlazimisha mtu kuandika barua rasmi ni kama vile kuomba kazi, kutoa ripoti, kuagiza bidhaa, kuandikia meneja wa gazeti na kadhalika.

3. "Barua ni nusu ya kuonana." Unapoipokea barua kutoka kwa mtu fulani, ni kama kumwona mtu huyo lakini si ana kwa ana bali kuna kitu yaani barua kinachomwakilisha. Ni kusema kuwa mwandikiwa amemwona mwandishi katika barua yake au amemwona kwa nusu tu.

4. Simu ni chombo kinachotumia umeme na kuwawezesha watu wawili kuwasiliana. Chombo hicho hupelekea na kupokelea mawimbi ya sauti baina ya mtu na mtu papo kwa papo. Simu huweza pia kuwa ujumbe au habari zinazopokelewa kwa kutumia chombo hicho au kwa kutumia mtambo mwingine (kama vile faksi, teleksi,...) na kuandikwa baadaye.

5. Sifa za simu ya maneno ni:
   - Kuwa fupi sana;
   - Kwenda haraka zaidi kuliko barua za kawaida;
   - Kuwa na maneno machache;
   - Kuandikwa kwa kutumia herufi kubwa.

6. Tangazo ni maandishi ambayo yanatoa na kusambaza habari juu ya jambo fulani.
7. Katika matangazo ya biashara, lugha ya mvuto hutumiwa kwa sababu huwa nyepesi kukumbukwa na huwa inaeleweka kirahisi.
8. Mwanafunzi ataandika barua kulingana na taratibu za utungaji wa barua rasmi.

## 3.5.TATHMINI YA MADA YA TATU

**(☞Kitabu cha Mwanafunzi : uk.227)**

*Mwalimu ahakikishe kuwa tathmini hii itafanyika kama kazi binafsi ili kupima kiwango cha uelewa wa mwanafunzi kuhusu mada husika.*

1. Mwandikie barua Mkuu wa Polisi ili kumwomba kutatua tatizo ulilonalo la ukosefu wa vitambulisho vyako.

2. Tuma simu ya maneno kwa mwenzako ili kumwomba auze nyumba yako.
3. Tunga tangazo la biashara na kulisomea wenzako.
4. Tunga sentensi moja kwa kuzingatia maelezo yafuatayo:
   a) Sentensi sahili
   b) Sentensi shurutia (tungo yakinishi)
   c) Sentensi shurutia (tungo kanushi )
   d) Sentensi changamano
   e) Sentensi ambatano

**5.** Changanua sentensi hii kwa njia ya visanduku na njia ya matawi.

Mtoto huyu anaandika barua yake lakini Kalisa amekwenda kucheza kandanda.

**Majibu**

2. Kila mwanafunzi atatunga barua rasmi.

3. Kila mwanafunzi atatunga simu ya maneno.

4. Kila mwanafunzi atatunga tangazo la kibiahara.

5.

b) Mwanafunzi atatunga sentensi sahili.

c) Mwanafunzi atatunga sentensi shurutia (tungo yakinishi)

d) Mwanafunzi atatunga sentensi shurutia (tungo kanushi)

e) Mwanafunzi atatunga sentensi changamano

f) Mwanafunzi atatunga sentensi ambatano

5.


a) Kuchanganua kwa njia ya visanduku

Mtoto huyu anaandika barua yake lakini Kalisa amekwenda kucheza kandanda.

| SA | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S1 | | | | | U | S2 | | | |
| KN | | KT | | | | KN | KT | | |
| N | V | T | N | V | | N | TS | T | N |
| Mtoto | huyu | anaandika | barua | yake | lakini | Kalisa | amekwenda | kucheza | kandanda |

b) Kuchanganua kwa njia ya matawi

Mtoto huyu anaandika barua yake lakini Kalisa amekwenda kucheza kandanda.



### 3.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI

### 3.7.1. Kazi za urekebishaji

Mapendekezo ya maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wenye uelewa usio wa haraka.

1. Barua ni nini?
2. Taja aina za barua unazozifahamu.
3. Taja sehemu kuu za barua rasmi.
4. Simu ya maneno hitwa tena……..
5. Ni njia gani tunazotumia kwa kuchanganua sentensi?

**Majibu**

1. Barua au waraka ni maandishi kwa mtindo wa kinathari yanayopelekwa kwa mtu kutoka mtu mwingine kwa madhumuni ya:
   - Kuarifu kwa haraka;
   - Kuomba kitu kama vile kazi, ruhusa,...;
   - Kuagiza bidhaa na kadhalika.
2. Kuna barua za kirafiki, barua za mwaliko, barua za magazetini na barua rasmi.
3. Sehemu za barua rasmi ni:

   a) Kumbukumbu namba (ikiwa unayo)
   b) Anwani ya mwandishi na tarehe
   c) Anwani ya mwandikiwa
   d) Kupitia kwa na anwani ya mwenye kusaini na kutia muhuri
   e) Salaam
   f) Yahusu / Kuhusu / Yah. / Kuh.
   g) Mwanzo au utangulizi
   h) Ujumbe
   i) Mwisho au hitimisho
   j) Saini ya mwandishi na jina lake
   k) Nakala kwa
4. Telegramu

5. Kuna njia ya visanduku, njia ya mishale na njia ya matawi.

### 3.7.2. Kazi za uimarishaji

1. Barua za kirafiki hutofautianaje na barua rasmi?
2. Kwa kuonyesha umuhimu wa barua waswahili husema nini?
3. Eleza mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji wa matangazo.
4. Barua yenyewe inamwakilisha mwandishi wake kwa mwandikiwa. Jadili.
5. Unaelewa nini kuhusu upambanuzi au uchanganuzi wa sentensi?
6. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi.
7. Tunga barua rasmi huku ukiomba kazi ya ualimu wa Kiswahili.

**Majibu**


1. Barua ya kirafiki ni ile unayoandikia rafiki yako au mzazi wako ambamo unaweza kuandika mambo mbalimbali kama vile porojo, kifo cha mwenzako aliyeangamizwa na ugonjwa mkali kama UKIMWI, watu waliokutukana na kadhalika ilhali barua rasmi au ya kikazi ni barua inayoandikiwa viongozi ili kuomba kazi, kutoa ripoti, kuagiza bidhaa, katika shughuli za kiserikali au kichama au kidini na kadhalika.
2. Waswahili kusema kwamba barua ni nusu ya kuonana.
3. Mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji wa matangazo:
   - Kuandika kichwa cha tangazo;
   - Kutaja mtu au shirika linalotangaza;
   - Kutaja watu ambao wanalengwa;
   - Kuonyesha kiini (au wazo kuu) cha tangazo;
   - Kuandika masharti ya tangazo;
   - Kuonyesha anwani ya mtoa tangazo;

- Kujulisha jina, wadhifa na njia za mawasiliano (namba ya simu, faksi, tovuti, barua pepe) za mtu yule anayewasilisha tangazo.

4. Anapoipokea mtu aliyetungiwa barua, anamwona mwandishi katika picha ya barua hiyo. Mawazo yanayopatikasna ndani yake ni yale ya mwandishi. Ni kusema kuwa barua yenyewe inamwakilisha mwandishi wake na kumpelekea mwandikiwa ujumbe kutoka kwa mwandishi.

5. Uchanganuzi au upambanuzi wa sentensi ni ufafanuzi wa sentensi unaofanywa katika kujifunza lugha mbalimbali na ambao humwezesha mwanafunzi kuchanganua vipashio vyote vinavyoiunda sentensi kuanzia kwa neno.

6. Mvua nyingi ilinyesha jana usiku.




7. Mwanafunzi atatunga barua huku akizingatia taratibu za utungaji wa barua rasmi.

### 3.7.3. Kazi kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Mapendekezo ya maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wenye uelewa wa haraka.

1. Tangazo na barua ni njia tofauti zinazotumiwa kusambaza habari juu ya jambo fulani. Jadili.
2. Kwa maoni yako, barua huandikwa kwa mtindo gani?
3. Waraka ni nusu ya kuonana. Jadili.
4. Lengo la matangazo huwa na uhusiano wa karibu na jambo linalozungumziwa. Jadili.
5. Kwa sababu gani lugha ya mvuto hutumiwa sana katika matangazo ya biashara?

6. Katika uchanganuzi wa sentensi, sentensi hugawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu hizo ni zipi? Zinatofautianaje?
7. Katika uchanganuzi wa sentensi, njia ya matawi ilibuniwa na nani?
8. Andika tangazo la kibiashara ukitangaza uzuri wa kutumia dawa ya meno kila siku.

**Majibu**

1. Tangazo ni maandishi ambayo yanatoa na kusambaza habari juu ya jambo fulani ilhari barua ni risala au mjumbe mwepesi anayemwakilisha mtungaji wake kwa mtu mwingine na kuwasilisha taarifa yake kwa mtu huyo.

2. Kwa maoni yangu, barua huandikwa kwa mtindo wa nathari yaani maandishi ya kawaida yanayotumia aya.

3. Ni kusema kwamba mtu akimwandikia barua mwingine anapata habari na kujua hali yake lakini kwa nusu kuliko kuwa pamoja naye ana kwa ana.

4. Matangazo ni maandishi ambayo yanatoa na kusambaza habari juu ya jambo fulani na huainishwa kufuatana na shughuli au jambo linalozungumziwa. Kwa hiyo kuna matangazo ya serikali, matangazo ya biashara, matangazo ya kazi, matangazo ya kifo na kadhalika.
5. Lugha ya mvuto hutumiwa sana katika matangazo ya biashara kwa sababu huwa ni nyepesi kukumbukwa, inaeleweka kirahisi na huwatumia watu maarufu ili kuwashawishi walengwa.

6. Sehemu hizo ni kiima na kiarifu. “Kiima” ni kikundi cha nomino kinachofanya tendo linalopatikana katika kitenzi ilhali “Kiarifu” ni sehemu ya sentensi inayotawaliwa na kitenzi kinachoambatana na shamirisho/ kijalizo au chagizo na ambayo inatoa taarifa kamili.
7. Njia ya matawi ilibuniwa na Mwanaisimu Noam Chomsky.
8. Mwanafunzi atatunga tangazo kwa kuzingatia taratibu za utungaji wa matangazo ya kibiashara.

## MADA KUU YA 4: KUSOMA NA KUFASILI

## MADA NDOGO: UFAHAMU NA UFUPISHO

### 4.1. Uwezo upatikanao katika mada

- Kusoma, kufahamu na kufupisha vifungu vya habari mbalimbali;
- Kutumia kwa usahihi nyakati tofauti za kitenzi katika sentensi.

### 4.2. Ujuzi wa awali

Katika vidato vilivyopita, wanafunzi walikuwa wakifanya kazi za kusoma vifungu vya habari na kujibu maswali ya ufahamu. Kwa hiyo, somo la ufahamu si geni kwao. Pili, katika kidato cha nne wanafunzi waliona masomo yanayohusiana na ufupisho. Masomo hayo yanapatikana katika sura ya 3 ambayo ni "***Uhakiki wa hadithi za masimulizi katika Kiswahili***", yenye mada ndogo iitwayo "***Muhtasari, fani na maudhui***." Masomo yenyewe ni sawa na:

- Somo la 14: Maana ya muhtasari na sifa zake
- Somo la 15: taratibu za kutoa muhtasari mzuri

### 4.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake

#### 4.3.1. Kidokezo cha mada

Kwa kutangulia mada, mwalimu aulize maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua mada hii. Maswali hayo yanapaswa kuzingatia maudhui ya mada nzima. Hapa mwalimu anaweza kuuliza maswali yafuatayo:

- Ukimpasha habari mwenzako ni kitu gani kinachokufahamisha kwamba anakufuata?
- Unaposoma kifungu cha habari unakuwa na lengo gani?
- Ikiwa umesikia habari fulani na ukaagizwa kuisimulia wenzako utafanya nini?
- Ikiwa umesoma kifungu cha habari au kitabu ukaombwa kuwasimulia wenzako utafanya nini?

### 4.3.3. Maelekezo kuhusu kidokezo cha mada

- Mwalimu atoe mwongozo wa kutoa majibu kwa kazi.
- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia kazi nyingine zilizotayarishwa au masomo ya mada nzima.

## 4.4. Orodha ya Masomo

| | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | Dhana ya Ufahamu wa habari na taratibu zake | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya ufahamu wa habari.<br><br>**Stadi :** Kujadili dhana ya ufahamu wa habari.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuimarisha tabia ya kusoma vifungu vya habari tofauti. | 8 |
| 2 | Ufahamu wa kifungu cha habari kuhusu usafi wa mwili | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha taratibu za ufahamu wa kifungu cha habari.<br><br>**Stadi**: Kusoma na kujibu maswali ya ufahamu kutoka kifungu cha habari.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuwa na utaratibu wa kusoma kifungu cha habari ili kukielewa waziwazi. | 14 |
| 3 | Dhana ya Ufupisho wa habari na mbinu zake | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya ufupisho wa kifungu cha habari. | 16 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | **Stadi**: Kufafanua dhana ya ufupisho wa habari na mbinu zake.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuimarisha tabia ya kutumia lugha ya mkato, kuzungumza au kuandika kwa ufupi. | |
| - | Sarufi: Jedwali la muhtasari wa matumizi ya nyakati katika Kiswahili. | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha viambishi vya wakati (hali yakinishi na hali kanushi) katika Kiswahili<br><br>**Stadi :** Kutumia nyakati tofauti kwa usahihi.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujivunia matumizi sahihi ya nyakati katika Kiswahili. | - |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Vipindi vyote vya mada ya kwanza** | | | **40** |

**Tnbh:** Sarufi huja kila wakati ndani ya kila somo baada ya kufundisha msamiati.

☞ **Kila somo huwa na kazi za aina sita :**

- Kazi zinazohusu kusoma na ufahamu
- Kazi zinazohusu msamiati
- Kazi za sarufi
- Kazi zinazolingana na matumizi ya lugha
- Kazi za kusikiliza na kuzungumza
- Kazi za kuandika

## SOMO LA 1: DHANA YA UFAHAMU WA HABARI NA TARATIBU ZAKE

### i. Malengo ya ujifunzaji

Katika somo hili, mwanafunzi ataweza:

- Kueleza dhana ya ufahamu wa habari
- Kujadili dhana ya ufahamu wa habari

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Ubao,
- Chaki,

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

**iv. Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.227)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kutazama picha (mchoro) na kueleza yanayoendelea.*

**Dokezo**

Kwenye picha (mchoro) kuna mwalimu ambaye anafundisha somo la "*Ufahamu wa habari*." Na wanafunzi wanakaa darasani wakimfuata mwalimu.

***Kazi ya 2: (uk.227)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu cha habari na kukihusisha na picha (mchoro).*

Kwenye picha (mchoro), tunaona mwalimu ambaye anafundisha somo la "Ufahamu wa habari". Kifungu cha habari nacho kinazungumzia kuhusu "ufahamu wa habari".

**Kusoma na ufahamu: Mbinu zinazofuatiliwa katika ufahamu wa habari**

***Kazi ya 3: (uk. 229)***

*Katika makundi yao, mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu upya na kujibu maswali ya ufahamu.*

1. Ufahamu wa habari ni dhana inayorejelea kujua na kulielewa jambo kwa usahihi ili kuweza kulieleza upya kwa usahihi bila kupotosha maana yake ya msingi.

2. Ili kufahamu habari anapoisoma, mwanafunzi wa kidato cha tano anatakiwa kufanya hivi:

   - Kubaini mawazo makuu;
   - Kutilia mkazo alama za vituo;
   - Kubaini maana ya maneno na misemo tofauti;
   - Kumakinikia kila kipengele anachokisoma.
3. Ili kuifahamu habari anapoisimuliwa, mwanafunzi huyo atafanya hivi:

- Kuwa na makini na kuelekeza akili yote kwa mzungumzaji ili asikie vizuri kinachosemwa;
- Kuzingatia vidokezo vya maana ili kujua iwapo msemaji anafafanua au anaongeza jambo jipya;
- Kuandika baadhi ya mambo muhimu ili yamsaidie katika kukumbuka hapo baadaye;
- Kumakinikia ishara mbalimbali za mwili (kama vile kunyosha mkono, kutingisha kichwa, kupepesa macho na kadhalika).

4. Ni muhimu kubaini maana ya maneno na misemo tofauti katika kuisoma habari ili kuifahamu zaidi kwani ndipo tunaelewa vema maana ya maneno aliyoyatumia mwandishi.

**Msamiati (uk. 229)**

***Kazi ya 4 :*** Eleza maana ya maneno yafuatayo:

1. Kupotosha 2. Kubaini 3. Kurekodi 4. Kupepesa

- *Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kutoa maana za maneno. Kwa mfano:*

- **Kupotosha**: Kitu kuharibika kwa kupoteza sifa kilichokuwa nayo
- **Kubaini**: Kueleza waziwazi; kufafanua
- **Kurekodi**: Kuhifadhi mambo kama vile kwa maandishi au kwa kuyanasa katika kinasasauti au sahani za santuri kwa ajili ya matumizi ya baadaye
- **Kupepesa**: Kuchezesha kope kwa kuzipeleka juu na chini kwa haraka; kukopesa

***Kazi ya 5:*** Katika jozi, tungeni sentensi moja kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafuzi ametunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno aliyopewa.*

**Sarufi: Matumizi ya nyakati za Kiswahili (uk. 242)**

***Kazi ya 6:*** Taja nyakati kuu zinazoweza kutumiwa katika sentensi ya Kiswahili.

- ➢ *Kazi hii ifanyike katika jozi. Mwalimu awaagize wanafunzi kutaja nyakati kuu za Kiswahili. Nyakati hizo ni:*

- Wakati uliopo;
- Wakati uliopita;
- Wakati ujao;
- Wakati uliotimilika;
- Wakati wa mazoea

***Kazi ya 7:*** *Katika makundi yao madogomadogo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma maelezo kuhusu nyakati (☞Kitabu cha mwanafunzi, uk.244)***.** Kila kundi litasoma maelezo na kutoa wasilisho darasani.

**Matumizi ya lugha (uk. 230)**

***Kazi ya 8:*** Kwa njia ya mazungumzo, fuata muundo huu wa sentensi na kutoa maelezo kuhusu ufahamu wa habari wa kusikiliza na kuandika:

| | |
|---|---|
| Katika ufahamu wa habari wa kusikiliza, msikilizaji anatakiwa: | kumakinikia ishara za mwili |
| | ........................................................................ |
| | ........................................................................ |
| | ........................................................................ |
| Katika ufahamu wa habari wa kusoma, anayesoma anatakiwa: | kubaini mawazo makuu |
| | ........................................................................ |
| | ........................................................................ |
| | ........................................................................ |

- *Kazi hii ifanyike kwa njia ya mazungumzo. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujaza jedwali kuhusu ufahamu wa kusikiliza na wa kuandika (Swali lilirekebishwa).*

| | |
|---|---|
| Katika ufahamu wa habari wa kusikiliza | Msikilizaji anatakiwa kumakinikia ishara za mwili. |
| | kuwa na makini na kuelekeza akili yote kwa mzungumzaji |
| | kuzingatia vidokezo vya maana |
| | kuandika baadhi ya mambo muhimu |
| Katika ufahamu wa habari wa kusoma | kubaini mawazo makuu |
| | kutilia mkazo alama za vituo |
| | kubaini maana ya maneno na misemo tofauti |
| | kumakinikia kila kipengele anachokisoma |

***Kazi ya 9:*** Soma kwa makini kifungu cha habari hiki "**Usafi wa mwili**" ili uweze kuyajibu maswali ya ufahamu:

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu. Mapendekezo ya majibu ni haya yafuatayo:*

1. Mambo manne yanayoweza kuhusika na usafi:
   - Mazingira yetu (kama vile usafi wa nyumba);
   - Vitu tunavyotumia katika kazi mbalimbali (kama vile usafi wa vyombo vya jikoni);
   - Lugha tunayotumia (kama vile usafi wa lugha au maneno);
   - Roho zetu (kama vile usafi wa roho yaani kutakasa roho zetu kutokana na sala);
   - Mwili wetu (Mfano: Usafi wa meno) na kadhalika.
2. Kumfunza mtoto kuhusu usafi wa mwili ni jambo muhimu kwa sababu ni njia bora kabisa ya kumwepusha na maadhara mengi.

3. “Baadhi ya watu hawana budi kutohusika na usafi wa mwili”. Kauli hii ni ya uongo kwani kila mtu (awe mtoto au mkubwa, mtu mzima au mlemavu,... anahusika na usafi wa mwili.
4. “Shule za chekechea”: Ni shule za wale watoto wachanga ambao hawajafikia umri wa kuanza shule za msingi; “Shule za msingi” ni shule zinazotoa mafunzo ya kwanza ambayo ni kama nguzo ya elimu maishani mwetu.
5. Usafi wa kinywa ni muhimu sana kwa sababu madhara yanayoweza kusababishwa na uchafu wa sehemu hizo ni mengi. Meno machafu huweza kuoza na kuvunjika, fizi inaweza kuvimba, kuoza na kutoa harufu mbaya na kadhalika.
6. Tunatakiwa kusugua meno mara kwa mara hasa hasa:
   - Asubuhi tunapoamka kabla ya kifunguakinywa;
   - Kila mara baada ya chakula hasa vyakula vyenye sukari;
   - Usiku kabla ya kulala.
7. Tunalazimishwa kunawa mikono yetu kwa ukawaida yaani:
   - Baada ya kutoka chooni;
   - Kabla ya kutayarisha, kuhudumia au kula chakula;
   - Baada ya kupiga chafya, kukohoa au kupenga kamasi;
   - Baada ya kutupa takataka;
   - Kabla na baada ya kumtembelea mgonjwa;
   - Baada ya kumgusa mnyama au kinyasi cha mnyama;
   - Baada ya kumbadilishia nepi mtoto au kumsaidia kutumia choo;
   - Kabla na baada ya kutibu jeraha au kidonda na kadhalika.
8. Kitendo cha kuosha mikono kinafanyika namna hii:
   - Lowesha mikono yako katika maji safi ya bomba na kisha utumie sabuni;
   - Sugua mikono yako pamoja ili kupata povu. Usisahau kusafisha kucha, vidole, pande zote za mkono na katikati mwa vidole vyako;
   - Endelea kusugua kwa sekunde ishirini (20) hivi;
   - Safisha mikono yako katika maji safi;
   - Kausha mikono yako kwa kutumia kitambaa safi au karatsi ya kukaushia mikono.

9. Ni lazima nguo za ndani za mtu ziwe safi kwa sababu zikivaliwa kwa muda mrefu bila kubadilishwa hutoa harufu mbaya na hivyo, chawa nao huweza kujitokeza na kuyahatarisha maisha yake.

**Kusikiliza na kuzungumza**

***Kazi ya 9 :***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze wanafuzi kujadiliana kuhusu swali lifuatalo: "Ni muhimu kwa kubaini maana ya maneno na misemo tofauti katika kuisoma habari ili kuifahamu zaidi."*

Dokezo

Ni muhimu kubaini maana ya maneno na misemo tofauti katika kuisoma habari ili kuifahamu zaidi kwani ndipo tunaelewa vema maana ya maneno aliyoyatumia mwandishi.

**Kuandika**

***Kazi ya 10 :***

*Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunze ametunga hadithi kwa kuzingatia matumizi ya nyakati za vitenzi vya Kiswahili.*

## SOMO LA 3: DHANA YA UFUPISHO WA HABARI NA MBINU ZAKE

### i. Malengo ya ujifunzaji

Katika somo hili, mwanafunzi ataweza:

- Kueleza dhana ya ufupisho wa kifungu cha habari.
- Kufafanua dhana ya ufupisho wa habari na mbinu zake.

### ii. Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- ➢ Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- ➢ Kitabu cha mwanafunzi,
- ➢ Redio,
- ➢ Rekoda,
- ➢ Runinga,
- ➢ Ubao,
- ➢ Chaki, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu fulani.

### iii. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.

- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi kwa njia ya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

iv. **Majibu**

***Kazi ya 1: (uk.236)***

*Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaelekeze waafunzi kwna kutazama mchoro (picha) na kueleza yanayoendelea kwenye picha (mchoro) hiyo.*

**Dokezo**

Mwalimu na wanafunzi wake wanaongea kuhusu "sifa za ufupisho wa habari."

***Kazi ya 2: (uk.236)***

*Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kusom kifungu na kukihusisha na picha (mchoro).*

**Dokezo**

Kifungu cha habari kinazungumzia "ufupisho wa habari" na picha inaonyesha mwalimu na wanafunzi wake wakiongea kuhusu "ufupisho wa habari huo".

**Kusoma na ufahamu: Mbinu zinazofuatiliwa katika ufupisho wa habari**

***Kazi ya 3: (uk.238)***

*Kwa kupitia makundi madogomadogo, mwalimu awaagize wanafunzi kusoma kifungu upya na kujibu maswali ya ufahamu.*

**Majibu**

1. Ufupisho wa habari ni ustadi wa kuiandika upya kwa ufupi habari uliyoisoma. Ufundi huo hulenga kuisoma habari, kuielewa vizuri (yaani kuifahamu) na kuweza kuieleza au kuiandika upya kwa maneno machache ukiyalinganisha na yale ya awali.

2. Umuhimu wa somo la ufupisho wa habari kwa mwanafunzi ni kuwawezesha kupima ufahamu wao na uwezo wao wa kujieleza kwa maneno machache.
3. Ni lazima kutumia "ubahiri wa maneno" katika zoezi la kufupisha habari kwa sababu ufupisho huwa mfupi kuliko habari ya mwanzo. Hivyo, ni lazima kutumia maneno machache iwezekanavyo ili kuyaeleza mambo mengi iwezekanavyo.

4. Mfupishaji hufanikisha shughuli au kazi yake ikiwa wazo kuu au dhamira kuu iliyozungumziwa katika habari imeelezwa kwa kifupi na ikiwa maelezo yanayotolewa yanajitegemea, yaani ikiwa yametolewa bila kuirudia habari asilia.

**Msamiati (uk. 239)**

***Kazi ya 4:*** Eleza maana za maneno yafuatayo :

1. Kulenga 2. Kufanikisha 3. Upungufu 4. Hatua 5. Aya

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kutoa maana za maneno. Mifano:*

- **Kulenga**: Kutuliza macho mahali kwa kusudi la kupata shabaha
- **Ligi**: Mkusanyiko wa timu za michezo kama vile klabu za mpira wa miguu zinazopambanishwa ili kupata mshindi au bingwa
- **Radhi**: Hali ya nafsi kuridhika au kutosheka na matendo ya mtu
- **Niwie radhi**: Ninakuomba msamaha

***Kazi ya 5:*** Katika jozi, tungeni sentensi moja kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

- *Katika makundi madogomadogo, mwalimu awaagize wanafunzi kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno waliyopewa. Kila kundi litatunga sentensi zake.*

**Sarufi**

**Kazi ya 6:** *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Kwa njia ya mazungumzu, mwalimu awaagize wanafunzi kujadiliana kuhusu kauli ifuatayo: "Maana ya sentensi hutegemea sana matumizi ya nyakati." Eleza kinagaubaga.*

*Dokezo*

"Maana ya sentensi hutegemea sana matumizi ya nyakati". Nyakati ndizo zinazoonyesha iwapo kitendo kilitendeka wakati uliopita, kinatendeka wakati huu ama kitatendeka wakati ujao. Na sentensi inafuata maana hiyo.

**Kazi ya 7:** *Kazi hii ifanyike katika makundi. Mwalimu awaagize wanafunzi kukanusha na kuyakinisha sentensi hizi:*

1. Yeye alikuwa mchezaji hodari.
2. Mwanafunzi hajaja.
3. Mvua ilinyesha jana.
4. Wao hawatafika kesho.
5. Sisi hatuwapendeleipendelei.
6. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
7. Atakapofika tutampokea vizuri.
8. Ningekuwa na fedha nengenunua gari.
9. Usipoomba hutapewa.
10. Wao hupenda ngoma za jadi.

**Majibu**

1. Yeye hakuwa mchezaji hodari.
2. Mwanafunzi amekuja.
3. Mvua haikunyesha jana.
4. Wao watafika kesho.
5. Sisi tunawapendeleapendelea.
6. Anayesikia la mkuu havunjiki guu.
7. Asipofika hatutajitayarisha.
8. Nisingekuwa na fedha nisingenunua gari.

9. Ukiomba utapewa.
10. Wao hawapendi ngoma za jadi.

**Matumizi ya lugha *(uk.239)***

***Kazi ya 8:*** *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kujaza jedwali. Mapendekezo ya majibu ni haya:*

| Sifa za ufupisho | Hatua zinazofuatiliwa katika kufupisha habari |
|---|---|
| • Huwa ni mfupi kuliko habari ya mwanzo. Kwa hiyo, ni lazima "ubahiri wa maneno" utumiwe;<br>• Huwa na ujumbe ule ule uliokuwa katika habari ya mwanzo;<br>• Hujumuisha mawazo makuu yaliyodondolewa kutoka habari ya mwanzo;<br>• Mawazo haya makuu sharti yapangwe katika mtiririko wenye mantiki. | • Kuisoma au kuisikiliza habari kwa makini na mara nyingi ili kuielewa vizuri. Hatua hii ndiyo iitwayo "ufahamu wa habari";<br>• Kutambua na kubaini mawazo makuu yanayojitokeza katika kila aya;<br>• Kuyaunganisha mawazo makuu na kuandika au kuelezea ufupisho wa habari hiyo kwa maneno yako mwenyewe bila kupotosha maana ya habari ya kwanza;<br>• Kuhesabu idadi ya maneno ya ufupisho ili kuyapunguza ikiwa yanazidi idadi iliyotakiwa;<br>• Pitia tena habari ya mwanzo kisha upitie tena ufupisho ili kujiridhisha kuwa hujaacha taarifa yoyote ya muhimu. |

**Kusikiliza na kuzungumza (uk. 241)**

***Kazi ya 9:*** Kwa kushirikiana na mwenzako, kumbukeni hadithi moja mliyoisoma au kusikiliza, kisha toeni muhtasari wake mbele ya darasa.

- *Kazi hii ifanyike kwa makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kukumbuka hadithi waliyosoma au waliyosikiliza na kutoa muhtasari wake kwa nja ya mazungumzo. Kila kundi lifanye kazi yake pekee.*

**Kazi ya 10:** Fuata habari kwenye redio au runinga kwa kuandika mawazo muhimu, kisha andika ufupisho wa habari hiyo na kuwasimulia wenzako kuhusu habari hiyo.

- *Kazi hii ifanyike katika makundi madogomadogo. Mwalimu awaagize wanafunzi kusikiliza habari kwenye redio au runinga, kuandika mawazo makuu, kufupisha na kuwasilisha mabele ya wenzao. Kila kundi liwasilishe kazi yake.*

**Kuandika (uk. 240-241)**

***Kazi ya 11:*** Katika jozi, someni kifungu cha habari kifuatacho " **Mazao ya biashara na fedha za kigeni**" na kufanya muhtasari wake. Ufupisho huo uwe 1/3 ya kifungu cha habari chote.

- *Kazi hii ni ya mwanafunzi binafsi. Mwalimu amweelekeze mwanafunzi kwa kusoma kifungu na kukifupisha.*

## 4.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

### 4.5.1. Maelekezo ya ziada kwa mwalimu

Katika mada hii tumeongeza kazi mbalimbali ambazo zitamwongoza mwalimu kufanikisha kazi yake. Katika masomo yote ya mada hii tumeingiza sarufi. Kazi za sarufi nyingi zimo katika Kitabu cha Mwanafunzi. Mwalimu alielekezwa kwa namna ya kutafuta kazi hizo katika Kitabu cha Mwanafunzi. Zile ambazo hazipatikani ndani ya Kitabu cha Mwanafunzi ni zile zilizotayarishwa upya ili kukamilisha zile zilizomo katika kitabu cha mwanafunzi.

### MASWALI YA ZIADA KWA TATHMINI YA MADA

1. Ufahamu wa habari ni nini?
2. Mwanafunzi wa kidato cha tano anatakiwa kufanya nini ili kufahamu habari anapoisoma?
3. Mwanafunzi huyo atafanya nini ili kufahamu habari anapoisimuliwa?
4. Eleza maana ya "ufupisho wa habari."
5. Kwa nini ni lazima kutumia "ubahiri wa maneno" katika ufupisho?
6. Taja sifa za ufupisho mzuri.
7. Ka sababu gani somo la ufupisho hutegemea lile la ufahamu?
8. Taja mambo manne yanayoweza kuhusika na usafi.
9. Ni wakati gani tunalazimishwa kunawa mikono yetu?
10. Tofautisha "shule za chekechea" na "shule za msingi"

11. Kanusha au uyakinishe sentensi zifuatazo

a) Mvua isingelinyesha asubuhu mapema tusingelichelewa kufika shuleni
b) Kijana yule alikua vizuri.
c) Kijana yule alikuwa mzuri
d) Wezi walikuvamia.
e) Usipomwaadhibu mtoto hatapata adabu njema.

**Majibu**

1. Ufahamu wa habari ni dhana inayorejelea kujua na kulielewa jambo kwa usahihi ili kuweza kulieleza upya kwa usahihi bila kupotosha maana yake ya msingi.
2. Ili kufahamu habari anapoisoma, mwanafunzi wa kidato cha tano anatakiwa kufanya hivi:

- Kubaini mawazo makuu;
- Kutilia mkazo alama za vituo;
- Kubaini maana ya maneno na misemo tofauti;
- Kumakinikia kila kipengele anachokisoma.

3. Ili kuifahamu habari anapoisimuliwa, mwanafunzi huyo atafanya hivi:

- Kuwa na makini na kuelekeza akili yote kwa mzungumzaji ili asikie vizuri kinachosemwa;
- Kuzingatia vidokezo vya maana ili kujua iwapo msemaji anafafanua au anaongeza jambo jipya;
- Kuandika baadhi ya mambo muhimu ili yamsaidie katika kukumbuka hapo baadaye;
- Kumakinikia ishara mbalimbali za mwili (kama vile kunyosha mkono, kutingisha kichwa, kupepesa macho na kadhalika).

4. Ufupisho wa habari ni ustadi wa kuiandika upya kwa ufupi habari uliyoisoma. Ufundi huo hulenga kuisoma habari, kuielewa vizuri (yaani kuifahamu) na kuweza kuieleza au kuiandika upya kwa maneno machache ukiyalinganisha na yale ya awali.
5. Ni lazima kutumia “ubahiri wa maneno” katika zoezi la kufupisha habari kwa sababu ufupisho huwa mfupi kuliko habari ya mwanzo. Hivyo, ni lazima kutumia maneno machache iwezekanavyo ili kuyaeleza mambo mengi iwezekanavyo.
6. Ufupisho

- Huwa ni mfupi kuliko habari ya mwanzo
- Huwa na ujumbe ule ule uliokuwa katika habari ya mwanzo;
- Hujumuisha mawazo makuu yaliyodondolewa kutoka habari ya mwanzo;
- Mawazo haya makuu sharti yapangwe katika mtiririko wenye mantiki.

7. Kwa sababu mtu anafupisha mambo ambayo ameyaelewa yaani kufahamu.
8. Mambo manne yanayoweza kuhusika na usafi:

- Mazingira yetu (kama vile usafi wa nyumba);
- Vitu tunavyotumia katika kazi mbalimbali (kama vile usafi wa vyombo vya jikoni);
- Lugha tunayotumia (kama vile usafi wa lugha au maneno);
- Roho zetu (kama vile usafi wa roho yaani kutakasa roho zetu kutokana na sala);
- Mwili wetu (Mfano: Usafi wa meno) na kadhalika.

9. Wakati wa kunawa mikono yetu:

- Baada ya kutoka chooni
- Kabla ya kutayarisha, kuhudumia au kula chakula;
- Baada ya kupiga chafya, kukohoa au kupenga kamasi;
- Baada ya kutupa takataka;
- Kabla na baada ya kumtembelea mgonjwa;
- Baada ya kumgusa mnyama au kinyasi cha mnyama;
- Baada ya kumbadilishia nepi mtoto au kumsaidia kutumia choo;
- Kabla na baada ya kutibu jeraha au kidonda na kadhalika.

10. “Shule za chekechea” ni shule za wale watoto wachanga ambao hawajafikia umri wa kuanza shule za msingi ilhali “Shule za msingi” ni shule zinazotoa mafunzo ya kwanza ambayo ni kama nguzo ya elimu maishani mwetu.)
11. Kanusha au uyakinishe sentensi zifuatazo:

a) Mvua ingelinyesha asubuhi mapema tungelichelewa kufika shuleni.
b) Kijana yule hakukua vizuri.
c) Kijana yule hakuwa mzuri.
d) Wezi hawakukuvamia.
e) Ukimwaadhibu mtoto atapata adabu njema.

## 4.6. TATHMINI YA MADA YA NNE

***Maswali ya tathmini ya mada (☞Uk.248)***

1. Kuchagua hadithi na kutayarisha maswali
2. Kutoa ufupisho wa hadithi
3. Kutunga sentensi

## 4.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI

Kazi hihzi ni kazi za kwasaidia wanafunzi kulingana na viwango vyao vya uelewa kuhusu mada husika. Katika kazi hizo kuna kazi za urekebishaji, kazi za uimarishaji na kazi za wanafunzi wenye uelewa wa haraka.

### 4.7.1. Kazi za urekebishaji

Mapendekezo ya maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wasio na uelewa wa haraka.

1. Ufahamu ni nini?
2. Neno ufahamu linatokana na kitenzi gani? Kinamaanisha nini?
3. Kuna aina gani za ufahamu?
4. Ufupisho ni nini?
5. Taja nyakati kuu za vitenzi vya kiswahili.
6. Kanusha au uyakinishe sentensi zifuatazo :
   a. Yeye alikuwa hapa jana.
   b. Mvua haitanyesha kesho.
   c. Jua limechomoza.
   d. Mzazi yule hakuzaa mapacha.
   e. Yeye hali ugali.

**Majibu**

1. Ufahamu wa habari ni dhana inayorejelea kujua na kulielewa jambo kwa usahihi ili kuweza kulieleza upya kwa usahihi bila kupotosha maana yake ya msingi.

2. Neno ufahamu linatokana na kitenzi “kufahamu” kinachomanisha “kujua”.

3. Kuna ufahamu wa kusoma na ufahamu wa kusikiliza.

4. Ufupisho ni ustadi wa kuiandika upya kwa ufupi habari uliyoisoma au uliyoisikia.

**5.** Kuna wakati uliopo, wkati uliopita, wakati uliotimilika, wakati ujao na wakati wa mazoea.

6. Kukanusha

a. Yeye hakuwa hapa jana.

b. Mvua itanyesha kesho.

c. Jua halijachomoza.

d. Mzazi yule alizaa mapacha.

e. Yeye hula/anala ugali.

### 4.7.2. Kazi za uimarishaji

1. Katika ufahamu wa kusikiliza msikilizaji hana buni kumakinikia ishara mbalimbali za mwili azitumiazo mzungumzaji. Ni kumaanisha nini?
2. Taja mambo ya kutiliwa mkazo katika ufahamu wa kusoma
3. Somo la ufupisho wa habari lina umuhimu gani kwa mwanafunzi?
4. Ni tofauti gani iliyoko baina ya wakati uliopo na wakati wa mazoea ?
5. Kuyakinisha au kukanusha sentensi

a. Njoo hapa!

b. Yeye alikuwa akirandaranda mitaani.

c. Mgomba ule haukukua vizuri.

d. Ukistaajabu ya Musa utaona ya firauni.

e. Kama angalijua kwamba angalitoboa siri asingalimwambia.

6. Kwa kufuata kanuni za ufupishaji, fupisha hadithi ya « Chura na Jongoo ».

**Majibu**

1. Ni kumaanisha kuwa msikilizaji anapaswa kuwa makini kwa ishara anazotumia mzungumzaji ili aweze kuelewa anayoyasema.
2. Mambo ya kutiliwa mkazo katika ufahamu wa kusoma :

- Kubaini mawazo makuu
- Kutilia mkazo alama za vituo
- Kubaini maana ya maneno na misemo tofauti
- Kumakinikia kila kipengele anachokisoma
- Kumakinikia kila kipengele anachokisoma

3. Umuhimu wa somo la ufupisho wa habari kwa mwanafunzi ni kuwawezesha kupima ufahamu wao na uwezo wao wa kujieleza kwa maneno machache.
4. Wakati uliopo unawakilishwa na kiambishi wakati -na- katika hali yakinishi, wakati huu huontenda tendo linalotendeka sasa ilhali wakati wa mazoea huwakilishwa na kiambishi wakati hu- na huonyesha tendo ambalo hutendwa kwa kawaida.
5. Kukanusha au kuyakinisha sentensi sifuatazo:

   a) Usije hapa!
   b) Yeye hakuwa akirandaranda mitaani/ yeye alikuwa harandarandi mitaani.
   c) Mgomba ule ulikua vizuri.
   d) Usipostaajabu ya Musa hutaona ya firauni.
   e) Kama asingalijua kwamba asingalitoboa siri, angalimwambia.

6. Kila mwanafunzi afupishe hadithi ya « Chura na Jongoo »

### 4.7.3. Kazi za wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Mapendekezo ya maswali na majibu kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka:

1. Je, inawezekana kufanya ufupisho wa habari bila ufahamu?
2. Ajue au la, kazi ya ufahamu ni zoezi linalofanywa na kila mtu maishani mwake. Jadili.
3. Kwa nini ni lazima mwandishi awe bahili katika maneno yake ili aweze kufupisha habari?
4. Ufahamu ni tofauti na uhakiki. Jadili.

5. "Maana ya sentensi hutegemea sana matumizi ya nyakati". Jadili.
6. Katika kitenzi dhana ya wakati huonyeshwa na nini?
7. Kanusha au uyakinishe sentensi zifuatazo:
a) Atakapohudhuria mkutano huo ataelewa vema sera za serikali.
b) Ningelifahamu tabia zake za wizi nisingemkaribisha kwangu.
8. Kwa kuzingatia kanuni zote za ufupishaji, kumbuka hadithi uliyosoma katika kidato cha nne kisha uifupishe.

**Majibu**

1. Hapana! Haiwezekani kufanya ufupisho bila ufahamu kwa sababu kabla ya kufupisha habari anapaswa kuieleza yaani ufahamu.
2. Kazi ya ufahamu ni zoezi linalofanywa na kila mtu maishani mwake kwa sababu katika maisha yake ya kila siku yeye huwasiliana na wengine. Katika mawasiliano yetu kuna wakati tunaelewa au tukashindwa kuelewana. Kuelewana huko ndiyo kazi ya ufahamu.
3. Neno bahili ni kumaanisha mnyimi. Ni lazima kutumia mwandishi awe bahili katika maneno yake katika zoezi la kufupisha habari kwa sababu ufupisho huwa mfupi kuliko habari ya mwanzo. Hivyo, ni lazima kutumia maneno machache iwezekanavyo ili kuyaeleza mambo mengi iwezekanavyo.
4. Ufahamu ni dhana inayorejelea kujua na kulielewa jambo kwa usahihi ili kuweza kulieleza upya kwa usahihi bila kupotosha maana yake ya msingi ilhali uhakiki ni kazi/ kitendo cha kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalumu.
5. Nyakati ndizo zinazoonyesha iwapo kitendo kilitendeka wakati uliopita, kinatendeka wakati huu ama kitatendeka wakati ujao. Na sentensi inafuata maana hiyo.
6. Dhana ya kitenzi huonyeshwa na kiambishi wakati.
7. Kukanusha na kuyakinisha sentensi
a) Asipohudhuria mkutano huo hataelewa vema sera za serikali.
b) Nisingelifahamu tabia zake za wizi, ningelimkaribisha.

8. Mwanafunzi atafupisha hadithi kulingana na taratibu za ufupishaji.

## MAREJEO


1. **ABDILAHI Nassir**, Tamrini za Kiswahili: Kitabu cha pili, Nairobi, Oxford University Press, 1974
2. **Co-Publishing Committee**, Hadithi za kwetu, Nairobi, Co-Publishing Committee, 1987
3. **INTANETI**, Tovuti mbalimbali, Julai 2015
4. **INTANETI**, Tovuti mbalimbali, Julai 2015
5. **MBUNDA Msokile**, Misingi ya uhakiki wa fasihi, East African Educational Publishers Ltd, Nairobi, 1993
6. **MINEPRISEC**, Ikinyarwanda: Gusoma no gusesengura imyandiko, Kigali, Nzeri 1982
7. **Mohamed, M.A. & Saidi, A.M**, Kamusi ya Visawe, Nairobi, East African Educational Publishers Ltd, 2002
8. **Mohamed, A.M.,** Sarufi Mpya, Dat-es-salaam, Press and Publicity Centre, 1986
9. **Mulokozi, M.M**., Fasihi ya Kiswahili, Dar-es-Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, 1996
10. **Mulokozi, M.M.,** Tenzi Tatu za Kale, Dar-es-Salaam, TUKI, 1999
11. **NICKY STANTON**, Mastering Communication, Hampshire, Macmillan Master Series, 1996
12. **NKWERA, F.M**., Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo, Dar-es-salaam, TPH, 1978
13. **OXFORD University Press**, Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Nairobi, Kenya, 2007
14. **Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari**, Kitabu cha Kiswahili III B, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari, Agosti 1987
15. **Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari**, Kitabu cha Kiswahili IV-VA, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari, Novemba 1987
16. **Wamitila, K.W.,** Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia, Nairobi, Focus Publications Ltd, 2003